

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Pili – Tarehe 2 Novemba, 2016**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae.

Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kama kawaida tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Ezekiel Maige, kwa niaba Mheshimiwa Mwambalاسwa!

Na. 16

**Kuanzisha Mfuko wa Maafa Kitaifa**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. EZEKIEL M. MAIGE)** aliuliza:-

Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi matukio ya majanga na maafa kama mvua za mawe pamoja na matetemeko ya ardhi yameanza kutokea mara kwa mara na mara zote Serikali imekuwa haina maandalizi ya kifedha na vifaa vya kusaidia wahanga kwa muda mfupi na muda mrefu na badala yake imekuwa ikitegemea zaidi wasamaria wema wa Mataifa mengine:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali imekuwa haisaidii kifedha na vifaa zaidi ya kuhamasisha wasamaria wema wasaidie na wenyewe kubaki na jukumu la kupeleka wataalam kama Madaktari na kuratibu misaada pekee?

(b) Je, ni kwa nini Serikali isianzishe Mfuko wa Maafa Kitaifa ambao utakuwa unachangiwa wakati wote kwa njia endelevu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali inatambua kuwa ni wajibu wake kusaidia wananchi pindi wanapokumbwa na maafa yanayoharibu mfumo wa maisha ya kila siku. Katika kutekeleza wajibu huo Serikali imekuwa ikitoa misaada ya aina mbalimbali kwa waathirika wa maafa ikiwemo vyakula, malazi, vifaa vya kibinadamu na huduma za afya.

Vilevile Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya kununua mahitaji ya dharura ya kibinadamu pamoja na kurejesha miundombinu iliyoharibika. Aidha, katika jitihada za kuhakikisha kuwa misaada inawafikia wananchi kwa haraka Serikali tayari ina maghala ya maafa yenye vifaa mbalimbali vya kukabiliana na maafa katika Kanda sita nchini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema ifahamike kuwa suala la kukabiliana na maafa ni mtambuka na haliwezi kuachwa mikononi mwa Serikali peke yake kwani wakati mwingine maafa yanakuwa ni makubwa sana hivyo kuhitaji juhudi za pamoja baina ya Serikali, wadau wa maendeleo na wananchi katika kuyakabili na kurejesha hali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo Serikali ilileta Muswada wa Sheria ya Maafa uliopitishwa na Bunge lako Tukufu na kuwa Sheria Namba 7 ya mwaka 2015 ambayo pamoja na mambo mengine inaelekeza kuanzishwa kwa Mfuko wa Maafa na pia, Kifungu 31 kinaainisha vyanzo vya mapato vya Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa wadau wa maendeleo pamoja na wananchi kwa ujumla kuendelea kushirikiana na Serikali katika harakati zake za kujiandaa, kukabili na kurejesha hali, ili kuhakikisha jamii yetu inakuwa salama zaidi dhidi ya majanga mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambalاسwa.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwona mwenye swali Mheshimiwa Maige amefika, kama inaruhusiwa; kama hairuhusiwi, basi niulize.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Swali la kwanza; tarehe 3 Machi, 2015 kulitokea maafa ya mvua kwenye eneo la Mwakata kwenye Jimbo langu na watu 47 wakafa na misaada mingi ilikusanywa. Kwa bahati mbaya sana kumekuwepo usimamizi usioridhisha wa matumizi ya misaada ile na wananchi wamekuwa wakiwatuhumu aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Bwana Ali Nassoro Lufunga na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, lakini pia Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya Bwana Benson Mpesya, aliyekuwa Mkuu wetu wa Wilaya kwamba, misaada ambayo ililenga kuwafikia waathirika wa Mwakata haikuwafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua Serikali itasaidiaje kuhakikisha kwamba, taarifa sahihi ya fedha zilizokusanywa na misaada mingine kwa ajili ya maafa ya Mwakata inapatikana kutoka kwa watuhumiwa hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa, Serikali inakiri kwamba, maafa ni jambo ambalo halitabiriki na pia inakiri kwamba Serikali ina wajibu wa kusaidia wananchi. Hatutaki Serikali ilipe fidia au kufanya chochote, lakini ni kwa nini isiangalie uwezekano wa kuwa na Mfuko, kama tulivyopendekeza kwenye swali la msingi, ambao unakuwa unachangiwa kwa njia endelevu ili likitokea janga hata mnapokwenda kusaidia angalau mna mahali pa kuanzia kuepuka aibu ambayo inajitokeza kwa sasa kwamba, zinafika mpaka nchi nyingine kuja kusaidia, sisi kama Serikali tunawaomba na kuitisha harambee sisi hata shilingi moja ya kuanzia hatuna. Hivi Serikali haioni kwamba, ni aibu katika mazingira ya namna hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na upatikanaji wa taarifa sahihi kutoka kwa watu wanaotuhumiwa. Niseme tu si kupata taarifa sahihi, Serikali itafanya yote yanayowezekana kwa mujibu wa Sheria ili kupata taarifa sahihi na kama hao watuhumiwa wamefanya makosa basi hatua mbalimbali zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Maige ashirikiane na sisi, ili kuhakikisha kwamba, kweli kama kuna mtu ametumia fedha hizo vibaya, basi afikishwe katika mikono ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu Mfuko. Tayari Sheria imeanzisha Mfuko wa Maafa, ni tofauti na Sheria ile iliyotungwa mwaka 1990 ambayo Mfuko ulikuwa kwa ajili ya Kamati na haukuwa umeelezewa vizuri sana. Sheria hii imeanzisha Mfuko wa Maafa ambapo una vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala kwamba ni aibu kwa wananchi kuchangia, naomba niweke sawa; masuala kama ya tetemeko ni majanga makubwa sana na Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kuchangiwa. Nitoe tu mfano, Iran lilipotokea lile tetemeko kubwa nafikiri mwaka 2013, lililofikia *magnitude 7.7*, mashirika mbalimbali yalisaidia ikiwemo *National Federation of the Red Cross*.

Mwaka 2015, Nepal kwa mfano, tunaona Wafaransa, Norway na nchi kadhaa yalisaidia, sitaki kusema nini kilitokea Japan na Indonesia na maeneo mengine ambayo matetemeko yamekuwa yanatokea mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi pia tumesikia kwa mfano Italy, ilikuwa inaomba msaada *European Union* ili kuangalia ni namna gani itaweza kurejesha hali baada ya kupata matetemeko kati ya Agosti na Oktoba. Kwa hiyo, kutokana na ukubwa wa matetemeko haya ni vigumu nchi kuwa haisaidiwi na ndio maana hata Umoja wa Mataifa ina wakala maalum wa kusaidia maafa kwa majanga kama haya, matetemeko, mafuriko na majanga mengine ambayo hayatabiriki. Kwa hiyo, niseme si aibu ila ni hali ya kawaida na Mfuko huu umeanzishwa kwa Sheria. Kwa hiyo, swali la pili kuhusu Mfuko nadhani limejibiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kumekuwa na tatizo la Serikali kuwatishia Wakuu wa Wilaya ambao wilaya zao zitapata janga la njaa, kwamba watapoteza Ukuu wa Wilaya na hivyo kusababisha wasitoe takwimu halisi za upungufu wa chakula uliopo katika Wilaya zao. Wananchi wengi wamekuwa wakifa kutokana na njaa kwa kuficha wasijulikane kama kuna njaa wilayani kwao. Je, ni kwa nini chakula kinakuwepo wilaya nyingine au mikoa mingine kingi na wilaya nyingine hakipo, watu wanakufa njaa ndani ya nchi hii moja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, mwambie tu walime huko.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nafikiri tutofautishe njaa inapotokea katika mkoa ambapo hakuna sababu, kwamba mvua zipo, ardhi yenye rutuba ipo, watu wa kufanya kazi wapo. Tutofautishe na sehemu nyingine ambazo kuna baa la nzige, kweleakwelea, ukame, hivi ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, niseme

tu kwamba, Wakuu wa Wilaya hawatishiwi ila walikumbushwa kuwajibika pale ambapo rasilimali zipo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, swali la Mheshimiwa Aweso.

Na. 17

## HITAJI LA X-RAY HOSPITALI YA WILAYA YA PANGANI

**MHE. JUMA H. AWESO** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Pangani ina uhitaji wa X-Ray ili kutoa huduma hiyo kwa wananchi ambao hutembea mwendo mrefu kufuata huduma hiyo Tanga Mjini:-

Je, ni lini Serikali itapeleka X-Ray katika Hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani imeomba mkopo wa kiasi cha shilingi milioni 70 kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwa ajili ya ununuzi wa X-Ray mpya katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. X-Ray iliyopo ni chakavu kiasi cha kuhitaji matengenezo kila baada ya miezi mitatu kupitia wakala wake wa *Philips*. Kwa sasa wagonjwa wanapata huduma ya X-Ray kupitia Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri imefanya mawasiliano na NHIF kwa ajili ya kupata mkopo huo na mazungumzo yanaendelea. Aidha, Halmashauri zinashauriwa kuweka kipaumbele katika kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa X-Ray kutokana na umuhimu wake kwa afya za wananchi.

**MHE. JUMA H. AWESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya kumuuliza. Mimi kama Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Pangani sikubaliani na majibu ya Mheshimiwa Waziri ya kusema kwamba mazungumzo yanaendelea, ilhali wananchi wangu wakitaabika. Tunapozungumzia suala la X-Ray, tunazungumzia uhai wa wananchi wa Jimbo langu la Pangani. Leo wananchi wanatoka Muhungulu, Mkalamo wanafuata huduma ya X-Ray Tanga Mjini.

Sasa nataka nijue ni nini nguvu ya Serikali katika kuhakikisha kwamba inatupatia fedha za dharura ili X-Ray hii ipatikane kwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, pamoja na changamoto ya ukosefu wa X-Ray bado Hospitali yetu ya Wilaya imekuwa na changamoto lukuki za ukosefu wa dawa pamoja na vifaa tiba. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuongozana na mimi baada ya Bunge kuhakikisha kwamba, tunaenda kukabiliana na changamoto ambazo Hospitali yetu ya Wilaya inakabiliana nazo? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, mwambie uko tayari tu haina haja ya kupoteza muda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lolote haliwezi kukamilika bila ya mazungumzo, ndiyo maana halmashauri pale imefanya utaratibu wa kupata hii milioni 70 kutoka NHIF.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mbunge kwamba, utaratibu uliowekwa na halmashauri yake na yeye mwenyewe akiwa mjumbe wa Baraza la Madiwani; na nikijua kwamba yeye ni kijana mahiri anapambana sana juu ya suala la afya katika eneo lake; sisi tuta-*fast track* hiyo *process* ya kupata X-Ray haraka ili wananchi wa Pangani ambao kwa muda mrefu anawapigania waweze kupata huduma ya afya, lakini nimpongeze sana katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuongozana na Mheshimiwa Mbunge, naomba nimwambie kwamba, niko tayari. Baada ya Bunge, mpango wangu ni kutembelea Mikoa ya Tanga, Lindi, Mtwara, Pwani na Mkoa wa Morogoro. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba, tutafika Pangani na tutakagua eneo hilo. Hali kadhalika tutakagua kituo cha afya ambacho wanaendelea kukijenga ili tuone namna ya kukusanya nguvu za pamoja za kuhakikisha kwamba, wananchi wa Wilaya ya Pangani wanapata huduma ya afya. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Hospitali yetu ya Manispaa ya Iringa ilifunguliwa ili kupunguza msongamano mkubwa sana uliopo katika Hospitali ya Mkoa, lakini mpaka leo hii Hospitali hii haina mashine ya X-Ray wala *Ultra Sound*. Pia hospitali hii imekuwa ikihudumia mpaka wagonjwa wanaotoka Kilolo kwa sababu Kilolo pia Hospitali yao ya Wilaya imekaa vibaya kiasi kwamba wagonjwa wanaotoka kule Kilolo wanakuja kuhudumiwa katika hospitali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba, kama mashine hizi zingekuwepo zingeweza pia kuingiza pesa ili kuzisaidia ziweze kujiendesha. Je, Serikali sasa inaisaidiaje hospitali hii iweze kupata hizi mashine ili iweze kuhudumia wananchi waliopo katika Manispaa ya Iringa?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nasema ngoja nilichukue hili kwa sababu katika kuangalia kwa haraka haraka sikuweza kufahamu kwamba mpaka hivi vifaa vya X-Ray bado vina changamoto kubwa, lakini naomba tulichukue hili kwa ajili ya kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea kule Kilolo, nilijua kwamba watu wa Kilolo wote wanakuja kupata huduma pale na nilijua kwamba vifaa vyote vimekamilika. Jambo hili tutalifanyia kazi kwa pamoja ili Hospitali hii ya Manispaa iweze kutoa huduma bora kwa wananchi wote kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme kwamba tutashirikiana kwa pamoja na Mheshimiwa Ritta Kabati pamoja na Wabunge wengine wa huko ili hospitali ile ambayo ni *centre* kubwa sana ya magari makubwa yanayopita kutoka nchi za jirani kuja Tanzania iwe na uwezo wa kuwahudumia watu kwa kiwango kikubwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Rweikiza.

Na. 18

### **Kuweka Miundombinu kwa Ajili ya Kidato cha Tano na Sita Sekondari za Bukoba Vijijini**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Bukoba Vijijini kuna Shule za Sekondari za Serikali na za Wananchi zipatazo 29 ambazo zinaishia Kidato cha nne na moja kati ya hizo ina Kidato cha tano na sita hali, inayosababisha wahitimu wengi wanaomaliza Kidato cha nne wakiwa na sifa za kuingia Kidato cha tano kukosa nafasi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga madarasa na miundombinu inayofaa kwa Kidato cha tano na sita kwenye baadhi ya shule zilizopo ili kutatua tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba inaendelea na upanuzi wa miundombinu ya shule mbili za Lubale na Lyamahoro ili ziweze kuwa na sifa na vigezo kuwa Shule za Kidato cha tano na sita ifikapo Juni, 2017. Serikali imepanga kutumia fedha za *Performance for Results (P4R)* kukamilisha miundombinu katika shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa Tanzania Bara kuhakikisha kila Halmashauri inakuwa na angalau shule moja ya kidato cha tano na sita. Vileile kila Tarafa iwe na shule moja ya kidato cha tano na sita. Shule hizi ni za Kitaifa ambazo huchukua wanafunzi waliohitimu na kufaulu kidato cha nne katika mikoa yote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Ni dhahiri kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema kuna shule 29 za sekondari ambazo ni nyingi kwa shule moja ya *form five* na *six*. Hiyo shule moja ya *form five* na *six* sasa hivi haipo tena, baada ya tetemeko la ardhi imeharibika kabisa na imefungwa. Sasa Serikali haioni kwamba umuhimu umeongezeka baada ya shule hii kuharibika kabisa kuharibiwa na tetemeko la ardhi, kwamba juhudi zifanywe za ziada kujenga shule ya *form five* na *six*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa vile shule ya namna hii ni shule ya Kitaifa kwa nini jambo hili wanaachiwa halmashauri ndio washughulike nalo kutafuta fedha, kujenga wenyewe na isijengwe na Serikali Kuu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunajua kwamba, pale hali imekuwa ni mbaya na hasa katika ile shule ambayo imeporomoka zaidi, na hata hii Shule ya Lubale karibu nyumba mbili zimehaibika pamoja na baadhi ya madarasa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali italiwekea hili kipaumbele. Na ndiyo maana katika Mfuko huu wa Maafa ya Mkoa wa Kagera maeneo ya elimu tumeyapa kipaumbele cha kutosha.



Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ile shule iliyoharibika tutaijenga upya yote, lakini halikadhalika hii shule ya Lubale tutaweka nguvu kubwa sana kuhakikisha kwamba majengo yanarudi katika hali yake nzuri, ili vijana ambao wanasoma wapate elimu. Vile vile juhudi za Serikali kwenye janga hili ambalo limeupata Mkoa wa Kagera zitakuwa ni kupeleka nguvu za kutosha katika taasisi zote zilizopata uharibifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake linalohusu shule hizi kuwa ni shule za kitaifa na kwamba kwa nini inaachiwa Halmashauri? Ni kweli na ndiyo maana tumetoa maelekezo kwamba kila halmashauri ifanye hivyo kwa sababu wote tunaunga mkono nguvu moja nguvu ya Kitaifa na ndiyo maana hata mpango wa Serikali wa uwezeshaji wa shule mbalimbali mwaka huu ni kuhakikisha tunaboresha zile shule za Kitaifa, lakini pia kuongeza nguvu kwenye zile za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo naomba nimpongeze sana ndugu yangu Mheshimiwa Rweikiza kwa juhudi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kwa upekee niwapongeze wananchi wa Mkuranga, nimpongeze Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Mkuu wa Mkoa wa Pwani pamoja na Mbunge wa Mkuranga kwa kuwahamasisha vijana wapatao 53 watengenezaji wa matofali mapya karibu 45,000. Naomba niwasihi Wakuu wote wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, mambo haya ni mambo ya kuigwa tufanye hayo kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shekilindi! Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Jafo nilipenda niongezee kwenye eneo lifuatalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisera kila Kata inakuwa na shule ya sekondari ya kidato cha kwanza mpaka cha nne, lakini kwa kidato cha tano na cha sita, shule hizi zina umaalum wake na ni lazima ziwe na vigezo ambavyo vimeelezwa kwa mujibu wa sheria na si lazima kila eneo kuwa na shule yake ya kidato cha tano na cha sita, Kwa sababu hakuna mtoto aliyefaulu kwenda kidato cha tano ambaye atakosa nafasi kwa shule zetu tulizonazo nchini; kubwa hapa ni ubora wa shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba Mheshimiwa Rweikiza kama wao wana mpango wa kujenga shule ya kidato cha tano na cha sita waje tutawapa vigezo vinavyotakiwa ili tusirudi kwenye makosa yaliyopita ili tuweze kujenga shule zenye sifa zinazostahili kwa ajili ya kidato cha

tano na cha sita, kwa sababu hata tulizoanza nazo nyingine bado zina changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wawakilishi wa maeneo yote kuhakikisha kwamba tunapotaka kuanzisha shule ya kidato cha tano na cha sita basi vigezo vyote vile vya msingi vizingatiwe ikiwepo kwanza uwepo wa umeme, uwepo wa maji maeneo husika, majengo yanayostahili lakini na mazingira yanayoweza ku-*accommodate* masomo ya watoto wa kidato cha tano na cha sita.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa na Wizara ya Maji, swali la Mheshimiwa Mlinga.

Na. 19

### **Mradi wa Maji Lupilo**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA** aliuliza:-

Mradi wa umwagiliaji Lupilo umesimama na haujulikani ni lini utaendelea kujengwa:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mbunge wa Jimbo la Ulanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechagua skimu za kimkakati katika maeneo ya uwekezaji wa kilimo ikiwemo Bonde la Mto Rufiji na Kilombero. Skimu hizo ni pamoja na eneo la Lupilo Ulanga, eneo la Sonjo Kilombero na eneo la Itete Malinyi. Ili kuendeleza skimu hizi Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa skimu za Lupilo na Sonjo pamoja na ujenzi wa skimu ya Itete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza skimu ya umwagiliaji ya Lupilo, Serikali imefanya upembuzi yakinifu wa skimu ya Lupilo yenye eneo la hekta 4000. Kazi zilizofanyika ni pamoja na uchunguzi wa udongo, uchunguzi wa athari za mazingira, upimaji, uchunguzi wa kiuchumi na maendeleo ya jamii, uchunguzi wa rasilimali maji, usanifu wa awali na makisio ya gharama za ujenzi wa skimu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa na gharama za ujenzi wa skimu ya Lupilo Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuendeleza skimu hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba nitoe pole kwa wananchi wangu wa Lupilo wanaopata misukosuko ya kubambikiziwa kesi na Jeshi la Polisi, nalaani vikali matumizi mabaya ya nguvu za Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, mradi huu tangu uanze una miaka mitatu sasa hivi; upembuzi yakinifu sijui nini vinafanyika. Sasa Mheshimiwa Waziri anawaambia nini wananchi wa Lupilo wanaotarajia mradi huu uwe mkombozi wa maisha yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Waziri haoni umuhimu wa kuiunganisha ofisi yake ya kanda na Mkurugenzi wangu wa Ulanga ili iwe rahisi kwa ajili ya ufuatiliaji na utekelezaji wa mradi huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuweka uzito katika masuala ya umwagiliaji kwa sababu huu ndiyo ukombozi wa huko tunakokwenda kuhakikisha Watanzania watakuwa na chakula cha uhakika kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu mradi huu, ni kweli kwa mwaka huu wa fedha tumeamua kwamba katika bajeti iliyokuwa imetengwa ya bilioni 35, bilioni sita ndizo fedha za ndani. Sehemu kubwa ya kazi hii ilikuwa ni kufanya upembuzi yakinifu na kufanya mapitio ya mabwawa mbalimbali ambayo tumelenga katika miaka mitano tufikishe hekta milioni moja. Kwa,hiyo, ni pamoja na bwawa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fedha zinazohitajika kwa bwawa hili peke yake ni bilioni 40, bajeti ya Wizara kwenye umwagiliaji ni bilioni 35. Kwa hiyo, ni fedha nyingi tunahitaji tu-*mobilize* fedha kutoka kwa wafadhili mbalimbali ili tuweze kupata fedha za uhakika. Naomba niwahakikishie wananchi wanaoishi kwenye eneo hili la Lupilo kwamba mradi huu Serikali itakwenda kuutekeleza na katika mwaka wa fedha 2017/2018 tutaweka fedha kuanza kujenga skimu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili, mapendekezo yake kwamba Ofisi ya kanda iweze kuunganishwa, naomba hili nilichukue tutakwenda kuangalia uwezekano wa kufanya hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magige.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa Wilaya ya Longido Mkoa wa Arusha ni mojawapo kati ya Wilaya ambazo zina changamoto kubwa ya maji, wakazi wa eneo hili wamekuwa wakitumia asilimia 90 ya muda wao kwenye kutafuta maji na kuna tuhuma ya kuwa kuna pesa zaidi ya milioni 400 zilitolewa lakini hazijulikani zimeenda wapi na wananchi wa Longido wanaendelea kuteseka. Je, ni lini Serikali sasa itatekeleza ahadi yake ile ya mradi mkubwa wa maji wa bilioni 13 katika Wilaya hii ya Longido? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika bajeti ya mwaka huu tumeweka fedha kwa ajili ya kuanza kujenga mradi huo mkubwa wa kupeleka maji katika Wilaya ya Longido. Naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, Serikali inaendelea na taratibu za manunuzi ili tuweze kupata mkandarasi wa kujenga mradi huu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Moshi Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya kuhudumia miradi ya maendeleo ya maji katika Kijiji cha Igagala na Kijiji cha Majalila ambacho ni Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Tanganyika. Serikali ilipotoa hizo fedha usimamizi wa mradi huu haukwenda sahihi. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza miradi ambayo tayari fedha ilikuwa imetengwa na wafanyakazi ambao ni wasimamizi wamesababisha hasara ya kutokukamilika kwa mradi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, hili suala la maji lina wachangiaji wengi, naomba majibu yawe mafupi na sahihi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya ziara Mkoa wa Katavi na mimi niliungana naye na hii miradi tuliitembelea na yale matatizo tukayakuta, kwamba miradi imeanza, miundombinu imejengwa lakini bado kuna matatizo madogo ya kuweka *pump* ili wananchi waendeleo kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuta pia kweli kulikuwa na tatizo la kimikataba lakini tatizo hilo tayari nimeshaliwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji ili waweze kuwasiliana na Katibu Mkuu wa TAMISEMI kwa sababu Halmashauri ya Mji wa Mpanda ndiyo iliyosaini ule mkataba. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala hili tayari tumeshalichukua tunalifanyia kazi.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningeomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la maji pale Ilula, Wilaya ya Kilolo ni kubwa na Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba anataka kuwatua akinamama ndoo kichwani, ni la muda mrefu. Je, Waziri anaweza akatoa majibu mazuri ambayo yatawafanya wananchi wa Ilula wapate moyo na kuacha sasa kuniita mimi Mwamaji badala ya Mwamoto? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mwamoto kwamba Serikali itapeleka maji ya uhakika kwa wananchi wa Ilula. Serikali bado inaendelea kushughulika kuweza kutafuta fedha za kugharamia mradi huo na tupo kwenye hatua nzuri. Serikali ya Austria imeonesha nia ya kusaidia mradi ule, bado hatujakamilisha tu makubaliano ya fedha ambazo tutaweza kugharamia mradi huo, lakini mazungumzo yanaendelea vizuri. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge hutaendelea kuitwa Mwamoto utaitwa Mwamamaji ili kusudi wananchi wa Ilula waweze kupata maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Tatizo la maji katika Jimbo la Nyangh'wale ni kubwa sana. Kuna mradi ambao unaendelea pale wa kutoa maji Ziwa Victoria kuyapeleka Wilayani Nyangh'wale. Mradi huo umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu na nimejaribu kuongea na wakandarasi wanadai kwamba wamesimama kuendeleza mradi ule kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Kuna mabomba mengi ambayo yameshasambazwa na yapo nje yanapigwa jua kwa zaidi ya miaka mitatu. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwapatia fedha hawa wakandarasi ili waweze kukamilisha mradi huo wa maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwamba Bunge lilipitisha Mfuko wa Maji na Mfuko huu tunashukuru kwamba kila mwezi fedha inatoka na ninyi wenyewe ni mashahidi huko mlipotoka kutokana na Mfuko huu tayari yale madeni yanalipwa na tunaendelea kulipa. Kama madeni hayajalipwa basi ujue kuna matatizo madogo madogo ya kiutendaji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Hussein mimi nalibeba niangalie kwa nini huko hakujalipwa ili tuhakikishe kwamba mradi huo wakandarasi wanalipwa ili waweze kuukamilisha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Machano Othman Said, kwa niaba.

Na. 20

### **Kufungua Ubalozi Mdogo - China**

**MHE. SALUM MWINYI REHANI (K.n.y. MHE. MACHANO OTHMAN SAID)**  
aliuliza:-

Serikali yetu kwa muda imekuwa na uhusiano wa karibu na watu wa China, Serikali ya Watu wa China ina Ubalozi Dar es salaam na Ubalozi Mdogo huko Zanzibar:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa umefika wakati wa kufungua Ubalozi Mdogo wa Tanzania katika Mji wa Guangzhou ili kutoa huduma nzuri kwa Watanzania wengi katika mji huo?

(b) Je, ni utaratibu gani unatumika katika kuwapatia visa Watanzania ambao wameamua kuishi China zaidi ya mwaka mmoja.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Machano Othman Said, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ina mpango wa kufungua Ubalozi Mdogo katika Mji wa Guangzhou uliopo katika Jimbo la Guangdong, China. Hatua hii imefikiwa baada ya Serikali ya China kuchagua majimbo matatu yatakayokuwa na uhusiano maalum na nchi tatu za Afrika ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majimbo haya ni pamoja na Jiangsu, Zhejiang na Guangdong ambayo yamepewa maelekezo mahususi na Serikali ya China kuhamasisha makampuni kutoka kwenye Majimbo yao kuhamisha viwanda vyao katika nchi hizo na kupeleka katika nchi za Afrika, Tanzania ikiwa mojawapo. Tunaamini kwa kuanzia katika mji huo, si tu tutakuwa na fursa ya kuyashawishi makampuni ya mji huo kuja kuwekeza nchini, bali tutaweza kutoa huduma mbalimbali kwa Watanzania wanaofanya biashara katika Mji wa Guangzhou.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo unawataka Watanzania na wageni kutoka Mataifa mengine walioamua kuishi nchini China zaidi ya mwaka mmoja kuwa na kibali cha kuishi. Kibali hiki kinapatikana kwa kuwasilisha maombi kwenye Wizara inayoshughulikia na masuala ya mambo ya ndani ya China na iwapo watakidhi vigezo vinavyotakiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za China watapatiwa kibali cha namna hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehani.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini tulikuwa tunataka kujua mkakati gani Wizara inayo wa kuwafanya Wachina hawa kuhamisha teknolojia na viwanda ambavyo vinazalisha bidhaa mbalimbali kutoka kwao kule kuanzishwa katika nchi yetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, swali fupi, jibu fupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati uliopo katika Wizara yetu na nchi ya China ni kufanya makubaliano na kusaini makubaliano hayo ya kuanzisha mahusiano ya kibiashara na kiuchumi Tanzania na China.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mwijage.

Na. 21

### **Kuyaendeleza Mabonde kwa Ajili ya Kilimo – Kagera**

**MHE. SVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Mkoa wa Kagera una mabonde mengi ambayo yanaweza kuzalisha vyakula pamoja na mboga mboga hususan mabonde ya Kalebe, Kagera na Kyabakoba:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyaendeleza mabonde hayo ili vijana waweze kupata ajira?

(b) Je, ni lini Serikali itawapa mikopo wanawake na vijana ili waweze kujiongezea kipato?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa yenye fursa nyingi za uwekezaji katika sekta ya kilimo. Aidha, Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa yenye vyanzo vingi vya maji ikiwa ni pamoja na Ziwa Burigi na Ziwa Rwelu na Mito ya Kagera na Rusumo inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kwa sasa, Serikali inafanya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya mradi wa mabonde yaliyopo Kagera yanayofaa kwa umwagiliaji chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia ambapo mabonde aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge yapo ndani ya mradi huo. Aidha, zoezi la upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni unatarajiwa kukamilika Aprili 2017 na baada ya hapo Serikali itaendelea kuwasiliana na wafadhili juu ya utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na halmashauri husika inaendelea kuainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo hasa kilimo kinachohusisha vijana na utekelezaji wa mpango na mikakati ya kuhakikisha vijana wengi wanajijiri kupitia sekta ya kilimo. Suala la upatikanaji wa ajira kwa vijana na wanawake linachukuliwa kwa uzito wa hali ya juu hasa ukizingatia vijana kuwa ni takribani asilimia 67 ya nguvukazi ya Taifa kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) pamoja na wadau wengine wa maendeleo tayari inafanya upembuzi yakinifu kwa kutembelea maeneo mbalimbali nchini ili kuainisha shughuli za vijana pamoja na kuhamasisha kujiunga katika vikundi, kuongea na Serikali za Mitaa ili kubaini changamoto ambazo vijana wanakabiliana nazo wakati wa shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara zingine za kissekta pamoja na sekta binafsi tayari imetayarisha mkakati wa kuhusisha vijana katika sekta ya kilimo uitwao *National Strategy for Youth Involvement in Agriculture* wa miaka mitano ambao utasaidia kuweka mzingira bora ya utekelezaji wa mipango kutoka kwa wadau ili kuwanufaisha vijana. Mkakati huu ulizinduliwa mwezi Oktoba, 2016.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage.



**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati wa Bunge la Tisa hili suala nililiuliza ikawa upembuzi yakinifu, sijui upembuzi yakinifu unachukua miaka mingapi kuweza kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama suala langu linavyosema na yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri amekiri, Mkoa wa Kagera sisi hatujawahi kuomba chakula; tunachoiomba Serikali ni kuwapa elimu wana-Kagera waweze kuwa na chakula cha kutosha. Kama hivi sasa tuna matatizo ya njaa, lakini ni mara ya kwanza, tungekuwa na utaalim wa kilimo cha umwagiliaji tusingekuwa na matatizo ya njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ni lini Serikali itaupa kipaumbele Mkoa wa Kagera kwa kila kitu? Kwa kuwa kila kitu tunachokisemea kinakuwa ni kesho, kesho, hata na haya maafa itakuwa ni kesho. Ni lini Serikali itaona huruma kwa kuwapa elimu vijana na wanawake wakawa na chakula cha kutosha pamoja na chakula cha kuleta uchumi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, kwamba upembuzi huwa unaelekea kuchukua muda mwingi kuliko ilivyopangwa, lakini kama nilivyosema tunatarajia sasa utakamilika mwaka unaokuja. Kwa hiyo baada ya hapo hatutakuwa tunazungumzia tena kuhusu kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuhusu Serikali kupeleka wataalam wa kilimo, nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari katika Serikali za Mitaa katika Halmashauri zetu tuna Maafisa Ugani wa Kilimo ambao wanafanya kazi za kutoa elimu kwa ajili ya kilimo na Wizara yangu imeweka mazingira wezeshi ya kisera ya kuhakikisha kwamba wataalam hao wanaotoa elimu wanatoa elimu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mara nyingi vikwazo vimekuwepo kwamba hawana nyenzo, hata hivyo Serikali inaendelea kuboresha shughuli za ugani ili wananchi waweze kunufaika na elimu ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuhusu vijana, Wizara yangu iko tayari muda wowote kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili kuangalia namna gani tunaweza kuwawezesha vijana kushiriki katika kilimo. Tayari katika Bunge hili kuna Mbunge mmoja, ambaye anashirikiana vizuri sana na Wizara yangu, Mheshimiwa Ester Mmasi, ambaye kupitia kwake na jitihada zake kwa vijana, tayari tumewafikia vijana 500 na tayari tumewapatia ardhi katika maeneo mengi; tayari tuko katika jitihada za kuwaunganisha na mabenki kwa ajili ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimkaribishe sana Mheshimiwa Mbunge aje ofisini kwetu, tukae, tuongee tuangalie namna gani tunaweza tukawasaidia vijana wa Kagera ili waweze kuondokana na tatizo la ajira. Vilevile, niseme kwamba, tunawapongeza sana watu wa Mkoa wa Kagera kwa sababu ni kweli kama alivyosema kwa miaka mingi sana wamekuwa wakijitosheleza kwa chakula na hata sasa ambapo changamoto za mabadiliko ya tabia ya nchi yametokea, Serikali yao bado itaendelea kuwa nao ili kuhakikisha kwamba, wanaweza kukabiliana na hizo changamoto ili waendeleo kujitegemea kwa chakula.

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Halima, jandee Mheshimiwa Umbulla.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na swali zuri lililoulizwa juu ya ajira ya kilimo kwa vijana wa Mkoa wangu wa Kagera, Serikali katika bajeti ya mwaka 2016/2017, ilionesha nia na dhamira ya dhati ya kuinua ajira kwa vijana. Je, Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wake katika sera ya ajira ya vijana katika sekta ya kilimo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba katika mpango wetu wa bajeti ya mwaka huu tuna mikakati mingi ya kuwasaidia vijana kupata ajira kwenye sekta ya kilimo. Kama nilivyokwishasema, tayari Wizara inashirikiana na vijana wengi ili kuhakikisha kwamba wanajihusisha katika shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari vijana wengi tumewasaidia kuingia kwenye Vyama vya Ushirika, lakini vilevile tayari vijana tunawaunganisha katika fursa za mikopo. Mfano mzuri, ni fursa iliyopo katika benki ya NMB ambayo tayari wametenga shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kilimo cha biashara na kwa wale vijana ambao wameunganika katika vikundi kama wale niliosema wanaosaidiwa na Mheshimiwa Ester Mmasi tayari tunaongea na NMB ili waweze kutoa mikopo kwa ajili ya vikundi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile NMB wako tayari kutoa elimu ya kilimo kwa ajili ya vijana ambao watapata mkopo. Vilevile, katika kutekeleza kusudio letu la kuhakikisha vijana wanapata ajira kupitia kilimo, tumetenga hekari 220 katika bonde la Rufiji ili liweze kuwa shamba darasa ili vijana wengi waweze kuelewa namna zaidi ya kujihusisha na kilimo. Kwa hiyo, kama ninavyosema kuna mipango hiyo na Mheshimiwa Halima namfahamu ni mtu ambaye anawapigania sana vijana nae vilevile ili...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ameshakuelewa!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Ili aweze kupata maelezo zaidi, namkaribisha...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ameshakuelewa! Mheshimiwa Martha.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Taasisi nyingi za fedha zinawakwepa wakulima na wafugaji kuwapatia fursa za mikopo, lakini nashukuru katika maelezo yake sasa hivi amefafanua hasa kwa wakulima. Sasa je, Serikali ina mikakati gani hasa kuwapa wafugaji mikopo ili waweze kuendeleza mifugo yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kilimo na mikopo iliyopo, pamoja na fursa zingine tunamaanisha vilevile ufugaji pamoja na uvuvi si kilimo cha mazao pekee.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis.

Na. 22

### **Matukio ya Kuvamiwa kwa Askari wetu kwenye Vituo vya Kazi**

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na matukio ya kuvamiwa kwa askari wetu wakiwa katika vituo vyao vya kazi na kujeruhiwa, kunyang'anywa silaha na wakati mwingine hata kuuawa:-

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya usalama wa askari hawa?

(b) Je, mpaka sasa Serikali imeshakamata silaha ngapi zilizoporwa kutoka kwa askari waliovamiwa wakiwa katika majukumu yao?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa usalama wa askari polisi wanapokuwa katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itaendelea kuliwezesha Jeshi la Polisi hapa nchini kwa vitendea kazi bora na kuwajengea uwezo askari wetu kwa mafunzo ili waweze kukabiliana na matukio ya uhalifu yanayohusisha uvamizi wa vituo vya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa kipengele cha pili, Jeshi la Polisi limefanikiwa kukamata silaha 19 kati ya 23 zilizoporwa kutoka kwa askari waliovamiwa wakiwa katika majukumu yao katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Septemba, 2016.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis.

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwamba swali langu limejibiwa vizuri, lakini naona kajibu kwa kifupi sana, hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza; je, ni lini Serikali itaanzisha mfumo wa *CCTV camera* katika maeneo ya vituo vya polisi ili kusaidia kubaini matendo ya uvamizi huo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali inasema nini kuhusu huduma za wanafamilia hususan watoto wa askari hao waliovamiwa na kuuawa; watuambie kwamba watoto wao watawapa huduma gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa *concern* yake ya usalama wa askari pamoja na huduma kwa wanafamilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *CCTV cameras* tunaliangalia kwa ukubwa wake ambapo tunalenga kuangalia majiji kwa ajili ya usalama wa majiji, vituo vya polisi lakini pia katika maeneo ambayo askari wetu wanalinda yakiwemo mabenki pamoja na maeneo mengine ambako huduma hizo zinahitajika. Kwa hiyo jambo hilo tumelipokea na tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma kwa wanafamilia, kwa sasa upo utaratibu ambao fidia huwa inatolewa, lakini tunaongea na wenzetu wa bima tuweze kuangalia upande wa bima ya afya, lakini na upande wa bima ya maisha ambao utalenga utaratibu mzima wa familia zinazoachwa na askari ambao wanapata dharura za aina hiyo. Pia kwa kuwa sasa hivi Wizara ya Mambo ya Ndani inaangalia upya *Police Force Act* ambayo itakuja Bungeni, ambayo inafanyiwa kazi tunategemea tutapata michango mingi ya Wabunge

kupitia Kamati, lakini pia na wote ambao watahusika katika kutengeneza Act hiyo mpya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niseme kwamba, natambua kazi nzuri inayofanywa na baadhi ya askari polisi, lakini kuna baadhi ya askari polisi ambao katika utekelezaji wa majukumu...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema, natambua kazi nzuri ambayo inafanywa na baadhi ya askari polisi, lakini kuna baadhi ya askari polisi ambao katika utekelezaji wa majukumu yao wanatumia nguvu kupita kiasi, wanatoa adhabu za kutweza wakati wa kukamata watuhumiwa, kuwasababishia vilema na wengine kuwasababishia maumivu ambayo ni ya muda mrefu.

Sasa Waziri atuambie ni hatua gani ambazo zinachukuliwa ili kuhakikisha kwamba baadhi ya askari hawa wanachukuliwa hatua au kuondolewa kwenye jeshi ili kuondoa chuki ambazo zinaweza zikajengwa na baadhi ya raia kwa jeshi zima la polisi kutokana na vitendo ambavyo vinafanywa na baadhi ya askari polisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Selasini kwa kutambua kazi nzuri inayofanywa na askari polisi. Nimezunguka nchi nzima nimewaelezea maaskari polisi kuchukua hatua kufuatana na makosa na kufuatana na rika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano vijana walio chini ya miaka 18 wanapokuwa na makosa madogomadogo waangalie namna ya kuyashughulikia, lakini pia na watu wanapokuwa na makosa ya aina hiyo na ni vijana wadogo wasiwekwe sana mahabusu yaliyo na watu waliokithiri kwenye vitendo vya uovu, mfano, kumweka kijana wa miaka 12 ambaye labda alikuwa yuko kwenye magwangala akakaa sehemu moja na watu ambao wameshazoea kwenye uuaji ni kumwandaa kisaikolijia baadaye kuwa mhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya nguvu; jambo hili lina dhana tofauti. Nimewaambia maaskari wanapopambana na wahalifu watumie nguvu zote kuhakikisha kwamba tunadhibiti uhalifu. Kwa mfano, watu wamekuja wamevamia na wana silaha, wakavamia kituo; ama watu wamevamia eneo kama maeneo ambayo tumeyaona, nimewaelekeza maaskari watumie nguvu

zote walizonazo kuhakikisha kwamba tunadhibiti uhalifu. Kwa hiyo, kwenye hilo la uhalifu, kwa wale wanaokuja kihalifu kwa kweli jeshi la polisi tutatumia nguvu zote kwa sababu hatutaruhusu wahalifu waweze kutamalaki katika eneo la nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faida.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa wavamizi ama majambazi hao, baadhi yao inasemekana wanatoka nje ya nchi yetu ambao wanaingia kwa njia za panya ama njia nyingine zote na hawa wanakuja kufanya uhalifu na hata kuwaua askari wetu. Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kulinda mipaka yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa hoja aliyotoa. Tunatambua kweli katika matukio ya uhalifu ambayo yamejitokeza tumebaini wahalifu wakiwa wanatoka nje ya nchi, kwa mfano, silaha zile tulizokamata pale Mbezi na watuhumiwa kati ya wale watu sita baadhi yao walikuwa sio Watanzania. Pia kati ya silaha zilizokamatwa Tabora, Mkoa wa Kigoma kwenye operesheni mbalimbali tulipoziangalia hazikuwa na usajili wa hapa ndani, ni silaha za kutoka nje ya nchi, kwa hiyo tumeendelea kuimarisha operesheni za aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunatoa rai kwa wananchi pale wanapotambua kwamba, katika nyumba ya jirani ama katika mtaa wao kuna watu wasiofahamika ama watu wasiotambulika au watu wasioeleweka kama ni Watanzania na kazi zao hazieleweki watoe taarifa katika vituo vya jirani ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaimarisha taratibu zote za mipakani, lakini wengi wanaoingia hawaingii katika njia rasmi, wanatumia njia za panya. Kwa hiyo, ni muhimu sana kila Mtanzania aweze kutambua kwamba ana wajibu wa usalama wake pamoja na mali zake kwa ujumla wake.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Hawa Subira.

Na. 23

### **Tatizo la Msongamano wa Mahabusu Tabora**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Mkoa wa Tabora unakabiliwa na tatizo kubwa la msongamano wa mahabusu kiasi cha kutishia afya zao kwa sababu magereza hayo yana uwezo wa kuchukua takribani mahabusu 1200, lakini mpaka sasa kuna zaidi ya mahabusu 2500 kinyume kabisa na haki za mahabusu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa hali ya magereza katika Mkoa wa Tabora zinaboreshwa na idadi hiyo ya mahabusu inazingatia haki za msingi za binadamu?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kesi zilizopo mahakamani zinaharakishwa kwa kuwa wapo mahabusu wengi ambao wana kesi za kubambikiwa au kughushiwa tu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba hali ya magereza katika Mkoa wa Tabora pamoja na mikoa mingine nchini zinaboreshwa ili kuzingatia haki za binadamu, Serikali inaendelea kufanya upanuzi wa magereza kwenye magereza ya zamani na kujenga magereza mapya ya mahabusu katika kila Wilaya ambapo mpango huu ni endelevu na utekelezaji wake umekuwa ukifanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni tatu katika bajeti ya fungu la maendeleo kwa ajili ya ukarabati na upanuzi na umaliziaji wa ujenzi wa mabweni mapya na majengo ya utawala katika baadhi ya magereza nchini likiwemo Gereza la Nzega na Gereza la Mahabusu Urambo. Kati ya fedha hizo, milioni 150 ni kwa ajili ya kuanza upanuzi wa gereza la Nzega kwa kujenga mabweni mawili ya wafungwa yenye uwezo wa kuchukua wafungwa 50 kila moja na milioni 35 ni kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa bweni moja la wafungwa ambalo linatarajiwa kujengwa liwe gereza la mahabusu huko Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa kuna msongamano wa mahabusu katika gereza la Tabora kama ilivyo katika magereza mengine hapa nchini. Kwa kutambua hilo, Serikali kupitia Jukwaa la Haki Jinai imekuwa kifanya

vikao vya kuharakisha kesi ambazo bado upelelezi wake ulikuwa haujakamilika ili kupunguza msongamano magerezani. Aidha, mafunzo yamekuwa yakitolewa kwa askari wapelelezi ili ukamataji wa watuhumiwa uzingatie uzito wa ushaidi wa mhusika kuepusha malalamiko ya kubambikiwa kesi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali madogo ya nyongeza. Nashukuru Serikali inatambua kwamba kuna msongamano hasa katika gereza la Manispaa ya Tabora. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kupanua mahabusu ya Kwa Zuberi ili kuweza kupunguza msongamano wa mahabusu walioko katika gereza la Tabora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuwasaidia mahabusu ambao wamepelekwa magereza bila kuwa na hatia na kusababisha msongamano usiokuwa na sababu eti kwa sababu upelelezi haujakamilika; wanaendelea kuwekwa tu katika mahabusu hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuleta jambo hili na bahati nzuri na mimi nilishazungukia Mkoa wa Tabora. Tunachokifanya tunakubaliana naye kwamba kuna msongamano katika gereza la Tabora na mapendekezo yake ya kufanya upanuzi katika gereza la Kwa Zuberi ni jambo la msingi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tunapokea maoni yote haya, lakini tunachofanya tunaweka vipaumbele katika kuongeza ukubwa wa magereza katika maeneo ambayo magereza yale yana kazi za kufanya ili wafungwa wanapokuwepo waweze kuwa na kazi za kufanya ili waweze kulisaidia Taifa katika kurekebishwa kwao kuliko kuwa na wafungwa wengi, tunatumia kodi za walipa kodi kuwatunza, halafu wakawa hawana kazi za kufanya na wala hawana namna ambayo wanarekebishwa. Kwa hiyo tumepokea na tutaweka vipaumbele kulingana na jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuwasaidia mahabusu ambao wamerundikana na wapate msaada wa kisheria. Serikali tumekuwa tukifanya hivyo na katika kipindi cha tangu Julai, binafsi nimezunguka, Waziri wa Katiba na Sheria amezunguka na katika vipindi tofauti aliambatana na Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na zoezi hilo limekuwa



endelevu na kuna wakati maafisa wenyewe wa ngazi ya juu kutoka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wamekuwa wakipita katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kutoa huduma hiyo na kushughulikia kesi zile ambazo si za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nilipopita Rukwa nilikuta kwenye gereza moja kulikuwepo na vijana kama 11 hivi, nilipowahoji kwamba kwa nini wapo pale, waliniambia makosa yao. Kumi walikuwa wana makosa ya kunywa supu. Walikunywa supu wakashindwa kulipa, walishakaa karibu mwezi hivi na mmoja alikuwa amekunywa soda ya kopo. Sasa nikawambia muda waliokaa umeshazidi gharama ya soda ile ya kopo na ile supu. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumewaelezea na wenzetu kule waweze kuchukua hatua za kurekebisha kulingana na makosa watu waliyofanya na wale ambao wanastahili kurekebishwa na kuondoka, wasirundikwe mle, wapate dhamana waweze kuondoka na kuendelea kufanyiwa hatua zingine.

**MWENYEKITI:** Amekuelewa Mheshimiwa! Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tatizo lililopo la msongamano wa mahabusu kwenye Gereza la Tabora linafanana kabisa na tatizo lililopo kwenye Gereza la Keko lililopo Jimbo la Temeke katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Mbaya zaidi ni kwamba, miundombinu ya majitaka ndani ya gereza imekufa na hivyo sasa vinyesi kutoka gerezani vinatiririka mpaka mtaani na kuhatarisha afya za mahabusu na wakazi wa maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maelezo Mheshimiwa Waziri amesema bilioni tatu iliyotengwa kwa ajili ya kukarabati magereza haijalitaja Gereza hili la Keko. Sasa nataka kujua, Mheshimiwa Waziri anawaambia nini wakazi wa maeneo ya Keko wanaolizunguka gereza lakini na mahabusu waliopo ndani ya Gereza la Keko, waendeleo kukaa katika mazingira hayo mpaka lini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshapokea concern ya Mheshimiwa Mbunge na kwa kuwa katika ratiba ya ziara zangu natarajia kuzungukia na magereza yaliyopo Mkoa wa Dar es Salaam, nitafika na Gereza la Keko na baada ya hapo kama Wizara tutakaa kuangalia hali hiyo na namna ya kulifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Safi sana, *short and clear*. Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kutokana na msongamano huo wa magereza na mahabusu ambao hata Mheshimiwa Waziri ameukiri hapa, kunasababisha magonjwa mengi hasa ya mlipuko; nimewahi kutembelea Gereza la Uyui pale Tabora, kulikuwa na wagonjwa wengi wa upele; na sasa hivi kuna tatizo kubwa sana la upatikanaji wa madawa sijui Serikali ina mkakati gani wa kufanya upendeleo kuhakikisha wale mahabusu na wale ambao ni wafungwa wanapata dawa za kutosha?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge Mwakasaka amefuatilia mara nyingi sana jambo hili na hata kuna kipindi tumekaa, yeye pamoja na wenzangu wa Wizara ya Afya. Jambo lake tulishalipokea, kadri mtiririko wa fedha unavyokuja tutalifanyia kazi kwa sababu ni jambo ambalo alishalifuatilia hata kwa ngazi ya Wizara na tulimuahidi kwamba tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, naomba uendelee kuvuta subira na niwapongeze wana Tabora kwa kukuamini kwa sababu kwa kweli umeendelea kulifuatilia hilo pamoja na mambo ya uhalifu ambao mara nyingi mmekuwa mkusemea na sisi tunachukua hatua.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Heche, jiandae Mheshimiwa Munde.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ningependa kuuliza swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri tulikuwa naye Tarime na alifika kwenye Gereza la Tarime. Gereza hili linatumika kama gereza linalotumiwa na wilaya mbili, Wilaya ya Rorya na Wilaya ya Tarime na bahati mbaya hata makazi ya askari Waziri mwenyewe aliona. Gereza limejengwa mwaka 1941 likiwa na uwezo wa kubeba watu 245. Sasa hivi gereza lina wafungwa 600 na mahabusu, watu hawana hata pa kulala, Serikali inasema nini kuhusu kurekebisha hali ile ili isije ikaleta matatizo makubwa pale? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishafika kwenye gereza analisema Mheshimiwa Mbunge, nimejionea hali yake na kumbukumbu zangu zinanionesha kesho nina swali la Gereza la Tarime na nitalifafanua kwa urefu zaidi. Hata hivyo, niseme nimeshapokea jambo hilo na kesho nitalifafanua na sisi kama Wizara tunayafanyia kazi mambo haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyaleta.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa sababu suala hili limekuwa ni kero ya muda mrefu toka naingia Bungeni humu 2010, watu wanaongelea kuhusu kujazwa kwa magereza na Serikali imekuwa ikitujibu kwamba itafanya upanuzi na itapeleka pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kutuletea sheria humu Bungeni ili tubadilishe makosa madogomadogo yalipiwe faini polisi; kama yale aliyosema Mheshimiwa Waziri, mtu kanywa soda anawekwa ndani mwezi mmoja, dada amekutwa barabarani akaambiwa anajiuza anawekwa ndani miezi mitatu, mtu amegombana kisimani na mwenzake anawekwa ndani miezi mitatu. Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza kuleta sheria sasa tukabadilisha humu Bungeni makosa mengine yakalipiwa faini polisi kama yalivyo ya trafiki? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Munde kwa hoja aliyotoa na kwa jinsi alivyoleta mapendekezo kwa umakini. Sisi kama Wizara tumepokea na tutaliangalia kwa ujumla wake hili alilolisema na kabla ya hapa, njiani alinishauri tulifanyie kazi na suala la *parole* kwa kupanua wigo kwa wanaonufaika na *parole*, wale ambao wamesharekebika waweze kufanya kazi wakiwa nje. Kwa hiyo, tumelipokea na tutakapokuwa tuna fursa ya mabadiliko ya sheria tutazingatia mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge ili kuweza kupunguza msongamano kwa njia hiyo na kuendelea kuwarekebisha watu kwa kadri sheria inavyosema.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Haonga.

Na. 24

### **Kurejesha Mashamba Yasiyoendelezwa kwa Wananchi**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA** aliuliza:-

Katika Kijiji cha Isenzanya Wilayani Mbozi, shamba lenye ukubwa wa hekari 1,000 linalohodhiwa na Mzungu aitwaye Joseph Meya halijaendelezwa kwa miaka mingi sasa huku wananchi wa kijiji hicho wakiwa hawana maeneo ya kilimo:-

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kulirejesha shamba hilo kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA  
(K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mbunge wa Jimbo la Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwana Joseph Meier na Bi. Enala Mgala kwa pamoja wanamiliki shamba lenye ukubwa wa hekta 330.16 ambayo ni sawa na ekari 825.4 kwa Hati Na. 257 MBY LR lililopo katika Kijiji cha Isenzanya, Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wamiliki hawa wameendeleza kipande kidogo cha shamba hili kwa kupanda kahawa na mazao ya msimu kama mahindi na maharage. Hata hivyo, kutokana na mahitaji ya ardhi kuongezeka, wananchi wa Kijiji cha Isenzanya kwa nyakati tofauti kupitia kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi wamekuwa wakiiomba Serikali kuwapatia ardhi hiyo ili waitumie kwa kilimo. Katika kutekeleza azma hiyo, November 2015 Mkurugenzi wa Halmashauri alifanya mkutano uliojumuisha wamiliki na wanakijiji wa Kijiji cha Isenzanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mkutano ukaguzi wa shamba kufanyika mpaka sasa mazungumzo na wamiliki wa shamba yanaendelea. Aidha, Sheria ya Ardhi, Namba 4 ya Mwaka 1999 imeeleza wazi namna ya utoaji wa maeneo pale ambapo mmiliki anakiuka masharti yake. Halmashauri kupitia Afisa Ardhi Mteule inayo mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa sheria husika. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali ikiendelea na utaratibu wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ambayo sijaridhika nayo hata kidogo, naomba sasa niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa mmiliki wa shamba hili ndugu Joseph Meier alimiliki shamba hili kwa njia za ulaghai ikiwa ni pamoja na kuwapatia viatu Wenyeviti wa Vijiji wa kipindi hicho kwa tiketi ya CCM na akamilikishwa shamba hilo, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuchukua hatua za kinidhamu kwa mmiliki huyu ambaye ni mmiliki haramu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Serikali katika majibu yake imesema kwamba mmiliki wa hili shamba analihudumia kwa kiwango kidogo sana, kwa maana ya kwamba katika ekari 1,000 ekari zinazoendelezwa ni kama ekari 10 tu kati ya 1000; je, Serikali haioni kwa kigezo hiki tu ni muda muafaka sasa wa kumpora huyu bwana hili shamba lirejeshwe kwa wananchi wa Jimbo la Mbozi ambao hawana maeneo ya kulima? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza la nyongeza anasema kuwa huyu mwekezaji alichukua shamba hili kwa njia ya ulaghai. Sisi tunasema kwamba kama mwekezaji yeyote na ndiyo maana Msajili wa Mashirika ya Umma (TR) anapitia mikataba yote ya wawekezaji wetu ambavyo wameweza kumilikishwa mashamba na wengine ambao waliingia kwenye ubia wa mikataba mbalimbali ili kuweza kujua kama kuna tatizo lolote lile katika umiliki. Kwa hiyo, pale tunapogundua kwamba mwekezaji au mbia wetu ambaye tumeingia naye kama Serikali, kuna ubadhirifu wa aina yoyote ulifanyika, hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaguzi hizo zinaendelea kwenye Mashirika yetu ya Umma yote kuhakikisha kwamba kuna usahihi wa umiliki, lakini vilevile hakuna ulaghai wa aina yoyote na hivyo kama itabainika kwamba kuna ulaghai ulitumika katika kujipatia shamba hili hatua zaidi za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; kwamba huyu mwekezaji amekuwa akiendeleza shamba hili kwa kiwango kidogo sana, ambapo *according to* yeye Mheshimiwa Mbunge ni kama asilimia moja au mbili ya shamba alilokuwa amekabidhiwa la hekta 830, lakini ameweza kuendeleza kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapa kwamba kinachotakiwa sasa Mheshimiwa Mbunge ajue jukumu hili liko kwenye halmashauri yake, yupo Afisa Mteule wa Ardhi pale ambaye ana jukumu la kufanya ukaguzi kwenye shamba hilo kuona maendelezo ambayo yamefanyika na akigundua kwamba hakuna maendelezo yoyote yaliyofanyika kwenye shamba hilo, basi amwandikie *notice* ya siku 28 ya kufanya marekebisho na baadaye amwandikie *notice* ya siku siku 90 ya kujieleza kwa nini asinyang'anywe ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo kama yote haya yatafanyika, mwekezaji huyu atakuwa ameshindwa kukidhi matakwa yanayotakiwa, basi atashauriwa Waziri wa Ardhi ili aweze kulitwaa shamba hilo na Waziri wa Ardhi atamshauri Mheshimiwa Rais afute hati husika. Baada ya hapo taratibu zikikamilika, basi hati itafutwa, umiliki utafutwa na umiliki wa shamba hili utarejeshwa kwenye halmashauri ambapo halmashauri ndiyo watapanga matumizi ya namna gani shamba hili litumike baada ya kuwa limerudishwa na Serikali mikononi mwa halmashauri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Magige, jiandae Mheshimiwa Qambalo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua moja ya changamoto kubwa inayoikabili nchi yetu ni migogoro ya ardhi na eneo ambalo inasemekana kumekuwa na migogoro ya ardhi ni pamoja na eneo la Kibada Kigamboni ambapo kuna viwanja vilipimwa na Serikali na wananchi wakapewa na Wizara husika. Sasa, nataka kujua nini *status* ya eneo hilo wakati Wizara imepima, imewapa wananchi lakini leo imetokea kwamba eneo ambalo amepewa mtu mmoja tayari amejitokeza mtu mwingine amesema hilo eneo ni la kwake wakati Wizara ndio wametoa hati; nini *status* ya eneo hilo? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakumbuka sote hapa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi akiwa hapa Bungeni alitamka kwamba migogoro yote ya ardhi ambayo Waheshimiwa Wabunge mliwasilisha humu Bungeni na migogoro mingine ambayo inahusisha taarifa mbalimbali ambazo zimeshafanyiwa uchunguzi, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi aliunda Tume ya kupitia taarifa hizi za uchunguzi zilizofanyika, lakini na migogoro ambayo Waheshimiwa Wabunge tayari waliwasilisha kipindi cha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwaambia kwamba, timu hiyo ya wataalam iko kazini na Mheshimiwa Bulaya avumilie, asubiri, taarifa hiyo ya wataalam itakapokamilika tutawaleta hapa Bungeni ili kila mmoja ajue *status* ya kila eneo la migogoro ambavyo limeshughulikiwa na Serikali. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Qambalo.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Matatizo ya ardhi ambayo haijapata kuendelezwa yaliyopo katika eneo la Mbozi yanafanana kabisa na matatizo ambayo tunayo kwenye Wilaya yetu ya Karatu. Katika Kijiji cha Mang'ola Juu kuna mwekezaji, Tembotembo ambaye amemilikishwa eka zaidi ya 3,000 lakini ameweza kuendeleza chini ya asilimia 25. Katika kijiji hicho pia kuna mwekezaji anaitwa *Acacia* naye ameweza eneo alilopewa kwa chini ya asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba hayo sasa yamebadilika kuwa hifadhi na mapori bubu ya kuhifadhi wanyama wa porini ambao ni hatarishi kwa wananchi wanaolizunguka. Je, ni lini Serikali itatoa mashamba hayo na kuwarudishia wananchi hao ili waweze kuyatumia? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya kutwaa mashamba kwa hekta zisizopungua 500 mmiliki wa shamba hilo anapewa miaka miwili tu anatakiwa awe ameliendeleza shamba hilo na asipofanya hivyo yuko halali kabisa kunyang'anywa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Namba 4 ya Mwaka 1999, kifungu cha 45 na cha 47, anayo haki ya kunyang'anywa ardhi ile. Wale ambao ardhi yao wamekabidhiwa zaidi ya hekta 500, kama hajaiendeleza kwa asilimia 80 ndani ya miaka mitano ardhi ile inaweza kutwaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri kwa Mheshimiwa Mbunge wa Karatu, kwa sababu mamlaka haya, nani anayeanzisha kazi hii, kazi hii inaanzishwa na Afisa Mteule wa Ardhi pale halmashauri, waanzishe tu halafu watuletee, tena wafanye mapema na mimi bado nakaimu huu Uwaziri wa Ardhi ili tuweze kuyashughulikia mapema matatizo haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Tatizo la ardhi kwenye Wilaya ya Mbozi linafanana sana na tatizo lililopo kwenye Mji wetu wa Tunduma. Katika Mji wa Tunduma katika Kata ya Mpemba kuna ardhi karibu ekari 500 ambazo zinamilikiwa na Shirika la Nyumba la Taifa na mpaka sasa hivi eneo lile halijaendelezwa zaidi ya miaka minane. Je, Serikali inasema nini ili kuikabidhi halmashauri, ambayo haina hata eneo la kujenga makao makuu ili iweze kutumia ardhi ile?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na swali hili ambalo limekuwa kila Mheshimiwa Mbunge akiliulizia, naomba tu nitoe wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na Maafisa wetu Wateule wa Ardhi popote nchini, katika maeneo na katika malalamiko ya namna hii, Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999 imewapa nguvu. Kwa hiyo, walianzishe jambo hili watuletee na sisi kama Serikali hatutawaangusha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Lijualikali.

Na. 25

**Ahadi za Ujenzi wa Barabara za Kidatu – Ifakara - Mlimba**

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI** aliuliza:-

Tangu awamu zilizopita hadi Serikali ya Awamu ya Tano, wananchi wa Kilombero wamekuwa wanapewa ahadi za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kidatu hadi Ifakara na kutoka Ifakara hadi Mlimba:-

(a) Je, Serikali haitambui mchango wa Wilaya ya Kilombero katika nchi wa kulisha Taifa?

(b) Kitendo cha Serikali ya awamu hii kuahidi ujenzi wa viwanda wakati eneo muhimu kwa uchumi wa nchi kama Kilombero likiachwa bila barabara inayosafirisha wakulima na mazao; je, maana yake ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Lijualikali, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mchango wa Wilaya ya Kilombero katika uzalishaji wa mazao ya chakula kwa wingi kwa ajili ya matumizi yao na Taifa kwa ujumla hivyo kulifanya eneo hilo kuwa miongoni mwa maeneo ya ghala la Taifa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano, pamoja na kuahidi ujenzi wa viwanda imeweka pia katika kuimarisha miundombinu ya barabara kuelekea kwenye maeneo yenye umuhimu wa kiuchumi kama Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza azma hiyo, Serikali katika eneo la Kilombero, pamoja na ujenzi wa Daraja la Kilombero unaoendelea, imekamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami kilometa 16.17 katika Barabara ya Kidatu hadi Ifakara kati ya Kiberege na Ziginali na Kibaoni hadi Ifakara. Aidha, katika barabara ya Ifakara hadi Mlimba zimejengwa kwa kiwango cha lami kilometa 24 kati ya Mlimba hadi Kihansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutimiza ahadi ya Serikali ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mikumi – Kidatu – Ifakara, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mikumi – Kidatu – Ifakara (kilometa 103.3) umekamilika. Usanifu huo



umejumuisha upanuzi na ukarabati wa barabara ya lami iliyopo na madaraja sehemu ya Mikumi hadi Kidatu kilometa 35.2 na Kidatu hadi Ifakara kilometa 74.4. Ujenzi wa kiwango cha lami wa sehemu ya Kidatu hadi Ifakara pamoja na madaraja umepangwa kuanza katika robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 chini ya ufadhili wa Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Serikali ya Marekani kupitia USAID na Serikali ya Uingereza kupitia DFID.

Usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara kutoka Ifakara hadi Kihansi (kilometa 126) ili kuunganisha na kipande cha barabara ya lami (kilometa 24) kilichojoengwa awali kati ya Ifakara na Mlimba unaendelea na umepangwa kukamilika mwishoni mwa Oktoba, 2016.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu haya mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kwa namna ambavyo wafadhili wetu wameonesha nia ya kuweza kusaidia, lakini kwenye majibu ya Waziri ameonesha mradi utaanza kwenye robo ya tatu, lakini sijaona mradi unakamilika lini? Kimsingi, kwa Kilombero hii imekuwa ni kero. Tumechoka kuzika ndugu zetu, tumechoka kuharibu magari yetu, mazao yanakuwa na bei kubwa kwa sababu ya usafirishaji; kwa kweli imekuwa ni kero kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri sasa aniambie kwamba huu mradi unaisha lini ili hii kero iweze kwisha nasi tujione ni sehemu ya Tanzania? Kwa sababu imefika hatua sasa ukiwa unakwenda Ifakara unasema sasa naingia Tanganyika, maana kule ni vumbi! Hii imekuwa ni kero, kwa hiyo, naomba atuambie sasa huu mradi unakamilika lini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine tunaomba atusaidie kwa sababu pale Ifakara na hii Wizara kwa sababu ni ya Uchukuzi na Mawasiliano, pale kuna daraja la Mto Lumemo, kutokana na mafuriko linakwenda katika muda wowote. Kwa hiyo, atuambie kama wako tayari kwenda kuangalia lile daraja na athari za mafuriko waweze kusaidia ili haya mafuriko yatoweke na daraja lipone. Nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, anataka *commitment* tu basi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wananchi wa Ifakara, Mlimba na maeneo yote mpaka kule Mahenge ambapo daraja la Kilombero linawahusu; kazi ambayo Serikali imeifanya ni kubwa na kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi, ujenzi utaanza kipindi cha robo ya tatu. Utakwisha lini? Nadhani kwa sasa ni mapema mno kwa sababu kuna baadhi ya makubaliano katika hawa wafadhili

yanatarajia kukamilika hivi karibuni. Tutakapokamilisha na mazungumzo yakikamilika na Mkandarasi tutaweza kuwa na majibu sahihi. Kwa sasa naomba Mheshimiwa Mbunge akubali na wananchi waelewe kwamba Serikali imeji-*commit* kujenga hiyo barabara na itakapofika robo ya tatu ya mwaka huu wa fedha kazi hiyo itaanza na baada ya hapo, tutajua kadri tutakavyoendelea, lini kazi hiyo itakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili, nikubaliane naye na bahati nzuri nina ratiba ya kwenda huko, nitamjulisha siku ambayo nitakuwa huko ili nitakapokuwa huko akanionyeshe hilo daraja tuangalie nini kinaweza kufanyika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Oliver na Mheshimiwa Mwambe ajiandae.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Tatizo la barabara ya Kidatu na Ifakara linafanana na barabara ya *junction* ya kuelekea Rusumo almaarufu kama zero-zero kupitia barabara ya Nyakahula - Rusahunga mpaka Nyakanazi. Hiyo barabara imekuwa ikifanyiwa ukarabati mara kwa mara lakini bado inaharibika kwa muda mfupi sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya matengenezo makubwa katika barabara hiyo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo anayoongelea hivi sasa tunavyoongea ina mkandarasi anayefanya matengenezo. Ni kweli hoja anayoongelea kwamba, kunakuwa na matengenezo ya mara kwa mara na hii inatokana na matumizi makubwa sana ya malori makubwa yanayopita katika barabara hiyo na naamini matengenezo ya sasa yamezingatia ukubwa wa matumizi ya barabara hiyo na hivyo matengenezo yake sasa yatakuwa ya muda mrefu tofauti na huko nyuma.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambe na Mheshimiwa Ntimizi, jiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi. Nataka kufahamu kwa uhakika ni lini Serikali itasema waziwazi siku ambayo kazi ya ujenzi wa barabara ya Masasi, Nachingwea utaanza? Kwa sababu upembuzi yakinifu ulifanyika pale muda mrefu, wananchi wanakosa amani katika eneo lile kwa sababu nyumba zao nyingi zilichorwa 'X' na hawajui lini zitavunjwa au waendeleo na ujenzi katika eneo lile. Tuliona tija ya Serikali

imetoa nguvu kubwa sana na sasa hivi wanakaribia kuanza ujenzi wa barabara inayokwenda Ruangwa kuanzia Nanganga. Tunataka tuone pia na upande wa Masasi Nachingwea na wenyewe ujenzi unaanza mara moja.

Kwa hiyo, tunaomba *commitment* ya Serikali watueleze, ni lini ujenzi wa hii barabara utaanza au kama siyo hivyo, basi wananchi wale waambiwe waendeleo kuendeleza yale makazi yao kwa sababu wanaishi katika maisha duni, hawajui ni lini nyumba zao zitavunjwa kwa sababu ya uendelezaji wa barabara katika eneo hilo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, muda wetu unakwenda sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mwambe awaelimishe wananchi waliopo katika barabara hiyo kwamba wasijenge, kwa sababu Serikali ina dhamira ya dhafi ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba katika mwaka huu wa fedha kuna fedha zimetengwa kwa ajili hiyo. Suala la lini, naogopa sana kusema kwa sababu kuna *process* ya kufikia hiyo hatua. Naomba tukamilishe hiyo *process*, itakapokamilika tutamjulisha lini tunaanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ntimizi.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Tatizo la barabara hii ya Kilombero linafanana na tatizo la barabara yetu ya Tabora - Itigi. Kipande cha Chaya - Nyahua kilomita 89 ambacho kinaifanya barabara hii mpaka sasa isiweze kupitika na tunaelekea katika kipindi cha mvua.

Barabara hii ni muhimu sana kwa sisi wakazi wa Tabora, Katavi na Kigoma. Tunaomba Serikali ituambie ni lini barabara hii itatengenezwa ili kufungua barabara hii na kusaidia wakazi wa mikoa hiyo? Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Musa Ntimizi anafahamu kwamba mwezi wa Kumi na Moja ndiyo tutakuwa na kikao na *Kuwait Fund* kuhusu hii barabara. Labda kwa maana ya taarifa kwa wananchi wa kule nao wajue ni kwamba tunatarajia kupata fedha kutoka *Kuwait Fund* kwa ajili ya kukamilisha hiki kipande

ambacho kimebakia kati ya Chaya na Nyahua; na kikao cha kupata hiyo *commitment* kitafanyika mwezi ujao mwezi Novemba. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Bwanausi.

Na. 26

### **Daraja la Mto Miesi**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Serikali kupitia Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ililihakikishia Bunge kuwa madaraja ya Mto Mresi katika barabara ya Ulinzi na Shaurimoyo na Nachalolo katika Mto Mwitwi yalizolewa na mafuriko na yatajengwa kwa dharura:-

(a) Je, ni maandalizi gani yamefanyika ili madaraja hayo yajengwe kwa haraka?

(b) Je, madaraja hayo yataanza kujengwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Ulinzi ya kutoka Mangamba – Madimba – Tangazo – Kitaya – Mnongodi – Mapili hadi Mitema Upinde inaunganisha Wilaya za Mtwara Vijijini, Newala na Nanyumbu. Sehemu ya barabara hii, yaani Mangamba – Madimba – Tangazo – Kitaya - Mnongodi hadi Namikupa yenye urefu wa kilomita 108 inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

Mheshimiwa Mwenyekiti, TANROADS imekamilisha usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha changarawe wa sehemu ya barabara hii yenye urefu wa kilomita 120 unaojumuisha madaraja ya Mbangara, Miesi na Kigwe yaliyopo katika barabara hii ya Ulinzi. Serikali kwa sasa inatafuta fedha ili kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, madaraja ya Shaurimoyo na Nakalola yaliyopo katika barabara za Mpindimbi hadi Shaurimoyo na Mpindimbi hadi Nakalola zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ambapo fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja hayo bado zinatafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, Serikali itaendelea kuifanyia barabara hii matengenezo ya kawaida, matengenezo ya muda maalum na matengenezo ya sehemu korofi. Aidha, kuhusu sehemu ya barabara ya Ulinzi iliyobaki kuanzia Mapili hadi Mitema Upinde yenye urefu wa kilomita 250, Serikali imetenga shilingi milioni 140 kwa ajili ya kuifungua.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bwanausi.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Swali langu la kwanza; Mheshimiwa Waziri atakiri kwamba wananchi wa Kata ya Mkundi, Kata ya Mpindimbi na Kata ya Singano wanapata tatizo kubwa sana kutokana na kutokuwepo kwa madaraja haya. Aliyekuwa Waziri wa Ujenzi katika Serikali ya Awamu ya Nne na Rais wa Jamhuri ya Muungano, aliahidi kwamba atasaidia jambo hili ili madaraja yale yajengwe. Je, nini kauli yake leo; kwa sababu hata usanifu katika madaraja hayo haujafanyika? Nini maelekezo yake kwa Watendaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa barabara ya Ulinzi ambayo inaunganisha kati ya Tanzania na Msumbiji ni barabara muhimu sana ya kiuchumi kwa wananchi katika maeneo yetu: Je, ni hatua gani zimeshafikia sasa katika maandalizi ya ujenzi wa barabara hiyo katika awamu hii ambayo ameisema kwamba shilingi milioni 140 zimeshapatikana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ahadi hii ya kuifungua hii barabara na pamoja na kuwawezesha wananchi wa Kata hizi za Mkundi, Mpindimbi na Singano zimetolewa na viongozi wetu. Naomba kumhakikishia kwamba haya niliyoyasema katika jibu langu la msingi ndiyo hatua madhubuti za kufikia utekelezaji wa ahadi hizi za viongozi walizozitoa katika nyakati mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa maeneo hayo ambao wanaathirika, kwamba Serikali ina nia ya dhati ya kuhakikisha madaraja yale yanarudishwa, lakini vilevile barabara ile ya Ulinzi inafunguliwa. Nini tunakifanya katika hiyo Shilingi milioni 140?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utangazaji wa tenda kwa ajili ya kazi hii utafanyika hivi karibuni na vilevile kazi hii ya upembuzi yakinifu nayo itafanywa na Mtendaji wa TANROADS Mkoa wa Mtwara. Labda kwa taarifa hii naye nimkumbushe kama alikuwa amejisahau kwamba kazi ya kuhakikisha hayo madaraja yanafanyiwa usanifu ili yaweze kukamilika kama viongozi wetu walivyoahidi, ifanywe haraka ili kazi ile itekelezwe kama viongozi walivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hali ya barabara za Lulindi ni nafuu kuliko Mbulu Vijijini; na kuna barabara imeahidiwa ya Karatu - Mbulu; Mbulu – Hydrom; Hydrom – Sibiti na Mheshimiwa Rais, kwa kujengwa kwa lami; na majibu ya Mheshimiwa Waziri yalikuwa yanasema mwanzoni uchambuzi yakinifu umeshaanza. Je, barabara hii inajengwa lini sasa ili wananchi wa Mbulu na maeneo mengine wapate nafuu ya kiuchumi na kupita hasa kuelekea kwenye Hospitali ya Hydrom?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano inapoahidi ina dhamira ya dhati ya kutekeleza ahadi zake zote ikiwa ni pamoja na barabara hii. Tumeongea mara nyingi ofisini kuhusu hili suala na tumemwambia mara nyingi kwamba tuna dhamira ya dhati, tunatafuta fedha. Hatuwezi kuanza ujenzi kabla hatujapata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za kutafuta fedha zinaendelea kwa kasi na mara zitakapokamilika tutamjulisha Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa maeneo ya Mbulu mpaka wanavyoangana na Hanang wajue kwamba lini barabara yao sasa itakuwa vizuri na sasa wataenda kwenye ile hospitali wakiwa na barabara nzuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, muda wetu umekwisha. Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel. Kwa niaba yake, namwita Mheshimiwa Kangoye.

Na. 27

### **Ujenzi wa Daraja la Kilombero**

**MHE. MARIA N. KANGOYE (K.n.y. MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA)**  
aliuliza:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuanza ujenzi wa daraja la Kilombero na utakamilika lini na kuanza kutumika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa daraja la Kilombero ulianza tarehe 21 Januari, 2013, nao unaendelea vizuri. Ujenzi wa daraja hili haukuweza kukamilika kwa wakati uliopangwa ambao ni Septemba, 2016 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo mvua nyingi za masika zilizosababisha Mto Kilombero kufurika na kupunguza kasi ya utekelezaji wa ujenzi. Kwa sasa ujenzi wa daraja hili umefikia asilimia 75 na ujenzi unatarajiwa kukamilika mwishoni wa mwezi Desemba, 2016 na daraja kuanza kutumika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangoye.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na kazi nzuri ya Serikali, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini barabara ya kutoka Kilombero - Kivukoni mpaka Mwaya - Ulanga itakamilika kwa ujenzi wa kiwango cha lami? (*Makofi*)

Swali la pili; je, ni lini ujenzi wa barabara ya kutoka Bigwa mpaka Kisasi itakamilika kwa ujenzi wa kiwango cha lami pamoja na madaraja yake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu. Mheshimiwa Waziri, muda wetu umekwisha, tunaomba majibu mafupi lakini yawe ya uhakika.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba barabara hizi ni muhimu na zinahitaji kujengwa kwa kiwango cha lami kama ambavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi imefafanua. Katika barabara zote mbili; moja, hii ya upande huu wa Ulanga Kusini na hii ya upande wa kwa Mheshimiwa Mbena, niwahakikishie kwamba dhamira ya Serikali ni ya dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumekuwa tukiwaeleza katika vipindi vilivyopita, dhamira yetu ya kujenga barabara hizi iko pale pale na tutahakikisha tunatafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo na kazi hiyo ya kutafuta fedha ya kujenga barabara hizi inaendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi, Mheshimiwa Ngombale.

Na. 28

### **Fidia kwa Waathirika wa Vita vya Majimaji**

**MHE. HAMIDU H. BOBALI (K.n.y. MHE. VEDASTO E. NGOMBALE)** aliuliza:-

Tanzania ni moja ya nchi duniani zilizoathirika kutokana na Tawala za Kikoloni na Vita vya Majimaji ni moja ya vielelezo vya athari hizo ambapo vita hivyo vilianza Wilayani Kilwa katika Kijiji cha Nandete mwaka 1905 - 1907:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha waathirika wa Vita vya Majimaji wanapata fidia kutoka kwa utawala wa kikoloni wa Kijerumani?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, harakati za kupambana kivita dhidi ya ukoloni zilifanywa na Makabila mbalimbali hapa nchini ikiwemo Vita vya Majimaji na nyingine nyingi. Vita hivi vilifanywa na Watemi wa baadhi ya makabila wakiwemo; Mtemi Mirambo wa Tabora, Mtemi Mkwawa wa Iringa na Chifu Abushiri Bin Salim wa Uzigua, Tanga. Aidha, madhila ya ukoloni kwa wananchi ni mengi yakiwa ni pamoja na utumwa, ubaguzi wa rangi, ukandamizwaji na kuuawa kwa tamaduni zetu za asili. Pia, uporwaji wa mali zetu na ardhi bora za kilimo pamoja na mazuiyo ya kuendeleza vipaji vya teknolojia kama vile uundaji wa silaha. Haya ni baadhi tu ya madhila ya ukoloni. Makusudi ya vita vya watawala wetu wa jadi ilikuwa kupinga ukoloni na kutaka kujitawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa harakati hizo za kivita za viongozi wa kijadi kwa pamoja zililenga kuwakomboa wananchi kutoka kwenye makucha ya ukoloni na kuleta uhuru kwa wananchi, siyo vyema kutoa madai ya fidia kwa jukumu hili la kizalendo lililotekelezwa na makabila mengi nchini mwetu. Badala yake madhila na athari ya Vita vya Majimaji yabaki kama sehemu muhimu ya kumbukumbu za ukombozi wa nchi yetu. *(Makofi)*



**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize swali moja la nyongeza Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vita dhidi ya ukoloni ilikuwa imegawanyika katika maeneo mawili; kulikuwa na vita ambayo ilipiganwa na viongozi wetu wa jadi kabla ya kuingia kwa ukoloni ambapo walikuwa wana-*resist* ukoloni usiingie, lakini kulikuwa na Vita ya Maji Maji ambayo ni vita pekee iliyopiganwa wakati tayari Wakoloni wanatawala Tanganyika na sehemu ya nchi yetu. Kwa hiyo, Vita ya Majimaji ni tofauti na hivyo vingine alivyovitaja Mheshimiwa Waziri kwenye majibu yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ukienda kwenye Hospitali ya Wilaya pale Kilwa, kuna orodha ndefu ya wazee wetu waliopoteza maisha tena kwa kunyongwa kutokana na Vita hivi vya Majimaji. Kwa hiyo, nataka kujua orodha ile ya wazee ambayo imewekwa pale kwenye Hospitali ya Kilwa, inatunufaishaje sisi wakazi wa Kilwa na Lindi kwa kujua tu kwamba hawa walinyongwa kwenye vita dhidi ya Ukoloni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa vita vingine vyote, kumbukumbu huwa zinawekwa na siyo ya Majimaji tu, ukienda katika nchi yoyote iliyopigana vita, utakuta kuna makaburi ya mashujaa na kuna majina yao kama kumbukumbu za kivita. Hoja yangu katika jibu langu la msingi ni kwamba hatupaswi kama Wazalendo kuomba fidia kwa kuitetea nchi yetu. Hii siyo kwa Maji Maji tu, hata kwa Vita vya Kagera watu walipigana; watu wamepoteza maisha; tumeweka makaburi ya mashujaa kwa wale waliokwenda kukomboa Afrika nje ya nchi. Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba tutawakumbuka kama mashujaa na tutaendelea kuwaenzi na kuweka kumbukumbu ya kivita, lakini siyo rahisi kuwalipa fidia kwa sababu walikuwa wanajitolea kwa ajili ya nchi yao; na hii imefanywa na wengi ikiwemo Vita vya Kagera. Hakuna aliyelipwa fidia, bali tunawaenzi kwa kazi nzuri waliyoifanya kuilinda nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba niulize swali la nyongeza. Mwaka 2013 nilitembelea Kumbukumbu ya Vita ya Majimaji, iko Songea na ni vizuri sana kwamba angalau tumeweka kumbukumbu ya mashujaa waliopigana Majimaji; isipokuwa katika Kumbukumbu ya Mashujaa wa Majimaji kuna watu mle ambao wamepewa heshima kwenye kumbukumbu ambao hawakuwa wamezaliwa wakati Majimaji

inapiganwa. Chumba kikubwa kabisa kwenye Kumbukumbu ya Maji Maji kinamhusu Laurence Mtazama Gama ambaye hakupigana Majimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumejenga Kumbukumbu ya Majimaji ili kumkumbuka Laurence Gama au kukumbuka waliokufa kwa sababu ya Majimaji? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya kumbukumbu za mashujaa ni kuwakumbuka wale walioshiriki katika vita husika. Kwa hiyo, hii taarifa ya kwamba kuna mtu ambaye amewekwa kama kumbukumbu wakati hakushiriki, pengine imetokana na kwamba kumbukumbu hiyo inajumusiha zaidi ya mashujaa wa Majimaji. Inawezekana kuna mashujaa wengine ambao wanajumuishwa. Kwa hiyo, naomba nipate fursa hii tuliangalie vizuri suala hili ili tuweze kulitolea jibu la uhakika zaidi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda sana, saa tano kasobo sasa. Tunakwenda Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua.

Na. 29

### **Ruzuku kwa Wachimbaji Wadogo wa Madini**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa kutambua umuhimu wa wachimbaji wadogo wadogo imekuwa ikitoa ruzuku ili kuwawezesha wachimbaji kunufaika na madini yapatikanayo maeneo mbalimbali nchini:-

(a) Je, mpango huo umenufaisha wachimbaji wangapi nchini?

(b) Je, ni Mikoa na Wilaya zipi zinazonufaika na mpango huo?

(c) Je, Serikali ipo tayari kuweka utaratibu wa kuwakopesha wachimbaji wadogo wadogo ili kuwawezesha kuchimba madini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mpango wa utoaji wa ruzuku uanze Serikalini mwaka 2013/2014, jumla ya Wachimbaji Wadogo wa madini 118 wamenufaika na mpango huu. Hadi mwaka 2015/2016 jumla ya shilingi bilioni 8.1 zimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku hutolewa kwa Wachimbaji wadogo wa madini kwa njia ya ushindani na kwa kuzingatia vigezo husika kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Wanufaika 118 wa ruzuku walitoka katika mikoa yote 22 na katika wilaya 53 yenye shughuli za madini hapa nchini. Wanufaika sita walitoka katika Mkoa wa Tanga na katika Wilaya za Handeni pamoja na Tanga yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013/2014 Serikali ilianzisha Mfuko wa kusaidia Wachimbaji Wadogo na kutenga jumla ya shilingi bilioni 2.3 ambazo zilitengwa na kuwekwa katika Benki ya Rasilimali Nchini (TIB) kwa ajili ya mikopo hiyo. Wachimbaji wadogo wengi walishindwa kukidhi vigezo vya mikopo na hapo sasa Serikali iliamua kutoa ruzuku. Kazi inayoendelea sasa ni kuwapa elimu ya namna sasa ya kunufaika na Mifuko hiyo ili kusudi wananchi waweze kupata fedha hizo kwa kupitia mabanki na taasisi za kifedha hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na nia na dhamira nzuri ya Serikali juu ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo lakini imeonekana kwamba masharti haya hayawasaidii hawa wachimbaji wadogo na tunajua kwamba sasa hivi wimbi kubwa la watu wanaokosa kazi ni vijana. Sasa, je, Serikali iko tayari kupunguza vigezo vile ili watu wengi waweze kunufaika na mpango huu?

Swali langu la pili, je, Naibu Waziri yupo tayari kuambatana nami kwenda Jimboni ili tuweze kuzungumza na wachimbaji wadogo ili wajue dhamira ya Serikali ya kuwasaidia hususan wachimbaji wadogo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Kigua kwa kutambua kwamba kulikuwa na vikwazo

tulipoanza utaratibu huu. Tumepunguza vikwazo vya kuomba mikopo. Tulipoanza kutoa ruzuku mwaka 2013 ilikuwa siyo ruzuku, ilikuwa ni mikopo. Sasa Serikali imepunguza masharti ya mikopo na badala yake sasa inatoa ruzuku. Hilo ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikwazo cha pili kilikuwa ni lazima wachimbaji wawe na *Bankable statement* inayoonyesha rasilimali ya madini iliyoko hapo chini. Sasa kulingana na uwezo mdogo wa wachimbaji wadogo, kigezo hicho kimeondolewa. Kwa hiyo, tunashukuru Mheshimiwa na vigezo vinaendelea kupungua ili Watanzania wengi wanufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kutembelea kwenye Jimbo la Kilindi na hasa maeneo ya Tunguli. Ningependa nifike Tunguli lakini hata Kwa Manga mpaka kule kwenye Kijiji cha Kikunde na Mafulila ambako wanachimba wachimbaji wengi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Jesca David Kishoa.

Na. 30

### **Mradi wa Umeme wa Upepo-Singida**

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwa na habari za uamuzi wa Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kujenga kituo cha kuzalisha umeme wa upepo Mkoa wa Singida:-

Je, ni lini mradi huo utatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na TANESCO imekuwa ikifanya tafiti kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa kutumia upepo katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo na maeneo ya Mkoa wa Singida. Kufuatia tafiti hizo, maeneo ya Kititimo pamoja na Kisaki Mkoani Singida yameonekana kuwa na chanzo kizuri cha kuzalisha umeme kwa njia ya upepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni binafsi ikiwemo Kampuni ya *Wind East Africa* pamoja na Makampuni mengine kama *Six Telecoms* na mengine yameonesha uwezo huo kutoka *UK*. Uwezo wa nguvu inaopata ni pamoja na kuzalisha umeme wa *Megawatt* 100 katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano kati ya Serikali kupitia *TANESCO* na Kampuni ya *Wind East Africa* sasa yanaendelea vizuri na yatakamilika mwezi Desemba mwaka huu, lakini ujenzi wa mradi sasa utanza mwezi Aprili mwaka ujao, 2016 na utakamilika mwaka 2019. Ujenzi wa mradi huu utagharimu Dola za Marekani milioni 264.77

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni nyingine inayoonesha kuwekeza katika mradi huo ni pamoja na Kampuni ya *Geowind* ambayo pia itazalisha *Megawatt* 50 na mradi utagharimu Dola za Kimarekani milioni 136 na utakamilika...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, naomba utulivu ndani ya Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** ... katika mwaka ujao wa fedha.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa mujibu wa jarida la *The Citizen* la tarehe 23, Oktoba mwaka huu, 2016, imeonyesha kwamba miongoni mwa mikopo iliyokopwa kutoka China mwaka 2015 ni pamoja na Dola za Kimarekani milioni 132 ambazo ni sawa na Shilingi bilioni 300 za Kitanzania kwa ajili ya mradi wa umeme wa upepo Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iwaeleze wananchi wa Singida fedha hizi zimekwenda wapi? Kwa sababu mpaka hivi sasa hakuna kinachoendelea, hakuna hata nguzo moja halafu tunaambiwa bado majadiliano yanaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa sababu mazingira kama haya ambapo mikopo inaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini fedha zinaelekezwa maeneo yasiyohusika. Ni lini Serikali itaona kuna umuhimu wa kumwagiza CAG akague mikopo inayoagizwa katika nchi hii? Kwa sababu katika deni la Taifa, inawezekana kuna ujanja ujanja unafanyika kwenye suala zima la mikopo. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mradi wa upepo wa Singida ambao unazalisha *Megawatt* 100 hautokani na fedha za mkopo, ni wawekezaji binafsi, niweke wazi. Kadhalika, kuhusiana na masharti ya mikopo, ni Makampuni yenyewe yanakopa na kuja kuwekeza kwa ajili ya kufanya biashara na TANESCO inanunua umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la CAG, ni taratibu za Kiserikali. CAG ana utaratibu wa kukagua na Mashirika na ofisi za Serikali zina utaratibu wa kuwasilisha taarifa za kukaguliwa. Tutaendelea kupeleka taarifa kwa mujibu wa CAG ili hesabu zote zikaguliwe. Kwa hiyo, hakuna suala la kuficha kwenye ukaguzi; CAG ana ratiba ya kukagua na Serikali tuna wajibu wa kupeleka takwimu ili zikaguliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kupeleka takwimu zikaguliwe.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa muda wetu sasa ni saa tano kasoro dakika 10. Tumetumia muda mwingi sana kwenye maswali. Kwa wale ambao walikuwa na maswali ya ziada naomba radhi hatukuweza kuyachukua.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, sasa nina matangazo. Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa mnatakiwa kujaza *form* za tamko la Viongozi wa Umma kuhusu rasilimali na madeni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995 na Na. 5 ya mwaka 2001 Kifungu cha (9) na cha (11). *Form* hizo zinapatikana Mapokezi iliyopo katika ukumbi wa Bunge. Hivyo, Mbunge yeyote ambaye bado hajachukua *form* hizo apite hapo na kuchukua kwa ku-sign kwenye *register* maalum iliyoandaliwa na kisha kuziwasilisha katika Ofisi ya Mheshimiwa Spika tarehe 20 Desemba, 2016 kabla ya kuziwasilisha kwa Kamishna wa Maadili tarehe 31 Desemba, 2016.

Tangazo la Misa; Wakristo wote na Wanajumuiya ya Mtakatifu Thomas More mnaalikwa katika Misa ya Kuwakumbuka na Kuwaombea Marehemu wote leo saa 7.30 baada ya kuahirisha Bunge katika Kanisa dogo jengo la Msekwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali anawatangazia Wajumbe wake wote kuwa leo tarehe 2, mara baada ya kuahirishwa kikao cha asubuhi hii, kutakuwa na kikao kwenye Ukumbi wa Msekwa (c) kuanzia saa 7.15.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji anaomba Wajumbe wake wote wahudhurie kikao leo saa 7.00 mchana chumba namba 227.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWGP) anawatangazia kwamba leo tarehe 2, kutakuwa na kikao saa 7.00 mchana ukumbi mkubwa wa Msekwa.

Mheshimiwa Steven Ngonyani anaomba kuwatangaza Madaktari Bingwa wa asili ya tiba mbadala kutoka Dar es Salaam; Dkt. Maneno Tamba, Dkt. Abdallah Mandal, Dkt. Mama Nuru, Dkt. John Lupimo, Dkt. Joseph Buberwa, Dkt. Mukurata, Dkt. Fadhil Emel na hawa ni wageni wa Mganga mwingine Maji Marefu. *(Kicheko/Makofi)*

Kocha wa timu ya kuvuta Kamba Mheshimiwa Leonidas Gama, anaomba Wachezaji wote wa mchezo huu kufanya mazoezi kuanzia saa 12.00 ili muwahi kupata namba kwa sababu wachezaji ni wengi na kuna hatari ya kukosa namba kama hamfanyi mazoezi. *(Makofi)*

Orodha ya Wageni imeletwa sasa hivi. Wageni walipo Bungeni asubuhi hii: wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 10 wa Mheshimiwa John Kadutu, Mbunge ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Ulyanhulu Mkoani Tabora wakiongozwa na Ndugu Ahmed Kombo. *(Makofi)*

Wageni wanane wa Mheshimiwa Steven Ngonyani na wataalam wa kutumia madawa ya asili; hawa nimeshawatangaza.

Wageni watano wa Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla ambao ni viongozi wa Kata wa CCM kutoka Wilaya ya Makete, wakiongozwa na Mheshimiwa Gerefasi Mwata, Mwenyekiti wa Kijiji cha Ikowo na Ndugu Jenesi Mbilinyi, Katibu wa CCM Kijiji cha Mfumbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ally Keissy, anaomba Wabunge wote wanaotoka Ziwa Tanganyika akiwemo Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Mwilima, Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Mipata na Mheshimiwa Kandege mkutane *Canteen* saa 7.00 mchana huu.

Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge sasa hivi tunaingia katika mijadala kwenye Kamati ya mipango.

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango.

## KAMATI YA MIPANGO

### **Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali Pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2017/2018**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Kamati yetu ya Mipango na orodha ya majina ipo tayari. Namwita Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Masoud Salim ajiandae.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia, ingawa umeniwahi sana, lakini nitajitahidi tu kuweza kuchangia yale ambayo naweza nikachangia kutokana na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ya Mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo naomba nilizungumzie ni suala zima ambalo ndiyo imekuwa kama nguvu kubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano katika mwaka huu mmoja na ndani ya bajeti hii ya kubana matumizi. Ni hatua nzuri kubana matumizi kwa sababu inasaidia kupata rasilimali fedha za kutosha kuzielekeza kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana hapa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi ametupa takwimu za watumishi hewa ambao wameondolewa kwenye payroll ya Serikali na hivyo kupelekea Serikali kuokoa shilingi bilioni 19 kila mwezi kutokana na suala zima la watumishi hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi kutoka kwa Waziri wa Fedha. Taarifa ya gharama za watumishi tunazipata kupitia taarifa ambayo kila mwezi Benki Kuu inaitangaza; inaiweka kwenye tovuti yake na kuigawa pia (*Monthly Economic Review*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Monthly Economic Review* ya mwezi Agosti mwaka 2015 inaonesha kwamba wages and salaries ambazo Serikali ililipa mwezi Juni, 2015 zilikuwa ni shilingi bilioni 456. *Monthly economic review* ya mwezi Agosti mwaka 2016 inaonesha kwamba wages and salaries ambazo Serikali imelipa kwa mwezi Juni mwaka 2016 ni shilingi bilioni 534; kwamba kuna nyongeza ya gharama za mishahara ya kila mwezi ya shilingi bilioni 78. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Utumishi jana ametuambia wanaokoa shilingi bilioni 19 kila mwezi kwa kuondoa watumishi hewa. Taarifa ya Benki Kuu inaonesha kwamba toka Serikali hii imeingia madarakani gharama za watumishi kwa mwezi zimeongezeka kwa shilingi bilioni 78. (*Makofi*)



Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi hewa wameondolewa, ajira mpya hakuna, nyongeza ya mishahara imesimamishwa, lakini gharama za wages *and salaries* zimeongezeka kwa bilioni 78. Haiieleweki! Kuna mmojawapo kati ya hawa wawili anadanganya umma. Ama zoezi la watumishi hewa ni *publicity stunt* au Serikali inatumia fedha kwa matumizi mengine halafu BOT inasema ni mishahara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nipate maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusiana na jambo hilo, kwa sababu ni jambo ambalo umma ni lazima uelezwe na liweze kueleweka tunapopanga mpango kuelekea katika mwaka ujao wa fedha ambao unakuja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni *Higher Education*. Jana nimepitia Mpango wa mwaka jana 2015. Mwaka jana tulichelewa kidogo tukaupitisha mwezi Januari. Serikali inazungumzia kuongeza idadi ya vijana, wanafunzi wanaopata mikopo kwenye elimu ya juu. Mpango pia wa mwaka huu unazungumzia hilo hilo na imeongeza; inasema, kuimarisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili kuongeza uwezo wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi wanaokidhi vigezo, kuendelea kupanua matumizi ya TEHAMA na ukarabati, upanuzi na ujenzi wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapozungumza, idadi ya wanafunzi ambao wana uwezo wa kuingia kwenye Vyuo Vikuu hapa nchini na wanao-*qualify* kwa mikopo ni takriban 65,000. Watoto waliopata mikopo ni 20,000 tu. Nini ambacho kinaandikwa na nini ambacho kinatendwa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hapa napata tatizo kidogo la *coordination* ndani ya Serikali. Waziri wa Elimu alikuja kwenye Kamati. Kamati ya Huduma ya Maendeleo ya Jamii ili-*dedicate* siku nzima na kujadili tatizo la mikopo. Wizara kwa maana ya Serikali kwa kupitia Wizara ya Elimu na Kamati tukakubaliana, kuna mambo yanayopaswa kwenda kuangaliwa upya kuhusu suala zima la *financing higher education* ili tuweze kutatua tatizo hili la mikopo la muda mrefu. Hata hivyo, ukisoma Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo hukuti jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelekezo ya Kamati kwa Waziri ni kwamba *by* mwezi Februari tutakuwa tuna utaratibu mpya. Wakati huo huo, wiki ijayo tuna mabadiliko ya sheria tunakuja kuyafanya ya mikopo ya elimu ya juu. Katika *Miscellaneous Amendment* kuna vipengele ambavyo tunaenda kuvibadilisha kwenye mikopo ambavyo vinabana upanuzi wa kupata mikopo zaidi. Sasa nashindwa kuelewa, kuna mazungumzo ndani ya Serikali kabla ya Serikali kuja ndani ya Bunge kuwasilisha Mpango kama huu? Baraza la Mawaziri linakaa ili kuhakikisha kwamba kila Waziri anaeleza *new development* ambayo

imetokea kwenye sekta yake ili jambo linalokuja Bungeni liwe ni lile ambalo limekubalika ndani ya Serikali? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya jambo tulilozungumza ni kwamba, ukisoma Mapendekezo ya Mpango kuna kipaumbele kimewekwa kwenye masomo maalum; gesi, gesi asilia, sijui nishati, uhandisi na kadhalika. Kwenye vigezo vya mikopo vya mwaka huu vimetolewa ni kwa wanaosomea Udaktari, Uhandisi, Gesi Asilia na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni nchi gani duniani ambayo haina *scholarship programs* kwa watoto wake? Kama ninyi mnataka kujenga nchi ya viwanda, mnahitaji Wahandisi kadhaa; mnahitaji wahandisi wa mitambo kadhaa; mnahitaji wataalam wa mafuta na gesi kadhaa; si ni wajibu wa Serikali kutoa *scholarship* kwa watu hao ili mweze kuwapata hao wataalam? Halafu ili eneo la mikopo, bajeti ambayo mmeitenga kwa ajili ya mikopo ibakie kwa ajili ya watu wengine wote waweze kupata mikopo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwaulize Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mnaweza mkasomesha Wahandisi wengi sana; mnaweza mkasomesha Madaktari wengi sana; hivi niambieni, kuna kiwanda hakina Afisa Utumishi? Kuna kiwanda hakina Mhasibu? Kuna kiwanda hakina Wachumi? Mnawezaje mkasema kwamba mwaka huu tutasomesha hizi *hard sciences* tu? *The best way to do that*, mnatoa *scholarship* kwa hizo *priorities*, hao wengine wanaendelea kupata mikopo kama kawaida. Hayo ndiyo mambo tuliyokubaliana kama Kamati na Wizara ya Elimu. Siyaoni kwenye Mpango; sasa hili ni tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, jana Mheshimiwa Bashe amezungumzia Kurasini na Kariakoo. Tunafahamu kabisa kwamba suala la Kurasini limeongelewa muda mrefu; lakini wakati tunaongea suala la Kurasini hatukuwa na nguvu hii tunayoongea kuhusu viwanda. Niliwahi kusoma makala moja aliandika Mheshimiwa Dkt. Mpango wakati yuko Tume ya Mipango, ilichapishwa na jarida la REPOA kuhusiana na suala la *staying the course*, kwamba mmepanga kitu hakikisheni mnakifanya na *sequencing*. Alitoa mambo kama manane na moja nitalizungumza mwisho kabisa ambalo ni la kumsuta kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kurasini inaenda kuwa ni ya biashara. Kama mnataka kujenga viwanda, kwa nini mnaruhusu uchuuzi huo kama lengo ni la viwanda? Kama kuna *transition* ambayo nakubali, lazima kuwe na *transition*; kwa nini tusiitumie Kariakoo kama hiyo *transition*? Kwa nini tuwae Waswahili, wafanyabiashara ambao wameanza kukua na kukuza mitaji yao kwenda kuimarisha viwanda vya China na wafanyabishara wa China kuleta bidhaa zao Kariakoo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiifanye Kariakoo kuwa ni *free trade area*; chochote kinachoingia Kariakoo kisitozwe kodi na kinachotoka kitozwe kodi? Kwa sababu Kariakoo Wazimbabwe, Zambia, Malawi, Congo wananunua pale, kila sehemu wananunua pale. Hili jambo naomba liangaliwe upya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sasa hivi, kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya Bajeti, mwekezaji yule wa Kurasini ameshaondoka, hayupo tena. Kwa maana hiyo basi, tutumie hii *opportunity* tuweze kuona namna ya ku-link; na kuna matatizo makubwa pale Kariakoo. Maana yake sasa hivi TBS wameongeza viwango vya tozo na faini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wadogo wa Kariakoo wanahangaika sana, lakini tunapoenda kwenye *transition* ya kuelekea viwanda, hawa ndio watu ambao wanapata *entrepreneurial skills through* biashara zao baadaye waweze kuja kuwa na viwanda. Lazima tuone namna gani ambavyo tutawasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, katika lile jarida moja ya jambo ambalo Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango wakati ule akiwa Katibu Mkuu wa Mipango, alisema lazima uongozi ujenge chini ya ushindi, kama atakuwa anakumbuka mwenyewe; *a winning coalition* ambapo kila mtu anaongea jambo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi. Serikali na Bunge hatupo pamoja katika utekelezaji wa mikakati ya nchi. Ama sisi Wabunge hatuielewi Serikali au Serikali haiwaelewi Wabunge; ni *either of the two*. Pia Serikali yenyewe miongoni mwa Mawaziri wenyewe, bado hawaelewani. Ndiyo maana kumekuwa na matamko ya kila mtu kwa kila kinachotokea utafikiri Serikali inakimbizana kupata *front pages* za magazeti. Nadhani kuna haja ya kuwa na *cooling of period*, tuweze kukaa *soberly* kabisa, Waheshimiwa Wabunge na Serikali tujiulize, wapi tunaenda sawa na wapi hatuendi sawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wanalalamika na wananchi wanalalamika kwamba hali ni mbaya. Mimi naelewa na *any development economist* anaelewa kwamba mnapopiga hatua fulani ya maendeleo lazima kuwe na maumivu. Ndiyo maana kuna dawa za maumivu; lazima kuwe na *palliative measures*, yale maumivu mpaka mfikie ile hatua ambayo mnyotaka kufika, hatuendi hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *through* Mpango tupate nafasi tukae kama viongozi, tuweze kuona nchi inakwenda vipi. Pale ambapo kuna matatizo tukubaliane, matatizo haya ni ya lazima lakini tutayaepuka namna hii. Sivyo hivi ambavyo tunakwenda; tutanyoosheana vidole, tutarushiana madongo na

hatutakwenda. Hali ya wananchi sasa hivi malalamiko ni makubwa sana. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Anafuata Mheshimiwa Masoud halafu Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Kishimba wajandae.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nami nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima na afya njema. Nami nichangie kidogo juu ya mapendekezo ya Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka huu ambapo umetolewa na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba bado napata ukakasi na wasiwasi na sijamwelewa Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mpango. Jambo ambalo alilizungumza kwenye Hotuba ya kwanza ya Mpango miezi saba iliyopita sasa hivi halimo wakati jambo hilo halijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ya viwanda kuelekea uchumi wa kati, sijamwelewa Mheshimiwa Dkt. Mpango wakati Mpango uliopita; miezi saba, nane iliyopita alitueleza vizuri juu ya suala zima la viwanda vilivyobinafsishwa, akatuambia kwamba Serikali ina mpango mzuri wa kuweza kutathmini viwanda vyote vilivyobinafsishwa. Hilo la kwanza.

La pili, akasema kwamba wanaandaa mpango mkakati mzuri wa kupitia mikataba yote na kuchukua hatua. La tatu, kufufua viwanda vyote vilivyobinafsishwa. Hakuna moja ambalo limefanywa. Mpango uko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata wasiwasi mkubwa kwa sababu kwa nini kwenye Mapendekezo ya Mpango wa sasa jambo hili asiliweke? Itakuwa kuna jambo ambalo limejificha. Sasa basi, naomba aeleze Watanzania ni viwanda vingapi katika vile ambavyo vilibinafsishwa vimefanyiwa tathmini? La pili, mikataba mingapi wameipitia na hatua gani wamechukua? Tatu, viwanda vingapi ambavyo vilivyobinafsishwa vimeendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata wasiwasi sana kwa sababu tumepiga kelele mara nyingi, Viwanda vya Korosho vilivyobinafsishwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ambavyo viwanda hivyo leo vimekuwa ni maghala, ni tatizo kubwa. Wananchi wanalalamika kwamba viwanda hivyo wamechukua vigogo wa Serikali; mmepeana kwa bei chee; mikataba haikuwa vizuri. Kwa nini muda wote ukiwauliza Wabunge wanaotoka Mikoa ya Lindi na Mtwara viwanda vile ambavyo mpaka sasa havifanyi kazi: Je, mikataba hiyo imepitiwa? Hakuna kitu! Kumbeni siri iliyopo, viwanda vile wamepeana vigogo wa Serikali. Sasa

mnaogopa kutumbuana. Mkitumbua, tumbueni wadogo na wakubwa. Msiwe na figisufigisu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, atuambie Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwa nini hamjafanya tathmini na baadaye mkapitia mkataba wa Kiwanda cha *Newala One*, Viwanda vya Korosho vya *Newala*, Lindi Mjini, kuna Masasi, Likombe, TANITA, Nachingwea na Mtama. Viwanda vyote ni vya korosho hivi. Leo korosho ghafi imefika kilo ni shilingi 3,700 au shilingi 3,800. Kumbe wananchi hao wa Lindi na Mtwara na mikoa yote ambayo inazalisha korosho, kama jambo hili lingefanyika; lakini Mheshimiwa Waziri ameshindwa kabisa, jambo ambalo amezungumza miezi saba iliyopita, sasa hivi hakuna kitu. Ni shida kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wajibu wetu ni kuishauri Serikali, lakini Serikali inayokubali ushauri. Kama Serikali haikubali ushauri, shauri yake mwenyewe. Hilo lilikuwa la kwanza. Ikumbukwe kwamba viwanda hivi sisi kujengwa kwake tulikuwepo kutoka Italy na Japan kwenye miaka ya 80 mamilioni ya dola na sijui kama mpaka leo kama sisi hatuna deni. Hebu atuambie Mheshimiwa Waziri, tatizo nini zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, lile ambalo linazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, kupungua kwa mizigo kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Hakuna asiyejua na Wabunge wengi wamesema kwamba Bandari ya Dar es Salaam imekimbiwa na wenzetu wa Zambia, DRC Congo wanasuasua, Burundi nao wamekimbia, Rwanda nako ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa sababu inaonekana hatuna mipango madhubuti wenzetu wa Msumbiji na wale wa Kenya baada ya mzigo wao kufika, wanapewa siku 90 bure wanahangaika na mambo mengine. Sisi baada ya siku saba unaambiwa taratibu za malipo zianze. Nenda Bandari yetu ya Dar es Salaam! Ukienda Kenya unaambiwa siku 90; ukienda Beira siku 90, ndiyo maana baadhi ya wafanyabiashara wetu wanatukimbia. Kwenye Mpango huu iko wapi? Hili hamlijui jamani? Nye ni wasomi wakubwa. Nafikiri ni vyema mwandae mazingira mazuri ambapo watu waweze kuja hapa na hizi shughuli za kodi ziangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu wanakimbia hawa Rwanda, Burundi na Zambia. Sasa hivi kuna malalamiko ya umoja wa majahazi. Majahazi nao ni aibu nyingine, wanakimbia. Mzigo mmoja wa jahazi unaotoka Dar es Salaam kwenda sehemu nyingine; mzigo wa shilingi milioni moja unatozwa kodi shilingi 600,000 au shilingi 700,000. Wamenituma Umoja wa Majahazi Dar es Salaam wanamtaka Mheshimiwa Waziri mhusika Mheshimiwa Mbarawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mzigo wa shilingi milioni moja au milioni moja na nusu unautoza kodi shilingi 600,000 au shilingi 700,000? Wale wa nje wanatukimbia, lakini hata watu wa majahazi wanatukimbia, si aibu? Hata watu wa majahazi wanatukimbia tena nchi hii? Waliotupa kura sisi wenyewe wanatukimbia! Aaah, toba! Shughuli kubwa! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kilio na mnaoweza kunyamazisha ni ninyi. Ndiyo maana basi kuna ripoti ya utafiti wa Kimataifa ya ushindani wa kiuchumi ya uwekezaji duniani. Unaambiwa katika utafiti huo ndani ya nchi 140 Tanzania imechukua nafasi ya 120 katika mazingira bora ya kuwekeza, ushindani ule wa kiuchumi wa uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi kuliko yote, kitu ambacho binafsi kimeniuma, ni kwamba ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki, katika ripoti hiyo ya uwekezaji na ushindani wa kiuchumi Tanzania sisi ni nchi ya nne. Tunaanza na Rwanda, ya pili ni Kenya, tatu ni Uganda, Tanzania ni ya nne. Aibu siyo aibu? Baba wa Taifa alisema, ili tuendeleo tunahitaji mambo manne; watu, tunao wengi; ardhi, *Alhamdulillah*; siasa safi, hakuna, ni shida; uongozi bora, ni bora uongozi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali ina haja ya kukubali ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. Sisi wajibu wetu ni kuishauri Serikali na kuisimamia. Nye Serikali siyo mtusimamie sisi. Pokeeni ushauri wetu, ni ushauri wa bure huo! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona katika hali ambayo isiyo ya kawaida, Serikali ituambie uko wapi mpango wa Watanzania wanaoishi ughaibuni (*diasporas*) ambapo wenzetu hawa watakuwa na namna ya kuchangia na kuwekeza ndani ya nchi yetu na kuchangamkia fursa? Hamna! Hakuna mpango huo! Ni shida kweli! Tatizo! Walioko Marekani, walioko Ulaya, Mashariki ya Kati kuwatambua kwao hapa ni shida! Ni tatizo! *Diasporas* wana mchango mkubwa kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtuambie uko wapi mpango wa usafiri wa kwenye maji baharini. Mpango mzuri wa wananchi ili wasipate usumbufu kutoka Dar es Salaam kuelekea Lindi na Mtwara kwa kutumia meli? Uko wapi mpango? Mpaka wapite kwa njia ya barabara? Mtuambie mpango ulio mzuri kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi, kwenda Mtwara kwa njia za meli? Uko wapi mpango mzuri kutoka Tanga kuja Pemba, Pemba – Tanga? Uko wapi mpango mzuri wa kutoka Dar es Salaam kuelekea Mafia au hata Rufiji pale Nyamisati kuelekea Mafia? Wananchi wanapata shida na ni ukanda wote; kwenye Ziwa Victoria, uko wapi mpango ulioe mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni shida kweli! Serikali ambayo haikubali ushauri eh! Eeeh, mwaka huu! Mlisema tutaisoma, namba lakini namba tunaisoma sote. Hii namba haisomeki! Sifuri sijui tisa; siielewi mimi mwaka huu. Labda naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango atueleze zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya ya uvuvi; viwanda vya kusindika mazao ya baharini kwenye ukanda huu kuanzia Lindi, Mtwara, Dar es Salaam mpaka Tanga; viwanda vile vya kusindika mazao haya ya samaki, mpango mkakati wenu hasa ni upi? Maana bado mmeleza kijuujuu tu, hamjaka vizuri kueleza haya mambo. Mtueleze, mtuelimisha vizuri; lakini ukiangalia kwa undani, bado ni tatizo. Kuna samaki walio wengi kwenye bahari kuu, lakini bado Serikali haijaangalia namna gani ya kuweza kupata mapato kutoka baharini kwa kusindika minofu ya samaki kwenye bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara hii mmegusia utawala bora. Hivi ni kwa nini basi mmeshindwa kugusia kwenye utawala bora suala zima la *Africa Peer Review Mechanism (APRM)*. Kwa nini kwenye mpango wenu wa mwaka 2015 mligusia mpango wa kujitathmini wenyewe? Ninyi wenyewe Serikali mlikubali kuwa miongoni mwa nchi za kujitathmini wenyewe katika Afrika (*Africa Peer Review Mechanism*). Kwa nini mara hii hamkuweka basi mkajitathmini? Namna gani kesi za kubambikiza zinavyoongezeka, kama alivyosema Mheshimiwa Riziki Mngwali kwamba watu wanachukuliwa hawajui wanapelekwa wapi na wananchi taarifa hiyo hawajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niulize, hivi katika tathmini zenu hamjaangalia utaratibu ulio mzuri juu ya suala zima la wale Mashekhe mliowakamata kutoka Zanzibar kuwaleta huku Tanzania Bara? Hilo hamlijui? Ni kiasi gani jambo hilo mnalipiga dana dana? Hivi Mashekhe wale kama ni Warathi wa Mitume pamoja na yote ambayo mnayo Serikali, kuna jambo gani ambalo limejificha juu ya Mashekhe wale mliowaleta hapa na manyanyaso ambayo yapo? Kwa nini hamwendi kwenye taratibu zilizo nzuri wakafikia mahali, mnawapiga dana dana tu au mnataka wale Mashekhe waoze kwenye Magereza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu mtuambie! Kwa nini msijitathmini na hili? Maandiko mengi yamewekwa juu ya Mashekhe wale ambao mmewachukua Zanzibar mkawapeleka huku, lakini bado kuna dana dana tu. Sisi Wabunge tukiuliza, aah subirini; kuna michakato, taratibu, kuna sheria, kuna hapa na pale. Tatizo nini? Mtuambie? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, Serikali gani isiyosikia? Wanasema Serikali sikivu; mnasikia nini? Hamsikii kitu nyie! Ni shida kweli! Sisi tunapoishauri Serikali, mjue tuko makini, tunaishauri Serikali vizuri na Serikali ikae vizuri. Mtuambie majibu mazuri, siyo majibu ya kubabaisha babaisha hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaumiza kweli, siyo jambo jema hata kidogo kuona watu wale ambao ni wacha Mungu hata kama kuna makosa yoyote. Chunguzeni vizuri basi hilo jambo liende vizuri, lakini mnalipiga dana dana; huyu anasema hivi, huyu anasema hivi. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ana nafasi kubwa juu ya hili. Maandiko mengi yanapelekwa juu ya Mashekhe wale, lakini hakuna chochote mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kwa hali ilivyo tunavyokwenda, hii namba mara hii ni ngumu kweli, haisomeki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache, nakushukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sixtus Mapunda, halafu Mheshimiwa Mashimba na Mheshimiwa Flatei wajiandae.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia kwenye mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niwapongeze kwa mpango mzuri waliotengeneza. Ukiusoma mwanzo mpaka mwisho hupati shaka kwa yanayoenda kutekelezwa na hasa walipogundua kuingia na mfumo wa *program* wa kibajeti ambao mimi naamini wakijielekeza kwenye *program* itawasaidia huu Mpango ukatekelezeka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri wa Mpango huu, nimeusoma kurasa zote lakini huu Mpango una changamoto moja, umekosa kitu kinachoitwa rejea. Tukipata nafasi ya kurejea mafanikio ya Mpango uliopita, unatupa nafasi nzuri ya kushauri Mpango huu tuutekeleze vipi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walatini wana msemu *repetitio est mater studiorum* wakimaanisha marejeo ni mama wa mafunzo. Tutakwenda na mpango huu, tusipopata fursa ya kurejea mwaka mmoja uliopita kwamba tulipanga nini, tumefanikiwa nini, tufanyeje ili tusirudi nyuma, hatutafika. Hilo ndilo jambo linalotia shaka mpango huo mzuri. Tusipopata marejeo ya mafanikio ili twende vizuri zaidi; ya upungufu ili turekebishe, hatutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango aje angalau na *summary* ya tulikotoka, tulipo na tunakokwenda ili tuutendee haki huu mpango ili tufanye vizuri ndani ya mwaka ujao na baada ya miaka mitano tuseme Tanzania tuliikuta hapa, tumeitoa mwaka 2015, tunaiacha hapa 2020 kwa mpango unaoeleweka na unatabirika. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1981 Chama cha Mapinduzi kilitoa mwongozo. Kwenye ule mwongozo kuna maneno mimi napenda sana kuyatumia na huwa napenda sana yawe sehemu ya maisha ya viongozi wenye utu. Yale maneno yanasema hivi, “kujikosoa, kukosolewa na kujisahihisha siyo dalili ya kushindwa bali ni njia sahihi ya kujipanga na kufanikiwa vizuri zaidi.” Tukiona pale tulipokosea aidha kwa kuambiwa au kwa sisi wenyewe kuona maana yake tumejikosoa, siyo kwamba tumeshindwa, inatupa njia nzuri ya kutoka hapa tulipo, twende mbele zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Nasema hivi kwa sababu huu mpango umekuja na *programs* ambazo tunaamini tumezipa vipaumbele. Kuna miradi ya vielelezo. Unaposema miradi ya vielelezo tafsiri yake ni kwamba kwenye haya mambo baada ya mwaka mmoja tutasema hiki ndicho kielelezo kinachotuoonesha kwamba tumefanya vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeelezea vizuri sana kuhusu viwanda, lakini nikiangalia sioni sehemu ambapo kuna mikakati itakayokuja kukabiliana na changamoto za viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia sana nchi zilizokuwa na viwanda, aidha zile za zamani za Ulaya zilizoanza na *coal and steel industries*, Wajerumani na Waingereza; au zile za Mashariki ya Mbali zilizoanza na *textile industries* baadaye zikaendelea, hawa wote walikuwa na misingi minne ambayo namwomba Mheshimiwa Waziri Mpango aiangalie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa kwanza wa viwanda ni *power (energy)* na gharama za *energy*; msingi wa pili wa ni *qualified personnel (manpower)*; watu wenye uwezo wa kuviendesha hivyo viwanda; msingi wa tatu ni malighafi (*raw materials*). Utavilishaje hivyo viwanda? Msingi wa nne siyo katika maana ya udogo wake, *is financing*. Una uwezo gani wa kuviendesha, *kuvifinance*, kuvigharamia hivyo viwanda aidha kwa mapato yako ya ndani au kwa kushirikiana na watu wengine wenye mitaji kuja kwenye mifumo ya kuwekeza kwa kushirikiana? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiyaangalia haya yote, yananipa sababu za kutosha kumwomba Mheshimiwa Waziri ayaangalie maeneo mawili kwenye mkakati wake. Eneo la kwanza kubwa ni mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na mradi wa chuma wa Liganga. Kwa nini nilianza na kusema *repetition est mater studiorum*? Huu Mpango ulikuwa mwaka 2007, ndiyo kwa mara ya kwanza tunataka sasa Mchuchuma na Liganga ije iwekeze kutuletea chuma, ije ituwekee umeme wa kutosha na iongeze umeme mwingine kwenye gridi ya Taifa, *it was 2007*. Leo tunapoongea, *we are approaching ten years*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nasema marudio ndiyo mama wa mafunzo. Tusiporudia kutaka kujua tulipotoka, tutadhani tunakuja na kitu kipya kumbe kitu kipya kilipata changamoto nyingi sana na hizo changamoto hatukupata fursa ya kuzirekebisha. Kwenye huu mpango, Mchuchuma, mmesema itazalisha *Megawatt 600*. Kati ya *Megawatt 600*, *Megawatt 250* ndiyo zitazalisha umeme kwa ajili ya chuma kile cha Liganga na 350 ndizo sasa watauziwa TANESCO kuingia kwenye *grid* ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa za wazi zinasema haya mambo yote yako sawasawa isipokuwa kuna mvutano mmoja kwenye *power purchase agreement* ambapo mbia anataka tununue umeme kwa 13% sisi tunataka tununue umeme kwa 7%; lakini tukumbuke *agenda* ya umeme ni ya mradi mmoja tu na *agenda* ya chuma ile siyo hoja pale ya sisi kujadiliana tumeuziana umeme kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashindwa kuendelea na mradi wa chuma cha Mchuchuma kwa sababu tu ya bei ya umeme. Kwa nini kwenye zile *Megawatt 250* ambazo ndiyo za mbia, azalishe 250, atuletee chuma sisi tuzalishe chuma, tuachane na 350 ambao tutaununua kwa sh. 7/= au sh.13/= . *It is wastage of time!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mpango, kwa dhati ya moyo wangu, hebu a-focus kwenye hili kwa sababu nalo lina maneno ya hujuma; hujuma zina sura mbili. Wanasema, bwana, kusikiliza maneno ya mtaani siyo jambo zuri, lakini yakisemwa kwa muda mrefu yanawafanya watu waamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema huu mradi unahujumiwa; kwanza unahujumiwa na mashirika makubwa na makampuni makubwa ya upande mwingine kwa sababu mradi kapewa Mchina, wanataka usuesue usifike kwa wakati, lakini wa pili wanasema, eh, kwa sababu Kusini siku zote ni Kusini, basi Kusini iwe ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mambo hayatujengi sisi kama Wabunge, haya mambo yanatufarakanisha, yanatufanya sisi watu wa Kusini tuendeleo kuwa maskini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie Kusini siyo Kusini kama mnavyofikiri, kama Kusini ingekuwa inamaanisha chini, Mto Nile usingetoka Ziwa Victoria kwenda Kaskazini. Nataka kukwambia Kusini ni juu na Kaskazini ni chini kwa lugha kama hiyo. Niombe kabisa, tusifike sehemu tukawafanya watu wa Kusini ionekane kwamba wanahujumiwa katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujipe muda wa kutosha kwenye hoja nzima ya Mchuchuma na Liganga. Kwa nini nasema hivi? Kanuni ni mbili tu; tukifanikiwa kwenye Mchuchuma katika maana ya kuleta chuma na chuma kile hakitafika peke yake, kitakuwa na madini mawili, tutapata *vanadium* na *titanium*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku chuma sasa ndipo tutakapoongelea mataruma yale ya kwenda reli ya kati yapatikane pale; mtakapotaka sasa madaraja yenu, vitu vitoke pale. Ndiyo zile kanuni nne nilizosisema; angalia sehemu zote, angalia eneo la *power*; *power* tunayo. Sasa unafanyaje kukifanya kiwanda cha *textile industry* kiende vizuri? *Power* yetu ni ghali, tuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatengeneza kiwanda cha nguo, tuna soko kubwa la nguo, tutashindwa ku-*compete* kitakufa. Kwa sababu nguo ya Thailand, China na Uturuki itauzwa bei ya chini kwa sababu ya *cost of production*, haya mambo yote Mheshimiwa Mpango yaweke katika mizani yake, tutatue hili tatizo Watanzania tutoke hapa tulipo twende mbele zaidi. Watanzania wanataka viwanda, nami nataka viwanda, nawe unataka viwanda; lakini viwanda lazima tuvipange vizuri kwa kuangalia kila *element*, tusiache *untouched stone*, kila jiwe likanyagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mashimba Ndaki, halafu Mheshimiwa Flatei na Mheshimiwa Sanga wajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami pia niweze kuchangia mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kama ambavyo Mheshimiwa Mapunda amesema. Nilidhani kwamba tungekuwa na rejea ambayo inatuelekeza ni kwa namna gani angalau tumejaribu kufanya kwa mwaka huu ambao unaelekea mwishoni, ingekuwa nzuri sana; lakini sasa tumekosa hiyo. Wakati nasoma haya mapendekezo nikawa najjuliza, hivi inakuwaje mtu anafikiria kuoa mke wa pili wakati huyu wa kwanza hata hajamwoa? (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unamwita mke wa pili au mke wa kwanza? Sasa kwa kweli hiyo tu ndiyo imeleta shida kwenye mapendekezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni vizuri kama ndiyo taratibu zetu, kanuni zetu au sheria zetu, basi ni vizuri kuzibadilisha ili tupate angalau matokeo ya miezi sita ya mpango ule uliopo kwenye mwaka, halafu tuweze kuangalia

sasa tunapendekeza nini. Vinginevyo inakuwa ngumu kweli kweli kuchangia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kitu cha pili kabla sijatoa mchango wangu. Cha pili ni kwamba, mwaka 2015 tulipokuwa kwenye uchaguzi kila mtu alikuwa anaimba mabadiliko. Mabadiliko ni rahisi kuyaimba lakini yana tabia moja ambayo siyo nzuri wakati mwingine. Mabadiliko yana tabia ya kumtoa mtu kwenye *comfort zone* yake. Sasa inaelekea Serikali hii ya Awamu ya Tano, kwa sababu imevaa njuga za mabadiliko, watu wengi hatufurahii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba kama tunataka mabadiliko, ni lazima tutoke kwenye *comfort zone* tuliyokuwa tumezoea. Haiwezekani ukataka kwenda Peponi au Mbinguni bila kufanya ibada. Ibadu nyingine ni mara tano kwa siku, nyingine inabidi uache kula na kunywa, lengo tu ufike Peponi au Mbinguni.

Sasa kuna vitu ambavyo sisi kama wananchi na Serikali yetu kama kweli tunataka mabadiliko yaliyo ya maana, vitu vingine inabidi tuvisahau na vitu vingine inabidi tuviache kwa sababu tunataka mabadiliko. Hatuwezi kufikia mafanikio ikiwa tutataka tukae kwenye raha ile tuliyokuwa nayo miaka 50 iliyopita. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ni lazima tulielewe hilo hata tunapojadili hali ngumu za maisha zinazowakabili watu wetu, tujue kuwa hiyo ndiyo hali halisi ya kutaka mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili ni kwamba humu Bungeni kuna kitu ambacho mimi sijakipenda sana kinatugawa Wabunge. Kuna kitu kinasemwa na Wabunge wengi wewe huwajui wapiga kura, wewe hukupigiwa kura, kuna mtu hakupigiwa kura humu ndani?

**MBUNGE FULANI:** Ndio.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Hapana. Mimi naamini kila Mbunge amepigiwa kura hapa, kura zetu zinatofatiana idadi tu, Mheshimiwa Mpango amepigiwa kura moja akawa Mbunge. Mimi nimepigiwa kura makumi elfu nikawa Mbunge, wenzetu wa Viti Maalum wamepigiwa kura kadhaa ni Wabunge, sasa tunapofika humu na kuanza kugawanyana wewe hujapigiwa kura, wewe huwajui wapiga kura, kila mtu anajua mpiga kura wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kutahadharisha tu ni kwamba Mheshimiwa Mpango kura yako wewe ni moja ukapata Ubunge, lakini nyuma ya kura moja kuna kura mamilioni ya Watanzania yaliyompa kura aliyekupa wewe kura. Kwa hiyo, aliyekupa kura anatarajia mamilioni ya kura za

Watanzania waliompigia waguswe kupitia wewe. Wewe ni Mbunge kabisa halali wa kupigiwa kura, ni Mbunge halali na Uwaziri wako ni halali, lakini kumbuka kuna kura nyingi huko nyuma ya kura yako zinataka kuguswa na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye kuchangia mapendekezo. Kitu cha kwanza mapendekezo yanasema kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu, ninakubaliana nayo, lakini ili maendeleo ya watu yaonekane yamefungamanishwa na maendeleo ya uchumi lazima ionekane kwamba katika huduma zile za kijamii ambazo zinagusa watu wengi, wananchi wetu wanazipata kwa urahisi kwa gharama nafuu, wanazipata wanapozihitaji. Hali ilivyo, wakati huu kwa kweli haiko namna hiyo, kwa sababu mpango ambao tuko nao sasa hivi haujawahi kutekelezwa kikamilifu kiasi cha kugusa maeneo yanayogusa wananchi wengi, kwa mfano afya, elimu na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapotaka kukuza uchumi wetu ili ufungamane na maendeleo ya watu lazima tufanye juu chini katika mapendekezo haya tufanye juhudi zile zinazogusa wananchi wetu hasa wanyonge. Tusipofanya hivyo hatutafungamanisha maendeleo ya uchumi wetu unakua ndio, lakini watu wetu watabaki kwenye hali zile zile, kwa hiyo ni ushauri wangu wa kwanza huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunatakiwa tuwe na miradi ya kielelezo ndiyo, lakini miradi ya kielelezo kutoka mwaka juzi, kutoka miaka ya nyuma sana mpaka tunaendelea na kuendelea nayo nadhani pia hii sio mpango mzuri, sio utaratibu mzuri. Nimejaribu kuangalia mapendekezo ya mpango huu, mimi nikawa nafikiri ningekuta kuna mradi angalau mmoja wa kielelezo wa umwagiliaji lakini hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napendekeza ni vizuri na ni muhimu sana tukaangalia kwa sababu tumekwishakupewa taarifa, hali ya hewa ya mwaka tunaoundea sio nzuri. Watu wa hali ya hewa wametuambia, lakini pia mabadiliko ya tabia nchi yanatueleza hivyo, hali sio nzuri ya mvua zitakazonyesha baadae, lakini tuna eneo na maeneo makubwa ambayo yangeweza kumwagiliwa yakatupa chakula na mazao ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mapendekezo haya unaona vitu vingine tu lakini jambo la umwagiliaji ambalo lingetupa maji ya uhakika halijawekewa msimamo, ambalo lingetupa mazao kila wakati, halijawekewa mpango, sasa tunafanyaje? Nahisi habari hii ya kuwa na umwagiliaji mkubwa ni ya muhimu sana kuwekwa kwenye mpango kwa sababu tuna vyanzo vya maji vingi, maziwa matatu makubwa na mito mikubwa tunayo hapa nchini kwetu, hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni uvuvi wa bahari kuu, hatujaona humu kama kwenye mpango kunapendekezwa kitu chochote. Mheshimiwa Rais ameimba wakati wa kampeni anasema anashangaa kwa nini ukanda wetu wa Pwani hakuna hata kiwanda kimoja cha samaki, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunashangaa hatuna meli ya kuvua hata moja ambayo ingeweza kununuliwa na Serikali kwa bei ambayo iko chini ya bei ya *Bombardier*, inawezekana kabisa tukinunua meli moja tunaweza tukawa na uvuvi mkubwa kwenye bahari kuu. Lakini kwenye mapendekezo haya unaona tu uvuvi umetajwatajwa tu kifupi kifupi tu lakini hakuna *seriousness* yoyote ambayo unaiangalia na kuiona iko humo ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha tatu ambacho nimekikosa ni mazao yetu makuu ya biashara kwenye mpango, kwenye mapendekezo hayapo, lakini ukijaribu kuangalia takwimu mazao yetu makuu ya biashara korosho, tumbaku, kahawa, pamba mazao haya uzalishaji wake unapungua kila mwaka, uko chini lakini kwenye mapendekezo hakuna kitu chochote kinachotajwa angalau mkakati kuonyesha ya kwamba tuna mkakati wa maana kupandisha uzalishaji wa mazao haya ili tuweze kupata hela nyingi za kigeni, lakini pia watu wetu waweze kujipatia kipato kwa sababu ndio wengi wanaolima mazao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nipendekeze pia kwamba mapendekezo haya ya mpango yajaribu kuangalia mazao makuu ya biashara tunafanyaje juu ya haya ili kwamba kuweza kupandisha kipato cha wananchi wetu. Mengi ya mazao haya tunauza yakiwa ghafi, kwenye mapendekezo ya mpango hakuna dalili zozote ya kuyageuza ili angalau tuyauze yakiwa na *value added*, hakuna, sasa tunafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka kusema hayo machache tu nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Flatei, jiandae Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachangia Mpango huu au Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya mwakani yaani 2017/2018 ni vema sasa tukafika mahali tukaongea uhalisia ambao utatupeleka katika maendeleo ya kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma vizuri sana Mpango huu, unaonekana kwa kweli ni mzuri, lakini mimi nina walakini kwa kuangalia mipango ambayo ipo na imeandikwa hapa hasa katika maeneo ya uzalishaji wa viwanda vidogo vidogo. Pia kuna mipango mikakati ambayo imeelezwa hapa katika mpango huu ambayo kimsingi nimekuwa nikisikia mimi kabla sijawa Mbunge na sasa nimeingia humu bado naendelea kuisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kuna mpango huu kwa miradi hii ya Kinyerezi, mipango hii ya *Special Economic Zone*, ni kweli Tanzania tunahitaji umeme na tunaona maeneo mengi yana ukosefu wa umeme. Lakini tunaona kabisa hapa mpango huu unaonesha kwamba utakuwa na faida ya kuongeza megawati 600, lakini tumekuwa na mipango mingi hatuoni utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia miradi hii ambayo imeoneshwa kwenye mpango wa Serikali hapa, vituo vya biashara vya Kurasini imekuwa ikisemwa muda mwingi, lakini sasa ukiangalia fidia imeshatolewa na mamilioni yako hapa yanaoneka sitaki kuingia *in detail*, lakini hoja yangu ni hii tu Serikali imeshaweka fedha nyingi hapa sasa na muda unaanza kwenda, ituambie basi ni lini inaanzisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina wasiwasi unaweza ukabeba mpango huu ukaelekea tena mwakani kwa sababu naamini kwenye mpango uliopita ulikuwepo, Kurasini, Kinyerezi, viwanda vidogo vidogo ambavyo vimekuwa vikielezwa hapa na hii SEZ, tunapiga maswali kwa wale wengine ambao tunakaa mbali na maeneo haya. Umeme tunahitaji kweli, viwanda tunahitaji kweli lakini ni lini sasa unaanza? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila tunapoona mipango tunategemea kwamba Serikali itakwenda kuifanya, tunaposoma vitabu hivi tunaamini kabisa mipango hii ya Serikali inakwenda kutekelezwa, lakini kinachotutia kichefuchefu ni kwamba tuna tatizo moja hapa kwetu la kutenda, tunatenda lini? Maamuzi tunayafanya lakini wakati wa kwenda kutenda hapo ndio tunaanza kuona danadana, leo, kesho, kesho kutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vizuri upande wa kilimo unaona kabisa mipango mizuri, ipo katika vitabu vyetu hivi na unaisoma vizuri sana, kwa mfano ukiangalia mpango wa kilimo umeiandika vizuri sana Mheshimiwa Mpango, je, wakati wa kwenda kutekeleza tunatekeleza kama tulivyoandika? Hilo ndilo tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia kwa uhalisia wa mwaka huu, tunaposema tunakwenda kusaidia sekta ya kilimo wananchi wetu wanajua tunakwenda kweli kusaidia tukiwa tumeamua kwa sababu mpango huu umeelezwa humo, na Wabunge kazi yetu kubwa ni kuishauri Serikali, hapa

tunaposhauri naomba ushauri huu uchukuliwe, na ukafanyiwe kazi wakati tumeamua kushauri, kwa sababu sisi ni Bunge na wao ni Serikali tunaamini ya kwamba tunafanya kazi katika *three pillars of the one government (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tufanye kazi moja rahisi tu, tunapoingia huku tunaingia kama tuna vyama, lakini tunapokuja huku tunawakilisha wale wasiokuwa na vyama, na wale wenye vyama. Mimi naomba lingine niwashauri ndugu zetu wa upinzani mara chache tunapoingia humu, tunaanza kukashifiana kwa lugha ambazo sio nzuri, hizi lugha zinatuondoa kwenye *mood* wa kuangalia *fact issues* ambazo zinafanya sisi Watanzania kule waone kwamba tumekuja huku kuwatetea. Tunapojadili habari hii kwa mfano kilimo sasa, hali halisi mpaka sasa hivi kwa sisi Wabunge tunaotoka maeneo ya kilimo hakuna pembejeo, hakuna ruzuku sijui ni lini tutapata. Sasa tukianza kuongea hatuna maana ya kusema jambo lolote mbadala na hili, ni hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo kwa mfano, mimi kule nategemea kilimo, tunategemea mifugo, pembejeo za kilimo hazipo, Serikali imekwisha kuahidi, Mheshimiwa Rais alikwisha kusema je, hebu tuambiane mpango huu unaeleza pia, kuna fedha imetengwa, je tunapatiwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi mvua zimeaza kunyesha je, hizi pembejeo tutakapopeleka baada ya mvua kunyesha; kwa mfano ukipeleka mahindi au ruzuku yeyote na pembejeo hizo, mbolea wakati msimu umeshapita unampeleka nani? Je, tukipata mwezi wa pili inafaa kupikiwa kande? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba tu tufike mahali tuende kwenye uhalisia wenyewe, lakini hata mkulima huyu, ukiangalia takwimu zinaonesha asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo, angalia leo kilimo hiki hakimsaidii na leo kuna maswali mengi yameulizwa asubuhi kuhusu kilimo na hali inaonekana kabisa kilimo ndiyo tegemeo. Lakini ukiangalia miradi yote ya umwagiliaji imesimama tatizo ni hela hakuna, hapa imeandikwa vizuri sana, sasa *nina-declare* tunafanyaje ili kuisaidia nchi yetu kama tunashauri halafu yale ambayo tunashauri hayatekelezwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali yetu tunaipenda sana ninaona kabisa jitihada za Waziri, naona jitihada za Rais, nazona kabisa jitihada zinazofanyika, tukafanye kazi ya kufanya kazi ambayo tumeamua kuifanya kweli. Angalia wakulima sasa hivi wamechoka, sisi vijana ambao tumekuja kuwatetea vijana tumeanzisha SACCOS zetu kule lakini utaangalia nimshauri sana ndugu yangu Waziri Mpango, kuna kodi ambayo imeanza kuwa katika maeneo yetu kule. Kodi hii inaenda kuwalenga wakulima wadogo wadogo wanaochajiwa VAT, tumeanzisha SACCOS, AMCOS katika maeneo yetu kule, lakini kodi hii ukiangalia ndiyo kodi ambayo Mheshimiwa Rais amesema kodi



kero tuondoe. Hivi leo mkulima mmoja mmoja anadaiwa zuio la kodi hii haistahili na hii siyo sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali iangalie maeneo ya kuweka kodi na maeneo ambayo hayapaswi kuwekwa kodi. Tuliingia huku tukisema habari ya kodi kwa watalii kwenye maeneo yetu ya kule, lakini tazama leo tunaona athari zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu wakati mwingine tunaposhauri kama Wabunge Serikali ichukue ule ushauri ikaufanyie kazi, bahati nzuri Tanzania tuna wasomi leo, tufanye *research* tuone kabisa je haya tunayoshauriwa na Waheshimiwa Wabunge ndiyo hasa yale ambayo wanaona kwa ushauri wao na kama wanakataa wakatae kwa hoja na sisi tunapoeleza tunaeleza kwa hoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye suala la miundombinu imeelezwa hapa, uboreshaji wa miundombinu, imeelezwa habari ya ATCL, imeelezwa habari ya TAZARA, imeelezwa habari ya ndege na yameelezwa mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine naangalia ninapoingia huku kule maeneo ya kwetu hatuwezi kukutana na hiyo ATCL, hatuwezi kukutana na hiyo TAZARA, hatuwezi kukutana na meli kwa sababu hatuna maziwa, hatuwezi kukutana na chochote ambacho mnasema, *standard gauge* ndio kabisa huku kwetu haipiti, sina maana ya kujitenga katika Tanzania, lakini nina maana ya kuuliza swali moja tu kama hamtatusaidia sisi barabara zetu zikaonekana kwenye huu mpango tutakuwa tumeingia kufanya nini huku. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa maeneo ya pembezoni tuangaliwe kama tunagawa rasilimali ya nchi hii tuigawe kwa usawa, haiwezekani maeneo fulani yanaonekana miradi mikubwa imeenda huko na maeneo fulani yamenyimwa kabisa. Ninajua wazi kwamba tutafaidi wote lakini tufaidi basi hata barabara. Sisi kwa Mikoa yetu ya Kaskazini ukiacha barabara hatuna kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine napenda kuishauri Serikali, hasa hili la mabenki ambayo kwa kweli sasa hivi tunaona *crisis* imetokea mimi sio mtaalamu wa uchumi lakini katika *study* yangu nime-*study* kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia tumekuwa tukishauri hapa habari ya vyanzo vya mapato, tunapenda sana kukusanya mapato, lakini naomba nishauri Serikali iangalie hii habari ya kukopa ndani ya nchi Serikali iangalie kwa sababu kuna fursa ya kukopa nje, kwa nini Serikali isitumie nafasi hii ambayo inayo ya kukopa nje ya nchi kuliko ndani kwenye mashirika ya kwake yenyewe? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie basi kwa sababu ninaamini kwamba Serikali ina nafasi ya kukopa nje, Serikali inaweza kufanya jambo lingine ione kama kukopa ndani na kukopa nje ipi nafuu. Lakini kwa sababu nimesikia kengele ya mwisho niseme kidogo katika suala la *fluctuation* hili suala la kufanya *fixing rating*. Tufanye utafiti wa kweli, tunaweza kuangalia tukaishauri Serikali ikaamua kubadilisha mtindo wa sasa wa kuangalia soko la dunia katika upandaji wa dola na kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza swali moja tukiamua kubadilisha mfumo huo, je, Benki Kuu ya Tanzania inaweza kweli kuhimili mapigo ya kushuka kwa uchumi hasa inaposhuka itapata wapi fedha ya kufidia ile sehemu na ile *gape*? Kwa hiyo, naomba Wizara ijipange, Serikali iangalie kama imekuwa tayari kweli kuingia katika mtindo huu, ikiingia hapa lazima nayo Benki Kuu imejiandaa katika kuziba *gape* la kiuchumi, vinginevyo uchumi wa dunia ukishuka, Tanzania hatupo nje ya dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba kuchangia hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Deo Sanga, ajiandae Mheshimiwa Chegeni.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mpango huu ambao umeletwa mbele yetu. Mpango huu ni mzuri sana, una mwelekeo mzuri na dira nzuri ya kuhakikisha shughuli zote ambazo zimepangwa hapa zinakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hata vitabu vitakatifu vinasema unapotaka kwenda peponi au mbinguni ni lazima ukeshe ukiomba. Sasa kazi ya kukesha na kuomba si ndogo, ni kubwa sana, kazi ya kukesha na kuomba na ukishakesha na kuomba ndio unaweza kufika peponi au mbinguni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Awamu ya Tano kazi kubwa ambayo ilikuwa ikiifanya ni kuturudisha kwenye mfumo, kuachana na ule utaratibu tuliouzoa kwa hiyo, ilikuwa inaturudisha kwenye mfumo. Turudi tujenge nidhamu katika Serikali na kazi hiyo imefanywa na Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, amefanya kazi nzuri sana. Hata wakati anawaambia Watanzania anaomba ridhaa aliyasema haya kwamba, nipeni nitafanya moja, mbili, tatu; leo anayafanya haya tunasema aahhaa, anafanya vibaya! Lakini mtu mmoja amewahi kusema ukiona mtu anakusifia jiangalie mara mbili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inayofanywa na Serikali kupitia Mawaziri waliopo na huyu ambaye ameleta mpango huu ni kazi nzuri sana. Sasa kwamba Serikali imeturudisha kwenye mfumo, imedhibiti mambo ya pesa,

Mheshimiwa Mpango baada ya kudhibiti sasa peleka kwenye Halmashauri ili zikafanye kazi, maana kwanza alikuwa anaturidisha kwenye mfumo na sasa tumerudi kwenye mfumo, kwa hiyo fedha sasa zianze kwenda kwenye Halmashauri ili zikafanye kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu waliozungumzia habari ya Liganga na Mchuchuma. Na mimi napata ukakasi, hivi kuna tatizo gani linalofanya shughuli ya Liganga na Mchuchuma ikwame? Kwenye mpango imekaa vizuri, tunaomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana suala la Liganga na Mchuchuma hebu sasa liweze kusonga mbele kadri ambavyo lilikuwa limepangwa ili liweze kusaidia Tanzania, tuweze kupata ajira nyingi kwa vijana wetu wa Tanzania kama ambavyo mpango upo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua napata taabu kitu kimoja kidogo sana! Mambo mengi amenimalizia yuko pale, ambayo nilikuwa nimeyaweka hapa kwa sababu...! Sasa naomba niseme! Eeh, ndio mwenyewe! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani wote ni Wabunge sawa, kila mmoja ana hadhi yake ameingia hapa, tunahitaji kuheshimiana. Tunapomnyooshea mtu, Mbunge mwenzako kwamba eti wewe huoni chungu kwa sababu uliteuliwa, tena huyu ndiye anaheshima kubwa sana kuliko wewe, kwa sababu kama alivyosema Mbunge mwenzangu pale kwamba kila mmoja amepata kura kwa idadi tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani aliyepata humu ndani kura nyingi kama za Mheshimiwa Magufuli, nani? Sasa zile zote si ndio amepewa yule kwa heshima ya Watanzania? Ndugu zangu tuheshimiane, aliyeteuliwa, ambaye hakuteuliwa wote ni Wabunge. Wakati fulani ninyi wenyewe ndio mnatoka huko mnakwenda pale, Waziri eeh, moja, mbili, tatu! Ni Waziri huyu, apewe heshima yake kama ambavyo Wabunge wengine tuko hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kudhibiti mambo yote sasa peleka fedha Halmashauri zikalipe na fidia zile pamoja na Makambako ikiwemo. Kuna fidia kule wananchi wangu wanadai kule ili zikaweze kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla mpango huu nauunga mkono vizuri, ni mpango mzuri ambao sasa peleka fedha zikaanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sina la ziada. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chegeni na ajiandae Mheshimiwa Gekul.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, amefanya kazi yake na mpango huu ni mpango mzima wa Serikali. Ni matarajio yangu kwamba tunapozungumza mpango huu hatuzungumzii peke yake Waziri wa Fedha, tunazungumza *co-ordination* yote ya Serikali ndani ya mpango huu. Kwa maana hiyo Waziri Mpango naomba uwe msikivu, lazima uwe msikivu na ujaribu kuyachukua mawazo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge tunayatoa hapa kwa mustakabali wa nchi hii.

Mheshimiwa Mpango nikupe tu siri moja, ni mtaalam mzuri, msomi mzuri, lakini una *professional arrogance*, una kakiburi, na mtu anayekwambia ukweli anakusaidia. Tunasema hivi ili baadae tutoke hapa tulipo tusonge mbele zaidi. Wenzangu wamesema tunaheshimu kila Mbunge aliyepo hapa ndani kwa sababu ameingia kwa nafasi yake, na wewe uko hapa kwa heshima zote, lakini chukua mawazo ya Waheshimiwa Wabunge yafanyie kazi, usipofanya hivi inatupa ugumu sisi na ukakasi wa kusema na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi nyuma Mheshimiwa Mpango kwenye bajeti ya Serikali iliyopitishwa mwaka jana, vitu vingi tulipendekeza hapa vilikuwa na mambo mazuri sana, lakini nadhani kwa kufikiria kwako au kwa kuona kwako mambo mengi hayakufanyika kama tulivyokuwa tumependekeza. Hii sisi ilitupa nafasi ngumu sana ya kuelewa sasa tunakwendaje kama Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili mpango huu unapaswa kuwa tenganifu, we *should harmonise*, mambo yote ambayo yanahusika katika kuwezesha uweze kutekelezeka. Haiwezekani tunapanga mipango, unakuja na kitabu hiki, hutuelezi vizuri kwamba hapa ya mwaka jana tumefanyaje, wapi tumekwama, nini tufanye kwa safari hii! Kwa sababu unapozungumza katika suala la mpango, lazima tu-*reflect* tumetoka wapi, nini tumefanya, nini tumeshindwa kufanya na nini tukifanye zaidi kipindi kinachokuja. Sasa Mheshimiwa Mpango naomba utusikilize sana, tunapotoa ushauri ni kwa nia njema, lakini vilevile tuki-echo kazi nzuri anayofanya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekuwa na nia njema sana, lakini naanza kupata wasiwasi kwamba inawezekana mlio karibu nae hamtoi ushauri stahiki kwake, hii inasababisha baadhi ya mambo mengine yasifanyike kama ambavyo watu wanategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tunaomba ifanye kazi kama timu moja. Haiwezekani Serikali hiyohiyo Waziri huyu anasema hiki, huyu anasema hiki, hakuna *co-ordination!* Na hili ndiyo tatizo ambalo linafanya hata Bunge hili lishindwe kuwashauri vizuri zaidi. Kwa hiyo, naomba sana kupitia mpango huu Mheshimiwa Mpango ongoza wenzako katika kutekeleza mpango huu, lakini uwe msikivu, usikivu wako utakusaidia ili tuweze kufanya kazi vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sasa hivi tunasema uchumi unakua. Ni kweli, ukienda *by figures and facts they never lie*, lakini hali halisi lazima iwe *translated* kwa wananchi wenyewe, waweze kuona kwamba uchumi sasa kweli unakua. Kama hakuna *translation*, hakuna *trickle down effect*, hata tungesema namna gani hii itakuwa ni ngonjera ambayo haina mwimbaji.

Nakuomba sana suala zima kwa mfano la kodi, tulisema hivi suala la kuweka *VAT on auxiliary services and transit goods* italeti matatizo. Tukiweka *VAT* kwenye *tourism sector* italeti tatizo! Tumeona yote haya kwa mfano sekta sasa hivi ya utalii imedorora, lakini mnasema eti imekua! Sasa nashangaa inakuaje wakati tunaona kabisa *the actual situation* hali ni mbaya, wewe unasema inakua!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumneona suala la bandari, ndiyo kulikuwa kuna ukwepaji kodi, suala la kimfumo na utaratibu *TRA* wangeweza kufanya kudhibiti, lakini tunategemea kwamba tupate *floor* nyingi ya mizingo inayokuja tuweze kupata mapato makubwa zaidi, Mheshimiwa Mpango naomba haya mambo ujaribu kuyasikiliza vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi tuka-*introduce VAT on financial services*. Tunaona sasa hivi mabenki yanavyo-*suffer*. Tunaona jinsi ambavyo hali ya kibenki na hali ya kiuchumi inavyozidi kuyumba. Tunaomba sasa kufanya kosa siyo kosa, kurudia kosa ni makosa. Tujisahihishe, kama kuna mahali tulikosea tujaribu kurekebisha mapema, tusiwe tunajaribu ku-*copy* mambo fulani na kuja kuya-*paste* hapa, tuyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba suala zima la *perception management* lifanyiwe kazi. Kuna watu wana *perception* za kwao kwamba sasa hivi uchumi wa Tanzania unakua, wengine wanasema uchumi wa Tanzania haukui, lakini ninaamini kwamba kwa sababu *numbers* na *figures never lie* uchumi unakua, lakini tunachoomba ni *translation* ya uchumi huo kwa wananchi waweze kuona kwamba uchumi unakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Halmashauri nyingi hazina fedha, Serikali haina pesa, wananchi hawana hela! Sasa unapozungumza *production*, kukua kwa uchumi ni pamoja na *production*, sasa kama *production* haiongezeki uchumi hauwezi kukua. Wananchi watazidi ku-*suffer* na ku-*suffer*, mimi ninaamini

kwamba Serikali hii ni sikivu na inajaribu kuyafanyia kazi mambo ambayo yamekuwa yana matatizo yaweze kurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imebana sana *spending* yake, lakini fedha iko wapi? TRA makusanyo yameongezeka kutoka shilingi bilioni 850 mpaka *1.3 trillion*, lakini ukiangalia *outflow* ya pesa tumekuwa na madeni, Deni la Taifa linazidi kupanda utadhani *as if* Waziri wa Fedha hutumii nafasi yako kuya-manage haya kwa sababu *you need to do a financial management, is just a simple financial management.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani pesa zinazidi kutumika zaidi licha ya makusanyo kuongezeka, lakini bado *spending* yake inakuwa *challengeable!* Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kupitia mpango huu ninaamini kwamba Watanzania tuna imani na wewe na Bunge hili litumie kama ni chachu ya kukusaidia wewe ufanye kazi yako vizuri zaidi, lakini timiza wajibu wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema hata kwenye maandiko mtu mnyenyekevu hata Mungu anampa baraka, nyenyekea Mheshimiwa Mpango, unapewa ushauri na watu sikiliza. Watu wa *Business Community* wamekuita mara nyingi ukutane nao unakataa! *And then you came to the budget!* Kamati ya Bajeti hapa, walikuwa wanasema Waziri tunamuita haji kwenye vikao. Sasa najiuliza kwamba sasa ni Waziri anafanya kazi gani hizi? Ni aibu, ni aibu. Dhamana ambayo unayo ni kubwa, hebu jaribu kuwa msikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni sekta ya kilimo, sekta ya uvuvi ambayo inaajiri watu wengi sana inatakiwa sasa iwekewe kipaumbele, ili wananchi sasa na hasa wakulima, wavuvi na uzalishaji wa viwanda, tunasema kwamba ni Serikali ya viwanda, sera yetu ni ya kujenga viwanda, lakini huwezi ukajenga viwanda ukafanikiwa kama unakuta Waziri wa Viwanda tena wanamuita mzee wa *sound!* Eti mzee wa *sound*, Waziri wa Viwanda ni mzee wa *sound!* Haiwezekani! Tunachotaka sisi ni Waziri azungumze vitu ambavyo vinatekelezeka siyo porojo za kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahali tukubali changamoto hizi, tupunguze maneno lakini tuwajibike zaidi na tutekeleze zaidi. Leo hii wananchi wanachotaka ni kuona kwamba matokeo yanapatikana. Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana, anafanya kila njia kuona Watanzania wananufaika na uchumi wao, Watanzania wananufaika na rasilimali zao na ninyi msaidieni sasa kwa nafasi zenu acheni maneno. Acheni kusigana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wenzetu wa Kenya walianza kito kinachoitwa *interest rate capping*. Riba kwenye mabanki zinazidi kupanda na zinapopanda ina maana wananchi sasa hivi wanashindwa kukopa fedha, wanashindwa kufanya *production*, kuna haja sasa Mheshimiwa Mpango suala

zima la riba kwenye benki liangaliwe upya. Serikali ifanye *serious intervention* ili kusudi mabenki haya yawasaidie wananchi kama wanakopa fedha basi ziweze kutumika vizuri katika kukuza uchumi wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kwamba lazima baadhi ya gharama nyingine za uzalishaji hapa Tanzania zipungue gharama. Huwezi ukasema unaweka viwanda wakati gharama ya umeme ni ghali, maji ni ghali, halafu kuna *series* kubwa sana ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kodi zaidi ya 100 ambazo mtu anapaswa kuzilipa, haiwezekani! Ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kupitia mpango huu hebu jaribu kuja na kitu ambacho kitasaidia ku-*harmonise* yote haya. Vinginevyo mpango wako ni mzuri na mimi sijawahi kukukosoa, mpango huu ni mzuri, lakini hakikisha kwamba unakuwa msikivu na yale mambo ya msingi yafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba yawezekana tuna itikadi tofauti, lakini maslahi yetu ni ya Watanzania wote. Hakuna mtu ambaye ana maslahi nje ya Watanzania na lolote unalolifanya ndani ya Bunge hili litusaidie kumsaidia Mtanzania ambaye ndiye ametuweka sisi hapa ndani. Ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge kupitia Bunge hili na haki za Wabunge ziweze sasa kuzingatiwa kwa sababu vilevile Mbunge aweze kufanya kazi zake anahitaji kuwa na uwezo wa kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Mpango pamoja na yote kapu lote umelikamata wewe na usidhani kwamba watu wanavyokuona namna hii wewe ni Waziri zaidi ya Waziri kwa maana umeshika sekta nyeti, lakini hakikisha kwamba unamshauri Rais vizuri, sikiliza wadau na mtekeleze yale ambayo Watanzania wanahitaji kuyaona. Tungependa kuona kwamba ndoto ya Mheshimiwa Rais Magufuli inatimizwa na Watanzania baada ya miaka mitano tuseme kwamba sasa uongozi wa Awamu ya Tano wa Serikali ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli umeweza kufanya moja, mbili, tatu na tujivunie kwa hilo, lakini naomba katika mpango huu vilevile sekta zote na Wizara zote zinakuwa *harmonized* hii itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wote, Mheshimiwa *Chief Whip*, mpango huu Mawaziri wanapaswa kuwa humu ndani wasikilize, ni wajibu wao kuona kwamba kila Waziri katika sekta yake anashiriki kikamilifu katika mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (Makofi)

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa.

### TAARIFA

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ili kuweka *record* sawasawa, naomba kutoa taarifa kwa mchangiaji aliyemaliza sasa hivi, hakuna hata siku moja ambapo Kamati ya Bajeti ilimuita Waziri wa Fedha akashindwa kupatikana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gekul hayupo, Mheshimiwa Heche ajiandae na Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri isingekuwa sahihi sana kama Wabunge wengine ambavyo wamezungumza kuanza kuchangia kwenye mpango huu au mipango mingine yoyote ya Serikali kabla ya kufanya tathmini ya mpango uliokuwepo ambao tunaendelea nao sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko kwenye *quarter* ya pili ya bajeti, Halmashauri hazijapelekewa pesa, hazijapelekewa OC, watu wanalia, mnataka wakusanye mapato lakini hamjawawezesha kuweza kukusanya hayo mapato, kwa sababu bila OC sijui mnataka watu watembeke kwa miguu kwenda kwenye minada kukusanya pesa, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema hivi, mimi sio mtabiri, lakini nataka nikuambie Waziri Mpango baada ya Waziri aliyetumbuliwa hapa unamkumbuka, anayefuata ni wewe, wewe ndio utakuwa wa pili kutumbuliwa na Mheshimiwa Rais Magufuli. Na kwa nini utakuwa wa pili ni kwa sababu mambo yanapokwama, mipango mliyopanga yote inapokwama wewe ndio utabebeshwa zigo hilo ili aonekane yeye yupo sawa wakati mnakosea wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira; mnaleta hapa kuzungumza mipango hii, mlisema hamuajiri kwa sababu mnafanya tathmini ya watumishi sijui kutafuta watumishi hewa, haya mmetafuta hewa mwaka mzima, vijana wamesomeshwa na baba zao watu maskini wako mitaani, dada zetu wanajiuza. (*Makofi*)



Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo nayo sijui mnatafuta wanafunzi hewa. Kilimo hakuna pembejeo mnatafuta majembe hewa, mnatafuta wakulima hewa? Jambo la msingi ni kwamba msem Serikali yenu imefilisika na haiweze kutekeleza chochote msaidiwe kuliko mnakuja hapa mnasema watumishi hewa, watumishi hewa mnatafuta mwaka mzima, wakulima hewa mnatafuta mwaka mzima, kilimo kimesimama. Wanafunzi mkawapa mikopo mwaka jana, mambo ya aibu kweli kweli! mwaka jana tumewapa mkopo leo mtu anaingia mwaka wa pili hamtaki kumpa mkopo, wengine wanaingia mwaka wa tatu hamtaki kuwapa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yenu hii mlitoa matumaini mnasema hapa kazi tu, hapa kazi nini sasa watu hawana mikopo wanafunzi wanalia, mnatoa mtoto kijijini anakwenda chuo anafika pale hana pa kuishi, hakuna mkopo, ni matatizo kwenye familia. Sasa mimi nakutabiria Mpango unakaribia sana kutumbuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye elimu; elimu yetu wakati anazungumza pale Mheshimiwa Mapunda, amesema vitu vinne ambavyo vinahitajika kuwepo kwa viwanda amezungumzia *personnel* au *man power*, ni *man power* ya aina gani ambayo imeelimika ili iweze kuajiriwa kwenye hivyo viwanda?

Leo elimu ni majanga; mama yangu Profesa Ndalichako mimi nilikuwa nakuheshimu sana ukiwa Katibu wa Baraza; umewahi kutoka pale unaonesha watu wamechora ma-zombie kwenye mitihani, wewe umepewa Wizara hii umechora zombie kubwa kuliko wale wanafunzi. Na sijui hata wizi wa mitihani utazuijaye kama wewe Profesa ulitoka hapa kwenda kuiba kura Kinondoni, sijui. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu hivi baada ya wewe kutoka hapo na Uprofesa wako na ni kwa nia njema tu, kwa sababu hili Bunge mmelifanya kama idara fulani ya pale Ikulu labda hata ya umwagiliaji maji pale, kumwagilia maua ndio maana leo Wabunge wanasimama hapa wanasema ukweli hali halisi ya uchumi ni mbaya, wengine wanasimama wanatetea. Jana tu walikuwa wanazungumza hapa wanapiga makofi, sasa hivi wamegeukana na mimi nilijua hamtafika mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchumi ni mbaya hata kwenye kununua vocha tu, ukinunua vocha ulikuwa unapewa GB sita leo ni GB 2.5 kwa shilingi 10,000; yaani hata mtu ambaye hajaenda shule anajua. Kwahiyo, hali ya mazingira ya mtaani elimu inazidi kuporomoka.

Tumetengeneza madawati tumepeleka, maeneo mengine madawati yapo nje yananyeshewa hapa kwenye mpango hamjaonesha mkakati wowote wa kujenga vyumba vya madarasa ili yale madawati tuliyopeleka yaingizwe ndani, yataoza kwenye miti, mwakani tena tuanze kukamatana kupambana na watu wanunue madawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kwenye elimu hapa Profesa Ndalichako ungekuja na mpango ambao utaondoa elimu yetu hii kwenye mkwamo, ambao tutajua kutakuwepo na maandishi yanayoeleweka kwamba elimu tunayoenda nayo ni ya aina hii, tutoke kwenye elimu ile ya akina Mungai ambayo tulikuwa tunaunganisha hesabu sijui na historia na wewe unaendelea huko huko. Leo mnafanya hivi kesho mnafanya hivi, keshokutwa mnatoa vigezo hivi, siku nyingine mnatoa vigezo hivi. Mimi nawaasa vijana Watanzania wote ambao Serikali hii imewatosa haitaki kuwapa mikopo wajue wana nguvu nyingi sana za kuunganisha kura yao ili mwaka 2020 waondoe Serikali hii kwa sababu hakuna matumaini katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda; amezungumza vizuri sana Mheshimiwa Chegeni hilo ndio jina la yule bwana sio sisi tunaosema ni wananchi. Ukikutana naye hapo nje ukamsimamisha Waziri vipi, nikupe kiwanda? Anaingiza mkono mfukoni, anataka kuchomoa kiwanda mfukoni akukabidhi. *(Makofi/Kicheko)*

Mpango wenu hamjajenga kiwanda hata kimoja mpaka sasa, mmebaki mkisikia Bakhresa anataka kufungua kiwanda mnakimbia pale. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa.

### TAARIFA

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimjulishe msemaji anayesema kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano imejenga kiwanda kikubwa sana katika Jimbo la Mkuranga chenye uwekezaji wa zaidi ya shilingi bilioni 200, kiwanda cha *ceramics* kama hataki hata yule anayepita njia ya *Kilwa road* atakuwa ni shahidi, ni Serikali hii ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa juu ya taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, taarifa hiyo Mheshimiwa Heche.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara kaa chini.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Waitara kaa chini, Mheshimiwa Heche endelea.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, rafiki yangu aliyenipa taarifa mimi namfahamu, tumekuwa naye kwenye siasa za vijana, najua anatafuta Uwaziri kupitia taarifa hizo, huwezi kupata Uwaziri kwa njia hiyo. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche, ni kukubali tu umeipokea taarifa hiyo, mengine hayana haja.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sihitaji taarifa hiyo kwasababu ni uongo.

**MWENYEKITI:** Endelea sasa!

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda Mheshimiwa Waziri Mpango wewe unajua, ni msomi na uwe unasikiliza watu hapo unaelewa. Kiwanda ndiyo kinaajiri kuanzia mama lishe mpaka *engineer* kiwandani peke yake. Kwa sababu mama lishe atakuwa pale atawauzia wabeba mizigo wa viwandani, atawauzia madereva wanaobeba mizigo kwenye kiwanda. Kiwanda kitaajiri *engineer* wa kuendesha mitambo, kiwanda kitaajiri mhasibu, kiwanda kitaajiri kila mtu.

Leo umekuja hapa, kwanza ninyi wenyewe Serikali hii ambayo sasa inataka kufuta eti siyo yenyewe, Serikali hii ya CCM ikaua viwanda, ikauza viwanda. Mmerudi mmeimba Serikali ya viwanda, leo tunaelekea mwaka mmoja na siku kadhaa hata kiwanda cha pini hamna mpango nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkisikia Bakhresa anazindua kiwanda chake mnakimbia pale mnasema sukari tuliyokunyang'anya tunakurudishia na shamba tunakupa zawadi. Halafu mnatoka pale kwamba tumefungua kiwanda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa mnakataa hapa kwamba Serikali haijaishiwa kuna taarifa mnatisha wafanyabiashara, mtu amelipa ushuru ana risiti mnamwambia hizo ni risiti fake, Serikali iliyokuwepo ilikuwa inatoa risiti fake. Mnawalipisha watu kodi mara mbili.

Leo Benki zinatangaza hasara, wewe ni msomi utuambie nini *implication* ya benki kutangaza hasara, CRDB wamesema, nini *implication* yake kiuchumi? Maana msituambie tu kwamba uchumi unakuwa vizuri, uchumi unakuwa vizuri watu wanalia mtaani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mmewaruhusu *traffic*, Wabunge walikuwa wanalia hapa kila *traffic* ameambiwa kwamba kwa siku ni lazima apeleke makosa matatu. Leo makosa ya barabarani ni chanzo cha uchumi kwa Serikali ya CCM, aibu. Makosa ambayo yanatakiwa kuzuiwa watu wasifanye makosa ninyi mna-encourage ili mpate uchumi....

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Kuhusu Utaratibu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche kaa chini, utaratibu.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68, lakini Kanuni ya 64(g). Kauli zinazotakiwa kuzungumzwa Bungeni inatakiwa ziwe ni kauli ambazo haziudhi, hazina uchochezi, hazina uchonganishi, lakini pia ziwe ni kauli angalau zinaleta *message* yenye ukweli na uhakika ndani ya Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64 inakataza kabisa kutumia lugha hizo ambazo..., Kanuni ya 64(g) inasema ni lazima Mbunge asitumie lugha ya kuudhi na inayodhalilisha watu wengine. Hapa anazungumzia habari ya *traffic* kwamba wamekuwa wakichukua majukumu ya kukamata watu ili waongeze mapato ya Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha hizi siyo lugha za Kibunge kwanza, lakini ni lugha pia za kuudhi ndani ya Bunge hili, ni lugha ambazo mwisho wake zinapelekea uchochezi ambao hauna maana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, nilikuwa naomba utaratibu uzingatiwe na hasa kwa kuzingatia lugha ambazo zinatumiwa ndani ya Bunge wakati Wabunge wakichangia katika ajenda tuliyanayo hapa mbele yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Heche, anayosema..., Mheshimiwa Heche kaa kwanza. Ni siyo jambo zuri kuzungumza watu ambao hawamo humu ndani na inawezekana vilevile Kiti kikatoa maagizo ulete uthibitisho ambao hutakuwa nao, sasa jielekeze kwenye hoja za msingi za mpango ambao umewasilishwa na Serikali Bungeni. Nakuomba ujielekeze hivyo, ahsante.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba unilinde kidogo muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Leo wakuu wa *traffic* nchi nzima wanatangaza mapato yaliyopatikana kutokana na makosa kwamba mwezi wa tisa tumepata bilioni kadhaa kutokana na makosa, nini maana yake? Kama hamu-*cherish* yale makosa kwamba ni chanzo cha mapato cha Serikali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa yale nafikiri yamewekwa ku-*discourage* watu kuendelea kufanya makosa, lakini unapotangaza unajisifu kwamba ma-*traffic* wamekamata makosa kadhaa ina maana ni chanzo mmeweka pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema siyo kwa nia mbaya ni kwa ajili ya kuwaambia hawa watu wasikie waelewe kwamba waliambiwa hapa tukikosa mapato yanayotokana na bandari mtaanza kufukuzana na bodaboda, watu walisema humu mkatuzomea. Sasa leo tunaposema haya hamtaki tena, mnataka tukae wapi? Tukisema hili ninyi kwenu baya, tukija hapa ninyi kwenu baya mnataka nini sasa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwaambia mkipoteza mizigo nchi hii haitawezekana. Leo eti TRA wanataka wawe TRA ya Congo pia wamesema Wabunge wengine hapa, yaani mnataka kujipa majukumu ya kukusanyia Congo kodi. Kwani kama Congo kule wanakwepa kodi ninyi inawahusu nini? Wamepitisha hapa, wamewalipa mapato yenu, mnachukua mnaanyiakazi, mnataka kuwakusanyia Congo ili wawape nini? Mmekuja hapa mnaongea na Rais wa Congo anawahakikishia mizigo itaongezeka, imeongezeka? Kwa sababu hana *mandate* ya kuwaambia wafanyabiashara lazima wapitie hapa na wao wamehamia Beira, wamehamia Mombasa sasa wote tunapiga miayo hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunadanganyana tumepandisha bajeti kutoka shilingi trilioni 22 *desperately* kabisa kwenda shilingi trilioni 29 eti mnataka hadi Mama Lishe alipe kodi, Mheshimiwa Mpango, mama lishe alipe kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana mnawaambia hawana ajira eti wajijiri, wewe mwenyewe umeshindwa kujijiri umeomba Ubunge hapa unataka kijana wa mtaani ajijiri. Wabunge wote hawa tumeshindwa kujijiri tukaenda kuomba ajira kwa wananchi, wengine Profesa sijui na nini. Kijana aliyemaliza mwaka wa kwanza mnamwambia nenda ujijiri kule! Vijana hawawezi kutengeneza ajira! (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la Serikali yoyote duniani kulinda watu wake na ni aibu kwamba leo nchi hii wakati wa hapa kazi tu hakuna madawa kwenye mahospitali; miradi yote mliyoweka ya kielelezo haiendi, barabara hamtengenezi tena na wengine hapa walikuwa wanaitukana Serikali ya... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lulida, ajiandae Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na niwaombe Mwenyezi Mungu vilevile awajalie Wabunge wenzangu wapate afya njema tuweze kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanzia na mazao mchanganyiko hasa katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani. Watu wa Mikoa ya Kusini walikuwa wanategemea mazao mchanganyiko kama ufuta, korosho, kunde na mbaazi. Katika nchi hii ya Tanzania tuligawanyika katika baadhi ya mazao yanayotokana na maeneo fulani, nasikitika sana tuliwaacha wafanyabiashara wachache wanaiyumbisha nchi kwa kununua mazao kwa bei ya chini na kuwafanya wananchi kuwa maskini. Tujiulize wataendelea wao kujitangaza matajiri mpaka lini, wananchi wa Kusini na Watanzania wanaendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, leo katika soko la Euro wanauza ufuta kilo moja euro tatu na wafanyabiashara hawa wanachukua ufuta Lindi, Mtwara, Pwani wanaupeleka Sri Lanka, ina maana ajira inakwenda Sri Lanka. Tunawaona hatuwaoni? Lakini tumenyamaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshindwa kutafuta soko kwa wananchi kuweza kuwakwamua leo ufuta kutoka 3,500 wananunua ufuta kwa shilingi 600 mpaka shilingi 800 na wengine upo majumbani hawana pa kuupeleka kwa ajili ya hawa wafanyabiashara wanaiyumbisha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize kwa miaka 50 kwa nini tumeachia uchumi wetu unachezewa na kukanyagwa kanyagwa na watu wachache. Ni hali ambayo imetufanya wananchi wamedhoofika, wananchi wamekuwa maskini kwa kuwa wafanyabiashara wanajiona wanakuwa matajiri na kuwaacha wananchi wanaendelea kuwa wanyonge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaazi zipo majumbani kutoka shilingi 3,800 mpaka shilingi 800 hazitoki, kunde, njugu na choroko zipo majumbani wao wameukamata uchumi na uchumi huo wameukamata kwa vile wana mahali wanapoegemea, wajjulize kwa nini wanaendelea kuikandamiza nchi ya Tanzania na Watanzania wenyewe wenye ngozi nyeusi wakiwa maskini, tujiulize tunajitambua Watanzania? Hatujitambui. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda muafaka kila Mtanzania humu ndani ajione kuwa yeye ni *part and parcel* ya kutetea wanyonge wa Tanzania. Watanzania wanadhaliika, mama lishe anakimbizwa Tanzania nzima kwa ajili ya kuambiwa atoe kodi lakini kuna ma-*giant* hawalipi kodi. Wanatufanya Watanzania kama *sleeping giant* ambapo wao hawatozwi kodi na wameamua kulindwa, Serikali kama inataka kusema kweli iwashughulikie hawa watu, haina haja ya kuwasema humu ndani mnawatambua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi, Mtwara na Pwani tulikuwa na viwanda vya korosho 13 vyote havifanyi kazi. Lindi peke yake haina ajira ya vijana hata moja kwa vile viwanda vyote vimefungwa. Je, tutawapelekaje vijana wale ambao hawana ajira watafanya kazi gani, wamelima ufuta, wamechukua mikopo benki, lakini leo ule ufuta uko majumbani. Hao vijana tunawapeleka wapi?

Tunataka tuhakikishe uchumi wetu utakwenda wapi, watoto watasomaje katika mfumo ambao unaona kabisa ni kandamizi wao wanatangaza mimi nitakuwa tajiri wa dunia, halafu hawa watu wa chini wanakwenda wapi? Ni kitu cha aibu, inabidi Watanzania tujiulize tutaendelea kuwalinda mpaka lini? Mimi na wewe wote tunataka tuangalie wananchi wanyonge wanapata haki yao, haki sawa kwa wote na asiependa haki aelimishwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Serikali imesahau uwekezaji hasa katika mablenki, yameingia mablenki mengi utitiri, riba zinatofautiana lakini anayekandamizwa mwalimu, daktari, mbunge, nesi na watu ambao wanachukuwa mikopo katika mablenki. Wao wanategemea taasisi zetu kuenda kuweka *fixed deposit* katika mablenki yao, mikataba wanayowekeana ni kutoka asilimia nne mpaka nane lakini leo mablenki wanatutoza riba ya asilimia 18.5 na kuendelea. Je, mwalimu wa kawaida ataweza kudumu au ataweza kumudu uchumi wa namna hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize kwa nini wanaweka riba kubwa jibu halipatikani. Leo kila mwezi wanakukata kodi, unakatwa kodi katika mshahara, unakwenda benki unakatwa kodi na bado unaendelea kuweka riba kubwa mara mia tatu mpaka mara mia nne tunasema nini humu ndani kuhusu watu hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki ni mwiba, leo ndani ya benki tunasikia lakini hakuna anayeguswa kwa vile ndani mle hakuna Lugumi wala hamna UDA. Lakini angekuwepo UDA humu ndani mngesikia kelele Bunge zima humu ndani. Wanatuibia vya kutisha, ukiweka pesa benki ukikaa mwaka mmoja haujaigusa akaunti yako hamna pesa mle ndani ya benki, tunafanya nini na riba chafu kama hizi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata katika Qurani wamesema riba ni haramu, lakini tunaona kabisa riba ni kubwa na zinawakandamiza Watanzania hatuangalii ndio maana wanajiuliza kwa nini sasa hivi wanaanza kupata woga, wanapata woga kwa vile walizoea kufanya wizi wa kukithiri ndani ya mabenki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki zetu zimekuwa siyo rafiki kwa Watanzania, anakopa Mtanzania anawekewa riba kubwa ambayo anashindwa hata kuimudu, ndiyo maana leo hata akina mama lishe wakikopa pesa benki ananyang'anywa vitanda vyake, magodoro yake maana yake wao wanaweka vitu vya vidogo vidogo kutokana na uwezo wao.

Naiomba Serikali iingalie hii riba katika mabenki ni wizi wa aina yake. Na kwa nini sasa hivi wanajaribu kukimbiakimbia kusema wanataka kufunga, huu ni uongo! Watu wa benki wamecheza michezo michafu kwa muda mrefu sasa hivi wanajaribu kusimamiwa ndiyo maana wanasema tunafunga benki, lakini hawafungi benki ni kwa ajili ya wizi waliouona ni mkubwa ambao unawakandamiza Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaingia sasa hivi katika mbunga yetu ya wanyama ya *Selous Game Reserve* sitaki kuangalia sehemu nyingine yoyote. Nimeizungumzia hii mbuga zaidi ya miaka kumi ndani ya Bunge hili. *Selous Game Reserve* ni mbunga ya kwanza kwa ukubwa duniani, lakini ndani ya *Selous* sasa hivi watu wanachimba madini. Tunachimba uranium, wanachimba dhahabu, wanachimba almasi sisi wenyewe tupo hapa humu ndani? Nani atatuletea ufafanuzi kuwa ndani ya *Selous* kunafanyika nini? Hakuna kinachojulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wameifanya *Selous* kama shamba la bibi, mapato ya *Selous* tungeweze kuhakikisha yanawasaidia Watanzania wengi na wanyonge wakafaidika hata na ajira. Lakini ndani ya *Selous* sasa hivi hakuna kinachoendelea zaidi ya kuchimba madini mengi yako mle ndani, kuhakikisha msitu wote unakwisha, wanyama waliokuwa ndani ya *Selous* wamekwisha. Je, tunakwenda wapi na uchumi wetu? Tufike mahali tujiulize Tanzania, hivi kweli tunaitakia mema nchi hii?



Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wachache ambao wanaingalia Tanzania kwa huruma, watu wengi hawataki kuangalia kwa huruma na ndiyo maana mpaka leo meno ya tembo yanauzwa na tunayaacha hivi tunaangaliana. Kila siku tunaangalia meno yanaondoka, kutakuwa na tembo nchi hii, kutakuwa na utalii nchi hii? Na utalii peke yake unatuingizia 27.5 percent, lakini unaona Selous imetupwa haina ajira haina kazi wala kinachofanyika ndani ya Selous; haiwezekani hali imefikia mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kuangalia hali tete inayohusu mazao. Tufike mahali tuwaonee huruma wananchi, wakulima wanalima, mpaka leo mazao yao yamekaa ndani hawajui yatayauza wapi? Leo ufuta kutoka shilingi ngapi wamekaa nao ndani mpaka shilingi 800 hakuna soko la ufuta. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshindwa kutafuta soko la ufuta, tumefika mahali wananchi tumewakandamiza hata pa kupita hawajui, wamekaa wamechanganiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahali, Serikali iangalie kwa makini mabenki na wakulima wanaokopa katika mabenki wanadhurumika vibaya mno. Mabenki yanaweka riba kubwa na ndiyo maana sasa hivi wanajidai ooh tumefilisika, hawajafilisika hawa, wanabadilisha majina tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili kuweza kuzungumzia mpango wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetulinda ametuleta tena kwa mara nyingine mahali hapa, tunaendelea kuomba neema yake na rehema yake atulinde mpaka tumalize Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya kwa ajili ya kupigania nchi yetu na maslahi ya Taifa zima. Naomba nipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri ambazo kwa muda mfupi kwa muda wa mwaka mmoja wameweza kuzifanya.

Leo hii naomba nimpongeze Rais wangu kwa kazi nzuri na maamuzi magumu ambayo ameyafanya kuhamia Dodoma, leo hii Serikali inahamia Dodoma ni mafanikio makubwa kwa sababu ilikuwa inazungumzwa kwa muda mrefu na miaka mingi leo Awamu ya Tano imeweza kufanya leo hii Serikali imehamia Dodoma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba niipongeze Serikali, ingawa bado pesa hizi hazijatoka za kwenda kila kijiji shilingi bilioni 59.5, tuna mategemeo Serikali hii ya Awamu hii ya Tano hizo hela zitafika kwa wananchi wetu kwa ajili ya uchumi wa Tanzania hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kununua ndege mbili mpya. Leo hii tunajivunia Serikali ina ndege, alama yetu ya twiga ipo ilikuwa haipo lakini leo sasa ipo kutokana na malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano yameendelea kuwa mazuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite sana kwenye masuala ya dawa. Ninaomba sasa Waziri wetu aweke mpango mkakati wa ujumla ili wananchi wetu waweze kupata dawa. Dawa ni kitu muhimu sana kwa wananchi wetu wa Tanzania. Ninaomba mikakati mikubwa ichukuliwe sasa hivi, ufanywe mkakati maalum kwa ajili ya dawa ili hospitali zote zipate dawa. Ninajua Serikali ya Awamu ya Tano ni sikivu, mipango inayopanga sasa iweke mikakati ili tuweze kupata dawa kwa ajili ya wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; lazima sasa tufanye mikakati ya kujenga vituo vya afya kila Kata ili wananchi wetu waweze kupata huduma za ukaribu. Tukiweka mipango mizuri na mikakati mizuri kila Kata iwe na kituo cha afya akina mama wengi wataende kufanyiwa *operation* ndani ya kata zetu na maeneo yetu husika, hiyo mipango iweze kupangwa. Mimi najua Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, mipango yote tunayomweleza Waziri wetu ataifanya na ataitenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la maji; bado maji hatujawafikia wananchi vizuri husasan maji mijini bado kuna maeneo ambayo maji hayajawafikia wananchi vilevile maeneo ya vijijini, lazima sasa hivi tuamue kuweka mipango mikakati.

Kuna Mbunge hapa amezungumza kama sisi tunapakana na maziwa, mfano Ziwa Tanganyika li-supply Mkoa wa Katavi inawezekana, kwa sababu kuna mipango iliyopangwa nyuma. Leo hii Mwanza, Shinyanga wanapata maji kutoka Ziwa Victoria, tunaomba na sisi tunaokaa Katavi, Mkoa wa Rukwa na maeneo mengine kama Kigoma yale maziwa yetu yaweze kunufaisha maeneo husika, vijijini pamoja na mijini, mpango ukikaa vizuri nafikiri tutaweza kufanikiwa vizuri sana upande wa maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu; ninaomba mipango mizuri ifanyike kwenye elimu. Tunajua Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi nzuri ya kutafuta madawati, leo hii tuna madawati mengi. Vilevile kutokana na Serikali ya Awamu ya Tano imefanya elimu imekuwa bure, kutokana na elimu bure sasa hivi wanafunzi tumekuwa nao wengi ndani ya shule zetu. Sasa tunaomba Serikali ipange mpango makakati wa kujenga madarasa ili watoto wote waweze kuenea ndani ya madarasa. Kwa sababu madawati, mpango umekwenda vizuri hakuna sehemu sasa hivi watu wanalalamika kuwa mtoto anaka chini, tunaomba bajeti hii inayokuja tuweke mikakati ya kujenga madarasa nchi nzima ili watoto wetu wote waweze kukaa madarasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa ardhi; leo hii tunawaleta wawekezaji, lakini kuna matatizo kidogo ndani ya maeneo yetu husika. Leo hii migogoro ya ardhi kati ya wawekezaji na wananchi imekuwa mikubwa mno. Ninaomba Serikali sasa kwa sababu tuna lengo zuri la kuweka mikakati mizuri ya wawekezaji nchini na vilevile tunaendelea kuwaleta wawekezaji ndani ya nchi yetu, kwenye upande wa ardhi tujipange vizuri na Watanzania tumeongezeka, lazima sasa hivi Serikali ipange mikakati ya kuongeza ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu nyingine tumeweka mipaka, mipaka ile tuipanue ili wananchi sasa pamoja na wawekezaji wakae sehemu nzuri. Wawekezaji wengine wanatukimbia kutokana na migongano kati yao na wananchi. Ninaomba Serikali iweke mipango mizuri, mikakati mizuri ili wananchi na wawekezaji waweze kukaa vizuri na waweze kujenga viwanda vyao ndani ya nchi yetu ili vijana wetu wapate ajira, mama lishe zetu wale wanaohangaika waweze kupata ajira kwa ajili ya mipango mizuri ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mikopo ya akina mama. Akina mama wengi bado hatujawafikia kwa elimu. Tunapenda akina mama wapate mikopo, tunapenda akina mama waweze kuinuka, lakini bado hatujawafikia ili waweze kupata elimu nzuri waweze kutumia hayo mabenki tunayoyasemea leo hii mambo yamekuwa siyo mazuri, akina mama tukiwafikia tukiwapa elimu nzuri wakiweza kujikomboa wao kama wao, tukiwawekea mikakati mizuri ninafikiri Taifa hili ukimwezesha mwanamke, tumewezesha jamii nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kilimo; bado Watanzania tunalima asilimia 80 ni wakulima, asilimia 20 ni wafanyakazi. Mpaka leo hapa tulipo wananchi kule hawajapata mbolea na hili lazima tuliwekee mikakati mikubwa na mipana ili kipindi cha mvua kabla hakijafika wananchi hawa waweze kupata mbolea kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katikati tulikuwa tuna mawakala, leo hii hiyo mipango ya mawakala tumeitoa na wale mawakala ambao tuliowatoa bado hatujawalipa wanatudai na mpaka sasa hivi hatuna mawakala wala hatuna nini, wananchi wameilewa. Hatujui hiyo mbolea itauzwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ichukue jukumu ambalo sasa kupanga mikakati mizuri na mipango mizuri ili wananchi waweze kupata manufaa kupitia Serikali yao kwa ajili ya kilimo kwa sababu upande wa kilimo ndiyo uwekezaji upo mkubwa sana kuliko upande mwingine, ninaomba Serikali hii sikivu mipango hiyo iweze kupangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepanga mipango mingi, tunaongea mipango mingi, lakini kuna watu ambao ni muhimu sana ambao tukiwajengea uwezo na tukiwafanyia mipango mizuri, mikakati mizuri wanaweza wakakaa vizuri zaidi. Hapa mara nyingi tunawasahau sana askari wetu na sehemu nyingi ukienda unakuta askari hawana sehemu ya kuishi, lazima sasa Serikali ichukue jukumu la kuweka mpango mkakati wa kuwajengea askari nchi nzima ili hawa askari wanaotulinda wananchi wawe na sehemu nzuri za kukaa ili nchi yetu iweze kuwa na amani na utulivu kama tulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima sasa tuwawekee mikakati mizuri na mipana ili kila sehemu nchi nzima, nyumba za askari, nyumba za manesi, nyumba za walimu ziweze kuwekewa mikakati mikubwa na mipana zaidi ili sasa nchi yetu iweze kutulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utalii, kwetu Mpanda nilishasema kipindi kilichopita tumejengewa uwanja mzuri. Naomba nirudie kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambayo ilifanyika kununua ndege mbili. Ninajua sasa uchumi wa Tanzania na uchumi wa Mkoa wangu wa Katavi utazidi kuongezeka, ninajua sasa ndege itatua Mpanda, Katavi kwa ajili ya kuleta watalii ili uchumi wa Katavi uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninaomba niunge mkono asilimia mia kwa ajili ya mpango huu mzuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Waheshimiwa Wabunge tumebakiwa na dakika sita na ninalirudisha Bunge tena, tutaendelea jioni, Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae!

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kutakuwa na kikao cha caucus leo saa tisa kwenye Ukumbi wa Msekwa, hudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wa mchana ni Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Godbless Lema.

Waheshimiwa Wabunge, ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.57 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Kwa vile Serikali ipo tunaendelea, Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018**

*(Majadiliano yanaendelea)*

#### **KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Kamati ya Mipango. Tulitaja majina ya Waheshimiwa watakaoanza kuchangia jioni na tutaanza na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MBUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango ambayo yamewasilishwa leo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Nishukuru Mpango umeeleza mambo mengi na umejikita kwenye mambo mengi makubwa zaidi. Inawezekana yakawa size ya uwezo wetu kama nchi au yakawa zaidi ya uwezo wetu kama nchi kwa sababu *projections* zilizopo kwenye Mpango huu ni kubwa kiasi fulani.

Mimi nataka kujikita zaidi katika kutoa ushauri ushauri kuhusiana na mwelekeo mzima wa huu Mpango ulivyo na mbele tunakokwenda. Mchango wangu zaidi utajielekeza kwanza kwenye sekta ya kilimo, lakini na uanzishaji wa viwanda kwa bidhaa zinazotokana na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu ulitakiwa zaidi uoneshe mwelekeo sahihi kwenye kilimo na hasa kwenye uzalishaji ili tuweze kupata dira na mwelekeo wa kuelekea kwenye viwanda. Tunajua kwamba kutakujakuwa na udadavuaji wa baadhi ya mambo lakini kwa hivi ilivyoelezwa ndani ya huu Mpango iko *too brief* na hapa ndipo penye roho ya uchumi na maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza katika hili, mpango haujaeleza mkakati mzima wa udhibiti na uendelezaji wa maeneo yale ambayo mazingira yake yameathirika. Miaka kumi iliyopita Tanzania ilikuwa zaidi inategemea mikoa minne kwa upatikanaji wa mvua ya uhakika, lakini sasa hivi hiyo mikoa minne tuliyokuwa tunasema ina mvua ya uhakika imeshapoteza mwelekeo. Tulikuwa tunaiangalia zaidi Kigoma, Kagera, Katavi, Njombe pamoja na Iringa. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa maeneo haya yamekumbwa na uharibifu wa mazingira na unapoweka mpango kama huu ambao unataka kutengeneza mazingira ya uzalishaji, vitu hivi lazima viwe na mtazamo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yetu tumeyaharibu, tukiangalia eneo kubwa tulilokuwa tunalitegemea, tunaliita eneo chepe la mabonde ya Usangu mpaka Ruaha leo hii imekuwa ni mbuga ya kufugia ng'ombe tu. Hata tukienda maeneo yale ya Kagera, Karagwe, Misenyi na Biharamulo nayo vilevile tumeyaachia huru *as if* nchi yetu haina mpango mkakati wa udhibiti wa uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo langu, turudi kwenye kuweka mkakati maalum wa udhibiti wa uharibifu wa mazingira katika maeneo hayo ili kurudisha uoto wa asili na hali nzuri ya unyeshaji wa mvua katika maeneo yale. Sambamba na hilo, ule mkakati uliokuwa umeanzishwa Dar es Salaam wa upandaji miti, tunarudia tena, uweze kusambaa nchi nzima kuwe na mkakati kama ule vinginevyo hatma ya nchi hii ndani ya miaka kumi tutakuwa kwenye mtihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, ni lazima nchi iwe na mkakati wa kuhakikisha kwamba kunakuwa na uzalishaji. Kwa kipindi hiki sasa mkakati mkubwa uelekezwe kwenye umwagiliaji maji. Bado mpango haujaonesha kiwaziwazi mkakati wetu wa ujengaji ama mabwawa au miundombinu yoyote ya umwagiliaji maji kwa kutumia rasilimali ya mito na maziwa tuliyonayo hapa nchini. Tanzania tumejaliwa, lakini mpaka tunajuliza sijui tumerogwa wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano tuliokuwa nao sisi wengine tuliopata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya nchi za wenzetu, mwezi uliokwisha kulikuwa na kikao cha wataalam wa kilimo cha SADC pale Angola, Wamisiri walikuja kutoa taarifa na uzoefu wao tu, kwa kutumia maji ya Mto Nile, ile *Suez Canal*, wenyewe wanaita *Suez Belt*, wana uwezo wa kuzalisha pamba tani milioni tano kwa miaka miwili. Sisi tuna Ziwa Victoria lakini uzalishaji wetu kwa Kanda ya Ziwa ambayo ndiyo maarufu kwa ajili ya uzalishaji wa pamba tunasuasua kwenye tani 300,000, wenzetu wanazungumzia kuongeza kutoka milioni tano kwenda kwenye milioni nane sisi tunaangalia 300,000 tutai-maintain vipi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ili uwe *smart* uangalie *raw material* zinazotokana na uzalishaji wa mazao mbalimbali ya kilimo. Hata hivyo, mwelekeo wetu uwe kwenye *irrigation* ili na sisi kama wananchi tupate fursa ya kutumia maji na mito ambayo ipo ndani ya maeneo yetu, kitu ambacho bado hakijatendeka vilivyo. Maji tunayo yanaishia baharini kama wengi walivyosema. Nikuombe Mheshimiwa Waziri tukafanye *restructuring* kwa baadhi ya mambo tuelekeze nguvu kwenye umwagiliaji maji ndipo tutakapokomboka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ni usalama wa chakula, tuwe na mipango ambayo itatuwezesha kuwa na uhakika wa usalama wa chakula hapa nchini. Kwa kweli bado na mimi nasema ni aibu nchi hii kulalamika njaa wakati fursa za vyanzo vya maji tulivyonavyo ni nyingi sana lakini bado hatujajiweka sawa, mipango yetu haijajielekeza kuhakikisha kwamba watu hawa wanalima kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mmoja, kama tutaweza kujenga mabwawa yakawa yanatumika kwa kilimo na mifugo, tukaweza kuendeleza hekta 50 tu kila Mkoa kwa yale maeneo yenye uwezekano wa kutengeneza yale mabwawa tuna uhakika wa *reserve* ya tani 500,000 kila mkoa kwa kila mwaka. Hii ni akiba nzuri lakini hiki ni chanzo cha *raw material* ya viwanda ambavyo tunategemea tuvianzishe na maeneo mengine yatumike kwa ajili ya chakula na mambo mengine. Tuwe na mkakati na muono wa mbele wa kuona kwamba nchi inakuwa na uhakika wa ile *reserve* iliyokuwa tunaisema tu lakini kuweka *reserve* ya chakula kwa kutegemea mvua ambazo hazina uhakika bado hatujaenda vizuri na hatujawa *stable*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri tuzingatie kuyafanyia marekebisho baadhi ya mambo, mtuite tuwape mawazo ambayo yataweza kutujenga. Kinachotia uchungu ni kwamba tunatumika katika nchi za wenzetu kutoa mawazo ambayo wao wanayafanyia kazi na wanaweza kupiga hatua.

**MBUNGE FULANI:** Hakika.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea mwezi uliokwisha, wenzetu wa Malawi baada ya kupata tatizo kubwa la ukame mtazamo wao sasa hivi ni huo. Haya maelezo ambayo mmeyatoa hapa katika *page number 16* ya mpango tuliokuwa nayo ni mkakati ambao *EU* kwenye *agricultural sector* ndiyo waliokuwa nao, *AU* ndiyo waliokuwa nao na *SADC* wame-copy and paste huohuo.

Kwa hiyo na sisi tusiwe tunauweka kimaandishi, tuweke kivitendo uwe *practical* na siyo tunachukua mipango kama hii na maelekezo ambayo wenzetu wameyaweka sisi kwetu baadaye yanaishia kwenye *shelf*. Nimuombe sana, tusipozingatia na tukaelekeza nguvu zetu kwenye kilimo tumewamaliza Watanzania na tutakuwa na ndoto tu ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mpango bado haujatuambia kwenye uvuvi tunafanya nini. Tumepata maelezo na baadhi ya watu wameeleza lakini katika eneo kubwa ambalo tutaweza kuajiri watu wengi kabisa ni sekta ya uvuvi. Tukijipanga vizuri katika eneo hili, wenzetu wametoa mawazo pale kwamba tutafute angalau meli moja tu ya uvuvi ina uwezo wa kutuanzishia viwanda viwili lakini ina uwezo wa kutoa ajira kwa watu mpaka 3,000. Kwa sababu kazi zilizopo kupitia sekta ya uvuvi ni nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutengeneze mazingira ya pale bandarini kuwepo na *port dock* ambayo itawalazimisha wale wanaovua katika maeneo mengine yote ile kuchakata wale samaki na *process* nyingine zifanyike katika maeneo yetu, tutatengeneza pesa ya kutosha. Taarifa zilizopo sasa hivi duniani, Tanzania baada ya kuzuia leseni za uvuvi katika uvuvi wa bahari kuu, *demand* ya samaki katika soko la dunia imepanda mpaka tani 230,000, soko lipo wazi, nafasi hii ndiyo pekee ya kuitumia. Nimuombe Waziri wetu wa Kilimo azuie kutoa vibali vya uvuvi wa bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaofuatilia haya mambo na tunayajua, ukiikodi meli moja ya uvuvi Philippines au Thailand wanakodi kati ya dola milioni tano mpaka milioni saba, *catchment* yake kwa wiki tatu mpaka miezi miwili ina thamani ya dola milioni 40.

Kwa hiyo, kwa wale wanaokodi, kwa wenzetu wanafanya *deal* kwamba akikodi meli mara moja harudi tena baharini kapata utajiri wa maisha anafanya mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utafiti unavyoonesha samaki wale wengi wanawatoa katika maeneo yetu na wakija katika maeneo yetu haya hawavui jodari tu peke yake, wanavua kamba, pweza, ngisi na samaki mbalimbali na baadaye wanakwenda kufanya uchambuzi katika maeneo yao sisi tunabaki



kama tulivyo. Ile ni bahati, ni riziki Mungu katupa tujipange vizuri tuitumie vizuri ilete manufaa katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linajieleza hapo, tutakapoweza kuwa na eneo la kuweza kushusha samaki, tukaweza kuanzisha maeneo ya majenereta ya kuhifadhia vizuri samaki, tutaweza kuongeza ajira kubwa kwa sababu wenzetu Ulaya wanachotaka ni minofu. Hivi sasa biashara kubwa iliyojitokeza maeneo ya Kongo ambao wanakuja kuchukua dagaa kwa wingi sana Zanzibar, Mwanza na Kigoma wanakwenda kutengeneza *raw material* ambayo wanapeleka Ulaya kama ni *fish meal*, *demand* yake sasa hivi ndani ya soko la dunia kubwa. Sisi tukiwa na meli hiyo pale zile *by products* zilizotokana na kutoa zile nyama za samaki tunatengeneza *fish meal* kwa kiwango kikubwa sana ambapo soko ndani ya eneo la soko la dunia ni kubwa sana. Fursa nyingine ni hizo, pale hutupi kitu, hata ule mwiba wa katikati wa samaki bado ni bidhaa adimu kabisa kwa sababu ile *calcium* iliyomo mle ni bora zaidi na inahitajika katika maeneo mengi sana kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali na dawa.

Kwa hiyo, mimi wito wangu na wazo langu ni kuiambia Serikali hili eneo la uvuvi lina fursa kubwa sana, kuliko kuwaita Wachina kuja kuweka soko pale la bidhaa zao mbalimbali, hapa pana pesa za waziwazi, tujikite jamani katika maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kuzungumza ni kwenye mazao ya biashara bado kama nchi tunaendeleza ukiritimba fulani hivi ambao hauleti maana. Leo hii kutengeneza *rustan coffee* mpaka twende Moshi, Arusha? Gharama za kuchukua kahawa iliyoko Mbinga ambapo kule tunafanya *process* ya mwanzo tu ya *catchment* uisafirisha uipeleke Moshi ni kubwa. Wakati mwingine unachukua kahawa kutoka Manyovu au Kigoma iende Moshi, *very unfair!* Tutengeneze viwanda ambavyo tutaweza kutengeneza kahawa ambayo itaweza kwenda kuuzwa katika soko la nje moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa yetu ni ya nne duniani, bado tuna nafasi kubwa. Kwa ubora hatujawapita Ethiopia, Rwanda lakini tumewapita Uganda, Burundi na Kenya. Kahawa yetu ni bora kuliko ya Brazil, bado tuna nafasi katika soko la dunia. Hata hivyo, utaratibu wa makampuni yanayoshughulika na zao la kahawa ni wa kujitengenezea faida wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi hiyohiyo ipo kwenye tumbaku. Tumbaku kilichotokea pale ni ukiritimba tu wa yale makampuni ya kujifanya wao ndiyo wao wakati bado kuna fursa kubwa ya ile tumbaku katika soko la dunia. Mnunuzi mkubwa wa tumbaku ni China. Sasa hivi China baada ya kuona *bureaucracy* ya Afrika anatenga hekta karibu milioni mbili azalishe tumbaku

nchini mwake, lakini mbegu ya tumbaku kutoka China sisi tunayo hapa. Sasa lile fishio la yale makampuni la kusema kwamba sisi hatununui wanasema wanatisha bwege ni ili sisi tuweze kujiachia hawanunui tupunguze uzalishaji ili wao ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mheshimiwa Maige, ajiandae Mheshimiwa Lema.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jambo langu la kwanza, naomba nikumbushie siku nachangia bajeti hii ya Wizara ya Fedha nilisema tukikubali mipango hii ya Mheshimiwa Mpango, tutauza hadi Ikulu, tumeyaona leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tumechangia, Mheshimiwa Waziri ametuelewa na hii ndiyo mara yake ya kwanza sasa hivi ana miezi minane tu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba tumpe nafasi, Waziri atajirekebisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba nichangie masuala yanayoendelea sasa hivi kwa upande wa wafanyabiashara. Wafanyabiashara wetu sasa hivi hatuwapi nafasi, wanapotoa ushauri Serikalini, Serikali inawapa nafasi finyu ya kuwasikiliza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba ukitoka hapa kakae na wafanyabiashara wetu. Mimi nina uhakika tukisikiliza maoni yao tutafika mbali. Haya yaliyotokea sasa hivi hayatatokea tena, ni masuala madogo tu ya kukaa na kuyarekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la tatu, katika Jimbo langu la Ulanga kuna migodi mikubwa ambayo inatarajiwa ianze, kwa kiasi kikubwa italisaidia Taifa letu katika kuchangia uchumi. Hata hivyo, wananchi wa kule hawasilizwi na kusababisha miradi hii kuchelewa kuanza ambapo ingechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Kwa hiyo, naomba Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu upo naomba uje Ulanga utusikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, katika Wilaya yangu ya Ulanga tunalima mazao mengi ikiwemo mpunga zao ambalo kwa kiasi kikubwa linachangia uchumi wa Taifa letu. Leo hii Wizara ya Maliasili inapanga kwenda kuwanyang'anya wananchi wa kule ardhi ambayo ingechangia kwa kiasi kikubwa mapato ya Wilaya ya Ulanga. Rais alipokuja aliahidi lile eneo watawaachia wananchi ili waweze kulima na kuchangia mapato ya Taifa hili.

Endapo tutawanyang'anya wananchi eneo lile nakuhakikishia robo tatu ya mapato ya Ulanga na Malinyi yatashuka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba suala hilo ulitazame katika jicho la pekee. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano, jana kuna kiongozi mmoja alinishangaza sana, aliuliza Serikali ya CCM itatumia miujiza gani kutekeleza ahadi zake. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tanzania kuwa Serikali ya CCM haitumii miujiza inatekeleza ilani yake kwa mipango na mikakati na itafanikisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namshangaa, kwanza ajiulize yeye huyo kiongozi *form six* amepata *division zero*, lakini huyo huyo ana miujiza ya kuwaongoza wanasheria maarufu kama akina Tundu Lissu wakatulia, ana uwezo wa kuongoza madaktari wenye *Ph.D* na wakatulia. Kwa hiyo, sisi hatutumii miujiza tunatumia taratibu, kanuni na uadilifu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la sita, kumekuwepo na sintofahamu Wakuu wetu wa Wilaya, Wakuu wetu wa Mikoa kutumia sheria ya kuwaweka ndani wafanyakazi wenzao kama Madiwani na watendaji wengine kama Wakurugenzi wa Halmashauri, kile kitendo cha kuwaweka saa 24. Wakuu wa Wilaya wametumia ile kama silaha yao ya kuwakandamiza viongozi kwa ajili ya kuwalipizia visasi. Kwa mfano, kila siku tunasikia Mkuu wa Wilaya amemweka ndani Mkurugenzi, kila siku Mkuu wa Wilaya amemweka ndani Diwani, vile vitu vinadhoofisha maendeleo ya nchi yetu. Watu wamekuwa hawafanyi kazi kwa juhudi zote, wanafanya kazi kwa uoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie hapo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Maige, ajiandae Mheshimiwa Lema.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutuwasilishia Mpango ambao sisi kama Wabunge tuna wajibu wa Kikatiba wa kutoa maoni yetu ili kuuboresha ili uweze kuwa na manufaa makubwa kwa wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Mpango ni mzuri sana na kwa kweli nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu yako baadhi ya maeneo ambayo tumekuwa tukiyazungumza sana ameyataja japo si kwa kiwango kikubwa ambacho tungetarajia lakini walau yamezungumzwa. Mojawapo ni suala la uboreshaji na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kwenye Bunge lililopita tulizungumza sana eneo hili, tulikasirishana sana na moja ya eneo tulilokuwa na wasiwasi ni ujenzi wa reli hii kwa kiwango cha *standard gauge* kwenye matawi yake yote. Nashukuru kwenye Mpango liko wazi, matawi yote yametajwa Kaliua - Mpanda - Karema - Uvinza - Msongati - Isaka - Keza na sehemu zingine. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, eneo hili ni la muhimu sana, tunakubaliana na yeye na yako maeneo mengi ambayo tunakubaliana. Naamini kwamba tukienda kutekeleza matokeo makubwa tutayapata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama taratibu zinavyotaka nifanye, naomba nizungumzie baadhi ya maeneo ambayo naamini yanaweza yakasaidia zaidi kufanya Mpango uweze kuwa na manufaa makubwa kwa wananchi lakini lengo kuu likiwa ni kutusaidia katika kufikisha au kutekeleza ahadi tulizozitoa. Kwenye kitabu cha Mapendekezo ya Mpango ukurasa wa 62 Mheshimiwa Waziri ameeleza maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2017/2018. Kwenye maeneo hayo yako baadhi ya maeneo ambayo mimi naamini yalitakiwa yaingizwe na yangepaa yatizamwe kwa upana mkubwa sana. Eneo moja ambalo mimi naona halijaelezwa kwa upana unaostahili ni mchango wa sekta ya kilimo kwa upana wake kama *engine ya raw material* inayotakiwa kwa ajili ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba hauwezi ukajenga viwanda bila malighafi na asilimia zaidi ya 80 ya malighafi zinazohitajika kwenye viwanda zinatoka kwenye sekta ya kilimo. Ili kweli kupata uchumi wa viwanda ni lazima tuangalie maeneo ya sekta ya kilimo na hasa mazao ambayo kwanza yanaajiri watu wengi lakini pili yana *multiplier effect* kubwa mfano ni zao la pamba. Zao la pamba mwaka 2000 tulizalisha marobota kama milioni moja na laki mbili hivi, uzalishaji wa mwaka jana ilikuwa ni chini ya marobota laki mbili. Kuzalishwa kwa pamba kwa kiwango kidogo namna hiyo kwa lugha rahisi maana yake ni kwamba zao la pamba limeanguka. Kuanguka kwa zao la pamba kunamaanisha wananchi wanaofikia zaidi ya milioni 14, wananchi wanaotoka kwenye Wilaya zaidi ya 42 ambao kwa kiasi kikubwa shughuli zao za kiuchumi zimekuwa zikitegemea pamba hawana shughuli ya kufanya. Iko Mikoa ambayo hauwezi ukapambana na umaskini kwenye mikoa hiyo bila kugusa pamba, mojawapo ni Mkoa wa Shinyanga na Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwenye mpango huu, mkakati maalum wa kufufua sekta ya kilimo utajwe, acha tu kutaja kwa ujumla jumla kwamba kuongeza pembejeo, lakini uwepo mkakati maalum wa kufufua zao la pamba, kujenga viwanda vya mafuta yanayotokana na mbegu za pamba vilevile viwanda vya kusokota nyuzi za pamba na hatimaye kupata nguo. Tukifanya hivyo, tutatoa ajira kwa Watanzania zaidi ya milioni 14 lakini pia tutaondoa umaskini kwa mikoa zaidi na nane ambayo inaishi kwa kutegemea

zao la pamba. Kwa hiyo, eneo hili nilidhani ni muhimu Mheshimiwa Waziri akalifizama kwa umakini unaostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni zao la mifugo na hapa kuna tatizo kubwa sana. Hivi sasa tunakisiwa kuwa na ng'ombe, mbuzi na kondoo zaidi ya milioni 26. Mifugo hii wote tunajua ambavyo imekuwa ni kero kati ya wahifadhi na wakulima kwa upande mmoja pamoja na mifugo yenyewe. Ukiangalia kinachopatikana kutoka kwenye mifugo hii kimsingi ni kama hakihesabiki (*negligible*). Naiomba sana Wizara hasa Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Kilimo mkae pamoja muwe na mpango mkubwa pia wa ujenzi wa viwanda vya nyama, ujenzi wa viwanda vya maziwa, ujenzi wa viwanda vya ngozi, tuache hivi viwanda vidogo vidogo ambavyo vimekuwa vikisemwa na rafiki yangu mmoja ametajwa hata hapa Waziri wa Viwanda kwamba anachukulia suala la viwanda ni suala rahisi, ni suala ambalo ni *complicated* sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani ng'ombe hawa zaidi ya milioni 25 ambao kwa wastani wa bei ya soko ya shilingi 300,000 kwa ng'ombe mmoja unazungumzia utajiri wa zaidi ya shilingi triloni 7.5, ambayo ni karibia theluthi moja ya bajeti yetu ya Serikali, utajiri wa namna hiyo tunauona hauna thamani, wafugaji tunawafukuza kila mahali na kuwaambia warudi walikotoka. Mimi nimekuwa nikihoji sana hiyo lugha ya kusema watoke kwenye hifadhi warudi walikotoka, nikawa najiuliza hivi sisi Watanzania tukiambiwa turudi tulikotoka itakuwaje? Kwa sababu Watanzania tulio wengi wengine wana asili ya Asia, wengine Wabantu wana asili ya Afrika ya Kati na wengine *Nilotics* wana asili ya Afrika ya Kaskazini, hivi na sisi turudi huko? Ni lazima tujue mifugo ni rasilimali yetu tuiwekee mkakati maalum mzuri wa kuiendeleza wala si kuiona kwamba ni kero na inawezekana. Kwa hiyo, naomba sana eneo hili la mifugo liweze kutazamwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni la mtawanyiko wa uwekezaji wa kimkakati katika nchi. Kuna eneo ambalo tumezungumzia miradi ya kielelezo na kanda za kiuchumi, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 18. Ukitazama kanda za kiuchumi zilizotajwa za Pwani, Tanga, Dar es Salaam, Mtwara na Kigoma, najiuliza kama kweli tunataka kufanya kanda ya mkakati wa kiuchumi iwe kanda hiyo na huko ndipo pengine tutakoweka uwekezaji mkubwa na biashara kubwa na viwanda, haitawezekana kwa malighafi zitakazotoka katikati ya nchi yetu za mifugo na mazao ya kilimo kuyapeleka kwenda kuchakatwa kwenye viwanda ambavyo vitajengwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ukuzaji wa uchumi kwa kanda za kiuchumi za kitaifa ziwe kijiografia kwa kuangalia kila eneo linazalisha nini? Tuwe na makakati maalum wa kuendeleza mifugo kwa hiyo tuwe na kanda maalum ya Dodoma; Kanda ya Mwanza tuwe na mkakati maalum wa kuendeleza

madini, kuendeleza kilimo cha pamba na kuendeleza mifugo. Kanda ya Kigoma kule kwa kina Nswazugwako tuwe na mikakati hiyo ya kuendeleza uvuvi wa *Lake Tanganyika*, mawese na vitu kama hivyo. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inatofautiana utajiri wa rasilimali eneo kwa eneo, hauwezi ukategemea chuma cha Liganga kiwe rasilimali kwa kiwanda kitakachojengwa Tanga au kiwanda kitakachojengwa Bagamoyo. Kwa hiyo, ni lazima eneo ambalo rasilimali inapatikana, mifugo inapatika Shinyanga kiwanda cha nyama kijengwe huko na ndiyo huko kuufanya uchumi uweze kugusa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie eneo moja ambalo naona kama linasahaulika la misitu. Uzalishaji wetu na *potential* yetu kwenye misitu hatuitumii vizuri. Bahati mbaya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili hayupo, nchi ya Finland kwa mfano, uchumi wake zaidi ya *Euro* bilioni 20 kwa mwaka unatokana na mazao ya misitu. Ardhi wanayolima ni kama hekta milioni mbili, sisi ardhi yetu iliyoko kwenye hifadhi (*forest reserves*) ni hekta milioni 13 na eneo linalolimwa kwa maana ya *forest plantation* ni hekta 80,000. Maeneo makubwa ya hizi *reserves* kwa lugha ambayo anaitumia sasa hivi ndugu yangu Lukuvi kwa wananchi wa kawaida tunaita mashamba pori. Naomba niwafahamisha kama kuna mtu tajiri wa mashamba pori ni Wizara ya Maliasili na Utalii. Maeneo haya yanaitwa hifadhi lakini ukifika ni nyika hakuna miti zilishabaki nyasi na yamebaki maeneo ambayo yanatumika kukusanya rushwa kwa watu wanaokwenda pale kujitafutia riziki, hayana ulinzi wala hayafanyiwi shughuli yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Wenzetu wa Finland maeneo haya wametumia *PPP*, sekta binafsi mnaaita mnaingia *concession*, wanalima miti kwenye maeneo hayo, Serikali inapata kipato fulani na wale wawekezaji wanapata. Kwa mfano, sisi mahitaji yetu ya mbaao ni zaidi ya *cubic meter* milioni 40. Sasa hivi uzalishaji wetu ni *cubic meter* 450,000. Soko la mbaao la Kenya, soko la mbaao la Djibouti, *South Sudan*, Ethiopia mpaka Muscat wanasomba mbaao na wananunua mbaao kutoka Tanzania. Uwepo wetu hapa kijiografia na kuzungukwa na nchi ambazo hazina ardhi ya kutosha, Kenya hawana ardhi ya kutosha, Somalia wana vita na maeneo mengine ni jangwa, kwa hiyo tukitumia ardhi yetu ambayo tayari tunayo, naamini tunaweza kabisa kwa *export* ya mazao ya misitu na *revenue* ya kutoka kwenye mazao ya misitu kwa *commercial plantation* kwa kutumia sekta binafsi kuwa zaidi ya dola za Kimarekani angalau bilioni 20 ambayo ni zaidi ya trilioni 40 ambayo ndiyo bajeti ya Serikali. Tukiwa na mkakati wa namna hiyo kwa miaka 20, 25 kule mbele naamini sekta hii inaweza ikatoa mchango mkubwa sana kwa uchumi wa nchi yetu. Naamini kabisa kwamba tukiyatazama mambo haya kwa upana unaostahili kwa kiwango hicho, tunaweza tukaitoa nchi yetu kutoka hapo ilipo kwenda mbali zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kuna eneo ambalo tunazungumzia kuangalia upya mikataba ili iweze kuwa na tija kwenye uchumi na kwa wananchi na hasa mikataba inayohusu kodi. Kwenye sekta ya madini kuna mikataba ambayo ilikwishakuwekwa inayozuia Halmashauri zisitoze ushuru wa huduma na mikataba hiyo imefanya Halmashauri zisiwe zinanufaika pamoja na mabadiliko mazuri sana aliyofanya Mheshimiwa Profesa Muhongo. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala inadai zaidi ya shilingi bilioni 14 kutokana na malimbikizo ya ushuru wa huduma ambao imekuwa hailipwi kwa sababu mkataba ulifungwa kwamba ilipwe dola 200,000 wakati *proper service levy* ya 0.3% ni zaidi ya dola za Kimarekani milioni 1.8 kwa mwaka. Kwa hiyo, mnafungiwa mkataba wa kulipa dola 200,000 wakati sheria inasema *mlipwe over and above 1.8 million dollar*. Kwa hiyo, naomba mambo tuliyokwisha kuyaanza ya kuzungumza ili kurekebisha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lema ajiandae Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Taifa hili kujadili masuala yote yanayohusu mipango ya maendeleo bila kujadili *stability* na demokrasia muhimu katika Taifa hili, kinachojadiliwa hapa kilicholetwa na Dkt. Mpango hata kama kingekuwa ni sawa kwa asilimia 100 lakini kwa Taifa ambalo hakuna utawala bora, kwa Taifa ambalo demokrasia imeminywa, kwa Taifa ambalo vyama vya siasa haviruhusiwi kufanya shughuli zake mpaka mwaka 2020, mipango hii ina-*create instability* katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma tumekuwa tukisema kwamba nchi hii haitawaliki na tafsiri ya upande wa pili ikawa ni kwamba tunasema kwamba nchi hii haitawaliki kwa sababu tumepanga kuingia barabarani kufanya maandamano, kuvuruga Taifa. Maana ya nchi kutokutawalika ni viongozi walioko madarakani sasa ambao ndiyo wanaotawala Taifa hili kushindwa kabisa kujua na ku-*predict future* ya Taifa hili itakuwaje *incase* kama watahindwa kusimamia utawala bora na demokrasia katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea Mpango ambao una lengo la ku-*attract investors*. Mwekezaji yeyote mwenye akili hawezi kuleta mtaji kwenye Taifa ambalo limeua vyama vya siasa kufanya kazi zake za siasa. Maana yake ni nini? Lengo la kuua vyama vya upinzani likifanikiwa vilevile litakwenda kuuwa chama tawala chenyewe. Litauaje chama tawala? Ikifika mahali vyama vya upinzani haviwezi kuongea chama hicho ambacho kimefanikisha mpango huo kitazuia watu wake wasiongee na ndiyo sababu baada ya kikao cha asubuhi Wabunge wa CCM wengi walikuwa *positive* juu ya jambo hili kilitwa kikao cha

*party caucus* kwenda kuwaelekeza Wabunge namna gani ya kuja kuongea ndani ya Bunge hili badala ya kuongea ukweli ni kubeba Mawaziri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili linapoelekea na mambo yote yanayopangwa hapa hayatatekelezaka bila utawala bora. Kwa bahati mbaya sana tunaongea Mpango wa Maendeleo wa Taifa hili katika Taifa ambalo Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi Watendaji hawana *confidence*. Hakuna mfanyakazi wa Serikali nchi hii ana ujasiri wa kwenda asubuhi kazini ikafika jioni akajua bado yupo kazini. Jambo hilo limeleta wasiwasi na kwa sababu imeleta wasiwasi kwa Wakurugenzi, Makatibu Wakuu na kwa Mawaziri wengine hawajui ni wakati gani watatumbuliwa na ni kwa vigezo gani watatumbuliwa, kwa hiyo imekosekana *creativity* ndani ya ofisi za kazi na hakuna *innovation*. Ndiyo maana Bunge lenyewe likikosa pesa badala ya kwenda ku-*push* pesa zipatikane, Bunge ambalo lilisema lina fedha ya ziada likatoa fedha za madawati likapeleka kwa Rais Bunge hilo leo limeshindwa kuchapisha nakala zake. Sasa unajiuliza hili Bunge lililokuwa na ziada ya fedha likachukua fedha ikampeleka Rais ya madawati mbona leo imeshindwa kuwa na mpango wa kununua hata *tonner* ya kufanya kazi zake ndani ya Bunge hili? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongelea mpango bila kuongelea *stability* ya Taifa hili, demokrasia, ustawi wa jamii katika Taifa hili mipango hii hata kama ni bora kwa kiasi gani haitafanikiwa. Leo tulimuona Mheshimiwa Rais alikwenda kufungua kiwanda cha Bakhresa, akasema tena nimefurahi sana na zile sukari zilizokuwa zimekamatwa Waziri nendeni mkampe. Unajiuliza sasa kama sukari zilikuwa zimekamatwa kinyume na utaratibu kwa nini zilizuwa na kama zilikuwa zimekamatwa ndani ya utaratibu kwa nini zilizuwa mpaka Rais afurahishwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo kwa sababu tukisema Waheshimiwa viongozi ambao ni sisi pamoja na huko nje tumekuwa na hofu kubwa dhidi ya kusema ukweli, dhidi ya kupigania ukweli, leo kila mtu ni muongo na woga ni njia anayotumia shetani kutenda miujiza na imani ni njia anayotumia Mungu kutenda muujiza. Kwa uoga huu ambapo watu hawawezi kuamua, kwa uoga huu hakuna mtu anakwenda kazini akajua jioni atabaki kuwa mfanyakazi, ndiyo maana Rais alisema watu wanaficha pesa, ni kweli kauli yake ilikuwa na uhalali kwa asilimia kadhaa. Mimi kama sina *confidence* ya kwamba nitakuwa kazini kesho maana yake itakuja ku-*minimize* gharama zangu za maisha. Mimi niki-*minimize* gharama zangu za maisha maana yake ni kwamba nakosa *spending confidence* kwenye jamii ndiyo sababu unaona biashara zinakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kikao cha kodi cha TRA cha Wilaya nilimuuliza mtu wa kodi Arusha peke yake hizi kampuni za biashara ya kati zaidi ya 48 zimeandika barua ya ku-*close business* itakapofika Novemba mpaka



Disemba mwaka huu. Sasa badala ya kumsaidia Rais na kumwambia ukweli na siyo mambo yote anafanya Rais Magufuli ni mabaya, ana *courage* ambayo watu wengi hawana, lakini *courage* hiyo ikikosa hekima, maelekezo na ushauri Rais anakuwa kama Mungu, anakuwa yeye ndiyo kila kitu, ndiyo *Pay Master General*, ndiyo Waziri wa kila kitu, anakwenda kufumania, kila kitu anafanya. Hii imesababishwa na ninyi kutokumwambia Rais ukweli, Rais amekuwa polisi. Imefika mahali hata mtu mdogo kwenye Kamati akiongea Rais anapiga simu mwenyewe, Rais anatoa maelekezo mwenyewe mpaka kwa ma-RPC, hofu kubwa imejengwa katika Taifa hili. *(Makofi)*

### **KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa Lema kaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshauri mchangiaji kama atafuata utaratibu wa kikanuni kujenga hoja zake bila kuvunja Kanuni ya 64 na kuomba utaratibu huu natumia Kanuni ya 68. Anapotaka kutumia jina la Rais kwenye kanuni ya 64(1)(d) kutaka kulishawishi Bunge hili kwamba Mheshimiwa Rais sasa amekuwa ni kila jambo kwenye nchi hii na ndiyo maana Mpango huu hauna mwelekeo kitu ambacho si sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi, Mawaziri wamekuwa wakifanya maamuzi mbalimbali wanapokuwa kwenye ziara katika maeneo mbalimbali na wanapofanya maamuzi hayo Rais hayupo katika maeneo hayo. Kwa hiyo, nimuombe sana mchangiaji asitake kuvunja kanuni ya 64(1)(d) kutumia jina la Rais ili kuweza kushawishi Bunge hili kwamba mpango huu hauendi inavyotakiwa eti kwa sababu Mheshimiwa Rais anafanya kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utaratibu ufuatwe katika kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lema na mimi ningekuomba ujielekeze moja kwa moja kwenye Mpango ili uweze kufikisha ujumbe wako ili Serikali kwa yale mazuri iweze kuyafanyia kazi.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namheshimu sana Mheshimiwa Jenista alikuwa Mwenyekiti wangu wa Kamati siku za nyuma, lakini nashukuru kwamba amekiri kwamba Mpango siyo mzuri na kwamba Mpango kutokuwa mzuri siyo *intervention* ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu tunachokisema ndicho ambacho mkiniambia ninyamaze sitanyamaza. Hili ni Bunge na kazi ya Bunge ni kushauri Serikali, inapofika mahali Bunge linashindwa kushauri Serikali ndiyo hiyo hofu aliyonayo, niliposema Rais ana *courage* ya kufanya maamuzi mazito na magumu mlipiga makofi, tukisema Rais anakosea hatumuudhi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesema nimeona maono kwenye maombi, leo nimepelekwa polisi na sasa hivi navyoongea nimeambiwa maelezo uliyotoa hayatakiwi, polisi wa Arusha wanakuja kunichukua kwamba nimeona maono makubwa kwa nini sijalala hata ndani nimepata *bail* kabla sijawekwa *lockup*, haya mambo katika Taifa hili yanakwaza. Sasa ninyi ambao mnamuogopa, mimi siogopi, najua Rais ana nguvu, najua hii Serikali ina Usalama wa Taifa, Mimi nikitaka kufa leo nakufa asubuhi *I have no weapon* lakini hatutaacha kusema ukweli *for the sake of this country*, hii nchi inakufa, imepandikizwa hofu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema hapa Mheshimiwa Mbunge mmoja kwamba Wakuu wa Mikoa na ma-DC na Wakuu wa Mikoa wanaweka watu ndani saa 48. Kuna mambo mengine tena mkiongea huko tutasema na Mawaziri tunaongea nao mambo haya nayoongea mimi tunawakilisha sisi, lakini haya ni mawazo ya kwenu mnayotuaambia sisi, hatuwezi kuendelea na Taifa lenye hofu kwa kiwango hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mikoani OC hazijakwenda, hakuna fedha, mambo yanakuwa ni magumu, biashara zinakufa sisi ni wafanyabiashara. Utalii hapa mmempa Profesa ambaye Kinana alimuita mzigo *some days ago*, leo amekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Novemba peke yake utalii umeanguka kwa asilimia 48. TRA wamekuwa kama polisi, kontena la futi 40 lililokuwa linakadiriwa shilingi milioni 18 hadi 20 wakati wa Awamu ya Nne leo ni shilingi milioni 35 mpaka shilingi milioni 40. Wananchi wakiona TRA wanaona kama wameona wanajeshi kutoka Sudan. Hakuna *friendliness* kati ya walipa kodi na wanaotoza kodi. TRA wamejisifu wanakusanya kodi kwa muda mrefu, Mheshimiwa walikuwa wanakusanya *arrears*, leo kuna makampuni yameambiwa yalipe kodi ya miezi sita mbele watakuja kurekebisha baadaye. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Taifa linayumba, hali inakwenda vibaya, mitaani hakuna fedha, *Tanzanite* imeanguka kwa asilimia 40, utalii umeanguka kwa asilimia 48 kwa mwezi Novemba. Leo watu wanaopita Serengeti na Ngorongoro hata boda boda akipita mnamuweka kwenye *database as if* ni mtalii amepita. Mheshimiwa Maghembe akienda aka-*print* anakuja anasema watalii wameingia milioni moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mliongeza VAT na haya mambo alisema Mbunge hapa, mmekaa na Kenya na Uganda mkakubaliana pamoja, tathmini waliotumia watu wanaoshughulika na mambo ya uchumi ni kwamba Kenya *International Airport* imekuwa *listed* kama sehemu hatari ya utalii. Kenya juzi wakamleta mmiliki wa *facebook* wakamtembeza nchi nzima, ana wafuasi zaidi ya mamilioni ya watu, Kenya utalii unakua, Arusha hoteli zinauzwa, hakuna biashara kampuni zinafungwa, hoteli zinauzwa hata wateja hakuna benki zinafunga. Ukienda leo kwenye *DSE*, *CRDB* hali siyo nzuri, *Twiga Bancorp* imekabidhiwa kwa *BOT*, uchumi unakwenda hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haya mambo kwenu ni mabaya ni mabaya kwa manufaa ya nchi hii. Ule UKUTA tuliosema tunautangaza kama hamtarekebisha mfumo wa kiuchumi na kiutawala sisi hatutaingia barabarani ila iko siku mtatuomba tuwaambie watu warudi nyumbani hali itakuwa ni mbaya sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Taifa hili Rais hasafiri kwenda kutafuta *partners*. Leo amekuja hapa Mfalme wa Morocco juzi kaenda Zanzibar kapiga pensi na tisheti yake ina ganja, ina bangi hapa kifuani huyu, ndiye mwekezaji...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa hujaona wewe. (Kicheko/Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema hebu kaa kwanza. Mheshimiwa Lema jaribu kuzungumza lugha ya staha ndani ya Bunge, hilo la kwanza. Huna haja ya kutaja majina ya watu au kutaja nembo ambazo huna hakika nazo ndani ya Bunge hili.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Hiyo ndiyo *rulling* yangu, una dakika moja iliyobakia.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde dakika zangu ambazo Mheshimiwa Jenista alinipotezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mfalme na lile jani la mzaituni ambalo linatumiwa na vijana wengi sana wa mjini. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachosema ni nini? Nachotaka Bunge hili lielewe ni kwamba kazi ya Bunge hili ni kuisaidia Serikali...

**MBUNGE FULANI:** Wewe mwenyewe unavuta bangi.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Bunge hili likishindwa kuisaidia Serikali maana yake ni kwamba Serikali hii itayumba, kumwambia Rais ukweli siyo kumdharau, kumwambia unakosea siyo kumdharau. Mfalme ambaye haambiwi ukweli siku akishtuka mlikuwa mnamdanganya na hamumuambii ukweli atafukuza wote kazi. Kwa sababu huko tunakoenda atashtuka na atauliza kwa nini sikuambiwa ukweli kuna jambo kama hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Taifa kama hili ambalo limejaa hofu na wasiwasi ambapo hakuna mtu anayejua kazini atakuwepo mpaka kesho ama kesho kutwa ni Taifa ambalo limekosa *creativity* na *innovation*. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msigwa wajiandae Mheshimiwa Dkt. Nagu, Mheshimiwa Kingu na Mheshimiwa King.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie hapo alipoishia Mheshimiwa Lema, Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linao uwezo wa kumu- *impeach* Rais. Sasa kama tuna uwezo wa kumu-*impeach* Rais halafu watu tukimtaja Rais hapa mnatetemeka maana yake tunataka tukiuke Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Bunge pekee, ni chombo hiki pekee, waliotunga Katiba walijua kuna wakati Rais anaweza akakosea na hiyo mamlaka iko mikononi mwetu. Mimi nashangaa Wabunge tukimtaja Rais kama anakosea tutamui-*impeach* vipi kama anakosea anapoingoza nchi yetu? Kwa hiyo, hebu turudi kwenye *senses* zetu kwamba mamlaka hiyo tunayo na wala hatumuonei kama anafanya makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Mpango, wengi wamezungumza mimi narudia na juzi nilisema na tunasema ukweli kwa sababu tunalipenda hili Taifa. Nikuombe sana unapoleta mambo yako hapa usilete kama vile upo kwenye *lecture room* kwamba unataka kutupa *lecture*. Sisi ni wawakilishi wa wananchi, wametutuma wananchi na ndiyo maana mnapoleta huu mpango hapa ni ili sisi Wabunge wote tujadili vinginevyo msingekuwa mnaleta mngekaa nao huko Serikalini muendele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana ulipoleta, tena mimi tulikutana pale nje, mimi huwa nasema *openly*, tulikutana pale nje nikakuambia hizo kodi unazoleta kwenye VAT utaleta *chaos*, nikakuambia hizo kodi unazoleta bandarini utaleta taabu. Bandarini sikuwa na utaalim sana walau kwenye

maliasili nilikuwa najujua kidogo, lakini zimesababisha shida kubwa kwenye nchi yetu halafu hapa tunalindanalindana, tunafichamafichama kuelezana ukweli na mnamdanganya mfalme kwamba mambo yapo vizuri. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu chake hiki najua kanuni zinaeleza kwamba hatuwezi ku-review bajeti iliyopita kwa sababu haijapita miezi sita, lakini haya mambo yote uliyoandika yame-based kwenye bajeti ile iliyopita ambayo hata wewe mwenyewe Waziri hukuwepo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mpango unaouleta hapa haupo *realistic* kwa sababu Ilani ya Chama cha Mapinduzi aliyomaliza Mheshimiwa Jakaya Kikwete kipaumbele hakikuwa viwanda, hii sasa ya Mheshimiwa Magufuli inazungumzia viwanda. Huu Mpango wako umetuletea mambo ya *DARTS* na kadhalika ambayo ni mafanikio yaliyopita ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Kwa hiyo, mpango huu haupo *realistic*, upo *baseless*, tunajadili kitu ambacho hakina miguu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali hii kwa sasa tunapozungumza mipango Mheshimiwa Waziri Mpango lazima tuwe na watumishi ambao wana *confidence*. Amezungumza Mheshimiwa Lema hapa ukienda kwa watumishi wote wa umma hawana ujasiri katika nchi hii, mmewa-*terrorize* wote, hawana *confidence*, hawajiamini kila mtu akiamka asubuhi hajui kitu gani kitatokea. Haya mambo tunayopanga tutawezaje kuyatekeleza kwa watu ambao hawajiamini! Umma umeaminishwa kwamba watumishi wote wa umma ni wezi, wafanyakazi wote hawana ujasiri wa kukaa kazini, ile *morale* haipo kwa sababu kila mtu ni mwizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza vizuri sana Mheshimiwa Lema tukisema dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kutaka kuleta mabadiliko na nidhamu katika nchi hii au ku-*restore glory* haipo tutakuwa tunasema uongo. Kuna mambo ambayo ameonyesha dhamira nzuri, wote tunakataa rushwa, wote tunakataa mambo mabaya ndani ya nchi lakini njia anazozitumia za kutisha watu na kuvunja sheria hizo ndiyo tunazozikataa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ripoti ya Utafiti wa Amani Duniani iliyotolewa na Taasisi ya Kimataifa ya *Institute of Economics and Peace* ya mwaka 2015, Tanzania ni moja ya nchi 64 duniani zinazokaribia hatari ya kuvunjika kwa amani kwa sababu ya ukandamizaji wa kidemokrasia. Sasa tusipokuwa na amani na kuheshimu na mipaka na mipango tuliyojiwekea wenyewe tutawezaje kusonga mbele na mipango hii mizuri? Hii nchi ni yetu sote, pale Rais anapofanya vizuri tutakubaliana naye, lakini mazuri yake yote anayoyafanya yanaharibika pale alipozungukwa na watu ambao hawamwambii ukweli. Sisi hapa tutamwambia ukweli, mtukate vichwa

tutamwambia tu, kama yupo uchi tutamwambia upo uchi, *we are not scared of him. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zitto amezungumza hapa Serikali hii haipo *coordinated*. Ukienda kwa mfano kwenye mipango yako hii hakuna mahali popote ambapo umezungumzia *espionage* (uchumi wa kijasusi). Wizara ya Mambo ya Nje ndiyo jicho la nchi ambapo mimi nashangaa katika mipango yako ya mwaka jana haikukuambia jinsi ambavyo Congo ni ya muhimu sana katika bandari yetu ya Dar es Salaam, Wizara ya Mambo ya Nje ilikuwa wapi? *(Kicheko)*

Leo Wizara ya Mambo ya Nje kama ni jicho, kama ipo *coordinated* ingeweza kusema unapopeleka mpango huu kwamba bandarini tutaongeza kodi kiasi hiki Mheshimiwa Mpango unakosea tutapoteza *potential customers*. Kama Serikali hii ipo *coordinated* ulipopandisha VAT kwenye mambo ya *tourism* Waziri wa Maliasili angekuambia *you are wrong* tunaenda kupoteza watalii. Hata hivyo, kwa sababu mkiamka kila mtu afanya la kwake, anawaza la kwake na mnashindana kwenda kujipendekeza kwa Magufuli matokeo yake ndiyo mnatuletea mipango ya ovyo ovyo. Tupo hapa kama Bunge, hampo *coordinated* ndiyo maana Mheshimiwa Kigwangalla anaweza akasema dawa zipo kidogo, Mheshimiwa Ummy anasema zipo za kutosha na Makamu wa Rais anasema hazipo, tumsikilize nani sasa, *the same government! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri najua ni msomi, Mpango huu kuna tafiti nyingi ambazo hata rafiki yangu asubuhi amezungumza hapa. Ukiangalia tafiti zilizofanywa na Taasisi ya Kimataifa ya GCI kuhusiana na mazingira bora ya uwekezaji Tanzania inashika nafasi ya 120 kati ya nchi 140 zilizotajwa kwenye uwekezaji huo. Ukiangalia moja ya matatizo tuliyonayo Tanzania nchi yetu imekuwa ni ya nne, mazingira ya uwekezaji hayajawa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Tanzania inahesabiwa kwamba hatujawa wazuri katika matumizi ya teknolojia. Huu mpango hautafsiri ni namna gani tunapambana na hayo maeneo ili tutengeneze mazingira mazuri ya uwekezaji. Kwa hiyo, hizi tafiti zinaletwa halafu Mheshimiwa Mpango na wewe unaenda njia yako. Serikali nzuri na jasiri inaweza ikasimama na mimi ningekuwa wewe ningekuja hapa kwa sababu kimsingi hili joto tunaloliona mwezi wa sita mwakani litakuwa kubwa sana na inawezekana Bunge likaondoka na kichwa chako hapa. Inawezekana Mheshimiwa Waziri huu mpango labda ali-copy New Zealand au Australia, ni busara tu kuja hapa na kusema jamani *this things it is not going to work here* nili-copy mahali nika-paste hapa hai-work, tutaambizana ukweli. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo ni kweli tumeshindwa kuyafanya kwa visingizio mnavyovileta, lakini kuna mambo we *told you*, ulishupaza shingo ukakataa. Kuna *data* nyingi zinaonyesha jinsi ambavyo Serikali yetu haina mazingira mazuri ya uwekezaji. Zimekuwa ni ngonjera nyingi hapa na kukandamiza demokrasia na kupiga wapinzani na yote yanayoletwa hapa yanakuwa hayatekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niwaombe Wabunge, hii nchi ni yetu sote na wala hatuitaji kugombana, tunahitaji kama Wabunge tuongee lugha moja lakini kwenye ukweli tumwambie mtu amefanya vizuri na kama amefanya vibaya tumwambie amefanya vibaya. Msingi wa kwanza lazima turudishe demokrasia katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hali mnayotaka kuiweka kwenye Chama cha Mapinduzi ya kuogopa watu mnaitoa wapi? Hata Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema tusiogope watu, tuwaheshimu watu. Leo ndani ya chama chenu mmeanza kuogopa watu hicho chama chenu hakina wazee cha kuwaonya watu wasiogopwe? Hivi vyeo ni dhamana, alikuwepo Baba yetu wa Taifa na nataka niwaambie Serikalli ya Awamu ya Tano msidhani wale wa Awamu za Kwanza, ya Pili, ya Tatu na ya Nne hawajafanya mazuri na hata wapinzani hatusemi hivyo, kuna mambo mazuri ambayo Baba wa Taifa aliyafanya lazima tuyaenzi na kuyaheshimu, lakini kuna mambo mabaya aliyoyafanya tutayakataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi kuna mambo mazuri aliyafanya na mabaya aliyafanya mazuri tutayaheshimu na alikosolewa, alisikiliza, tukampenda. Akaja Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alifanya mambo mazuri tukampigia makofi, tulipenda hata hotuba zake za kila mwisho wa mwezi zilikuwa ni hotuba zilizoshiba siyo za vijembe za kutukana watu, lakini kuna mambo mabaya tulimsema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaja mzee wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na kwamba tulim-*challenge* ni kweli, pamoja na kwamba kuna mambo hatukukubaliana naye lakini alisaidia nchi hii kwenda mbele. Kipindi chake aliweka mazingira walau watu duniani walianza kupenda kuja kuwekeza Tanzania na walau aliruhusu demokrasia. Tulimsema humu ndani lakini alihakikisha kila mtu kama Mtanzania anatoa mawazo yake, leo kwa nini Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli asisemwe? Tulikuwa tunakaa naye pale kwenye kiti tunamfuata pale leo tunamuogopa ana mapembe? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wabunge wa CCM hebu tuweke itikadi zetu pembeni, tusimame kama Bunge, Rais akikosea tuwe na uwezo wa kusema *no*, wewe ni Rais wetu lakini hapa *no*. Hatuwezi tukawa waoga,

anatisha kila mtu na kila mtu anajipendekeza kusema uongo. Hii nchi ina hali mbaya lazima tushirikiane. Ninyi mnaopeleka hiyo mipango kwa sababu mnamzingira akisimama kwenye vyombo vya habari anasema wale waliokuwa wanaiba pesa ndiyo wanapata taabu, hivi maskini wanaouza vitumbua kule...

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Msigwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtaarifu tu Mheshimiwa Msigwa kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Wewe jipu tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Kwa sababu sitarajii mpinzani wako akushauri jambo jema na akikushauri hilo jambo liache.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MBUNGE FULANI:** Yaani unaongea hivyo mbele ya Waziri Mkuu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Namna ambavyo Serikali inaendeshwa chini ya Rais Mheshimiwa Magufuli ni kwa *style* ambayo sisi tunataka. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waoga.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upande huo huo uliosema Serikali iliyopita ilikuwa ni dhaifu, haichukui maamuzi, haifanyi nini hao hao.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kutoa taarifa tu kwamba hao hao leo hii wanasema sisi tunafanya mambo kwa kumwogopa Rais, sisi tunamheshimu Rais kwa sababu ameshinda uchaguzi na alichaguliwa na Watanzania. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*



**MWENYEKITI:** Ahsante inatosha, Mheshimiwa Msigwa Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Tulia tujenge nchi wewe.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mheshimiwa Simbachawene siipokei na haya ndiyo niliyoyasema ndiyo uoga tunaouzungumza huo. *(Makofi)*

La pili hayo maneno aliyoyazungumza Mheshimiwa Simbachawene wakaongee kwenye *party caucus*. Hapa tunaongea... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa jielekeze kwenye hoja iliyoko mbele yako.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Sawa Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi ndiye ninaye-control mazungumzo humu ndani.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Nimekusikia Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Na mimi ndiye mwenye kadi nyekundu na kadi ya njano, hakuna mwingine humu ndani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu uulinde.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ndugu zangu nimesema hapa hakuna mpinzani yeyote anayesema Serikali zilizopita hakuna mazuri yaliyofanyika, hakuna anayesema hivyo. Tunachosema mabaya tutakosoa na tutaendelea kukosoa. Kama ninyi mnamuogopa Mtukufu Rais sisi tutamsema, tutamkosoa ndani ya Bunge na nje ya Bunge na akifanya vizuri tutamwambia.

Niombe Wabunge wote tushikamane, tunapojadili mambo mazuri ya nchi wote tuwe pamoja uchumi uko vibaya, hakuna pesa mifukoni hakuna pesa kwa watu. Mheshimiwa Rais mnam-*mislead* eti anasema waliokuwa wanapiga

rushwa ndiyo wana shida huko mitaani mama ntilie kwenye majimbo yenu walikuwa wanapiga rushwa wapi? (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Ukweli huo.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Watu wana hali mbaya. Wanashindwa kulipiwa ada halafu mnakuja hapa mnasema wapiga rushwa walikuwa wanapiga rushwa wapi kwenye majimbo yenu. Hivi ninavyozungumza nyuso zenu zinawashuka kwa sababu mnajua ukweli huo kwamba hali ni mbaya. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba wote tuchangamke tumdhibiti Waziri wa Fedha alete mipango na bajeti inayoeleweka. Mawaziri wengine mnabeba mzigo sio wenu, wakati wa bajeti mwaka jana tulikuwa tukiwaambia pesa hazitoshi mnasema aah zinatoshia hivyo hivyo. Sasa hivi kwenye Kamati mmerudi tena mnasema kwa kweli hazitoshi mtusaidie ninyi ninyi, sasa hivi mnasema hazitoshi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala tumbane Waziri wa Fedha alete mipango inayoeleweka siyo mipango ya ku-copy na ku-paste sijui kutoka wapi iwe katika mazingira ya kwetu. Tuletee mipango *in our context* siyo mme-copy New Zealand au sijui Australia huko *it doesn't work here*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nataka niwakumbushe Kanuni ya 64(1)(e) inasema:-

*“Hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote anayeshughulikia utoaji wa haki, isipokuwa tu kama kumetolewa hoja mahsusi kuhusu jambo husika.”* (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, mwenye hoja hapa ni Mheshimiwa Mpango, Rais hayupo humu ndani siyo jambo jema kutaja jina la Mheshimiwa Rais humu ndani wakati yeye hayupo humu ndani.

**MBUNGE FULANI:** Aje ni sehemu ya Bunge.

**MWENYEKITI:** Natoa tahadhari *yellow card* nimeshaionesha, mimi nataka tuchangie hoja za msingi ili Serikali iweze kufanyia kazi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu wajiandae Mheshimiwa Kingu na Mheshimiwa King.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongea na...

**MBUNGE FULANI:** Mlikuwa mnachukuia JK eeh!

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** ...kutoa mapendekezo kuhusu mpango huu ambao ameuleta Mheshimiwa Dkt. Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kwenda hapo, naomba niwakumbushe Wabunge kwamba jukumu letu humu ndani kama wengi wanavyosema ni kuishauri na kuisimamia Serikali. Siyo jukumu letu kuonyesha Serikali haifai na kupinga pale ambapo hata haistahili kupingwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya kushauri na kusimamia Serikali kati ya vyama vya upinzani na chama tawala lazima ni tofauti. Nasema hivyo kwa nini?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Nimewasikiliza hamkusikia mama Nagu akisema naomba na wengine wanapoongea msikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama ukiwa na watoto nyumbani wengine wa kwako na mwingine wa kambo, yule wa kwako anapoangusha *glass* unasema bahati mbaya, wa kambo anapoangusha *glass* unasema makusudi, huo ndiyo ukweli wenyewe.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utamaduni wa vyama vingi *unless* mnakataa jukumu la vyama vyenu, utamaduni wa vyama vingi ni upinzani kuonyesha Serikali...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nagu hebu kaa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, naomba na imekuwa ni *habit* upande huu mkichangia upande huu wapo kimya, upande huu wakichangia huku mnaanza vijembe, siyo jambo zuri.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy nimekuona, nakupa *yellow card* ya mwisho. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu endelea.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mama yao hata wakinitukana nitaosha mkono sitaukata. *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba jukumu la wapinzani ni kupinga Serikali iliyo madarakani hilo linajulikana, lakini basi pingeni kwa lugha ya staha. Sisi ambao ni chama wa tawala kazi yetu ni kuisimamia, kuishauri kwa lugha ya staha. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naenda kwenye Mpango wa Maendeleo, huu ni mpango wa miaka mitano wa pili ili kufikia dira ya Taifa letu. Dira ya Taifa letu inatutaka mwaka 2025 tuwe ni Taifa ambalo lina uchumi wa kati na tunatumia mipango hii na utekelezaji wake kutusogeza pale. Kwa hivyo, tulifanya tathmini ya miaka mitano ya kwanza tuliyoitekeleza na tukaona kwamba tumepiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ilika bila mipango kwa miaka mingi. Mimi nakumbuka kabla ya mipango hii uchumi wa nchi hii ulikuwa ni hasi mbili leo tuko asilimia sita na zaidi maana yake uchumi umepanda kwa asilimia nane. Kwa hiyo, miaka mitano ya mpango huu, mwaka wa kwanza ulitufanya tukapiga hatua na huu ninaamini utatufanya tupige hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie kwamba hakuna kazi nzuri ambayo haifanywi kwa bidii. Sisi akina mama na nitatumia mfano ambao unanihusu mimi, tunabeba mimba miezi tisa tunatapika tunaenda *labor ward* tukitegemea kufa na kupona. Katika mpango huu vilevile tufikirie hivyo kwamba baada ya kutekeleza tutapiga hatua. *(Makofi)*

Sasa nataka niseme tulivyotathmini mpango wa kwanza wa miaka hii mitano ya mpango tumepiga hatua uchumi unapanda. Hata hivyo, tunajua maeneo yanayopandisha uchumi siyo yale ambayo yanahusika na watu *directly*. Kwa hivyo, sasa tuangalie yale ambayo yanahusika na watu *directly*. Tunakubaliana kwamba azma yetu ya miaka hii mitano ni kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimkumbushe Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango kwamba hatutakuwa na viwanda bila kuwa na kilimo kinachotegemewa. Huo ndiyo ukweli wenyewe kwenye

maelezo yake ya hakuongea hata kidogo juu ya kilimo. Kwanza kuongea juu ya kilimo ni kuwapa moyo Watanzania asilimia 80 wanaotegemea kilimo. Kilimo ndiyo kitatoa chakula kwa wale watakaofanya kazi viwandani, kilimo ndiyo kitakachotoa malighafi ya viwanda, tija ya kilimo ndiyo itafanya watu waondoke kwenye kilimo waende kwenye viwanda. Kwa hiyo, naomba katika mpango huu na tunapotekeleza mpango huu kupitia bajeti tuone kwamba kilimo kinapewa kipaumbele ili tufikie viwanda tunavyovitaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tumeamua uchumi wa viwanda lazima tuangalie ni viwanda gani ambavyo vitatusaidia. Kiwanda cha kwanza narudia tena kama walivyosema Wabunge kiwanda cha chuma ni kiwanda mama, kiwanda cha kemia ni kiwanda mama. Viwanda vile mama lazima tuvipe kipaumbele ili vituwezeshe twende kwenye viwanda vingine na tuwe na *sustainable industrial development*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo ndugu yangu Mheshimiwa Mpango hakikisha utekelezaji wa kiwanda cha chuma cha Liganga na mkaa wa Mchuchuma umepewa kipaumbele. Vilevile katika kuchochea kilimo hakikisha viwanda vya mbolea vinapewa kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tujue kwamba siyo bajeti ya Serikali tu ndiyo itakayotekeleza mpango wetu. Kwanza naomba katika kukusanya kodi huwezi ukamkamua ng'ombe bila ya kumlisha, lazima tutambue sekta binafsi inataka kulishwa, muone ni namna gani tutaipa nguvu na iweze kutoa kodi ya kuaminika. Kuna wale wanaokimbia kodi wale ni wachache lakini kwa ujumla sekta binafsi lazima tuiimarishe. Sekta binafsi itatusaidia kutekeleza mpango huu kupitia kilimo, kupitia viwanda na vingine vyote tulivyovipanga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna rahisi ni utekelezaji wa sera na Sheria ya PPP, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Naomba sana tusipuuze hili kwa sababu huu ni uchumi wa soko tumeshakubali na uchumi wa soko unategemea sekta binafsi. Nasema kwamba pengine kuna mahali ambapo tumeenda kando, naomba tuache kule tulikoenda kando mimi napendekeza kwamba tukae na sekta binafsi ijue kwamba kodi yao ndiyo itawatengenezea mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta binafsi naomba tuwe na *One Stop Center effective* ile ambayo ipo ni ya maneno tu. Naomba mfanyabiashara anapotaka kuandikisha biashara yake aweze kutoka na leseni na ajue aende kukopa au *equity* itatoka wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulisema ndugu zangu mliongea juu ya *Logistic Center* ya Kurasini. *Logistic Center* ya Kurasini tulikuwa tumepanga kwa ajili ya ku-feed Kariakoo siyo kuua Kariakoo. Bidhaa

zinazouzwa Kariakoo zinatoka China, Thailand na Indonesia, Kurasini ndiyo italetwa bidhaa hizo *in bulk* na wale wa Kariakoo watachukulia pale, hiyo ni namba moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ya pili *Logistic Center* itaonyesha viwanda gani ambavyo vitakuwa na faida Tanzania kwa sababu pale ndipo *demand* itajulikana kama ni nguo watu wanataka tukijenga kiwanda cha nguo tutapata faida, kama ni viatu tukijenga kiwanda cha viatu tutapata faida. Kwa hiyo, *Logistic Center* hiyo tumeshaanza kuitekeleza naomba iharakishwe kusudi tunapojenga viwanda vyetu tujue ni viwanda vipi ambavyo vinatakiwa na tusikisie viwanda vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo nataka kulisema ndugu zangu ni kwamba hii ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi lakini uongozi mpya. Uongozi mpya unapokuja kwa vyovyote watu hawatakuwa na uhakika; na mfanyabiashara anataka awe na uhakika; kabla hajawa na uhakika yanayotokea ndiyo yanatokea. Pale ambapo tutawahakikishia uchumi wao wafanyabiashara watarudi na mimi nina hakika nchi hii baada ya hapo itakuwa *steady* hatuna sababu ya kuogopa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia tena uchumi huu ambao tunaujenga lazima uwe na uhusiano wa watu na ndiyo maana kama Mheshimiwa Mpango atakumbuka nilimwambia tuandike maendeleo ya watu ili isiwe maendeleo ya vitu tu. Tunavyopiga hatua tunataka maisha ya watu yawe bora zaidi, tunataka uchumi wa nchi uwe bora lakini ubora wake utokane na watu kusema kwamba tuna nyumba bora, tuna dawa za kutosha, tuna nguo za kutosha hii ndiyo itakayofanya mpango huu uwe mpango wa maendeleo ya watu na si maendeleo ya vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ili wengi wapate nafasi na ninaombeni pingeni, tusimamie na tushauri lakini wote wawili tutumie lugha iliyo na staha na tutajenga heshima ya Bunge hili kwa upande wa upinzani na upande wa chama tawala mimi sina wasiwasi, ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kingu, ajiandae Mheshimiwa Omar King.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita moja kwa moja katika ushauri kwa Serikali. Jambo la kwanza ambalo ninafikiri nitumie nafasi yangu ya uwakilishi kuishauri Serikali ni katika ongezeko la mahitaji ya matumizi katika fedha tunazozipata kutokana na deni la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba katika kipindi cha mwaka ulioisha 2015/2016 matumizi makubwa ya deni la nje na ndani la Taifa yalielekezwa katika sekta za nishati, barabara, madaraja na viwanja vya ndege. Nataka nimshauri kwa dhati kabisa Waziri wa Fedha, tunakopa fedha kutoka nje na ndani kwa lengo la kwenda kuwekeza kwenye sekta ambazo kimsingi hazina uhusiano wa moja kwa moja katika ku-stimulate ukuaji wa uchumi, kuna tatizo. Ninatoa mfano, tunakopa fedha kutoka katika taasisi za kifedha za ndani na za nje ya nchi, tunajua sote kwa pamoja asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima. Hivi ndugu zangu katika fikra tu za kawaida, nimeshawahi kuwa Mkuu wa Wilaya pale Igunga, katika vitu ambavyo lazima Waziri wa Kilimo na Waziri wa Fedha mfanye kazi kwa *coordination*. Ndugu zangu ukiangalia miradi tuliyonayo kama nchi, miradi mikubwa ya *schemes of irrigation* ni miradi ambayo ilijengwa na muasisi wa hili Taifa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kwamba nchi tunataka tuwasaidie wakulima ambao ni asilimia 80 ya Watanzania, hivi tunaachaje kwenda kukopa fedha na kwenda kuwekeza kwenye miradi ya kuwasaidia wakulima kufunga *irrigation schemes*? Nina mfano mmoja na Mheshimiwa Dalaly Kafumu utaniunga mkono.

Nilipokuwa Mkuu wa Wilaya ya Igunga, tuna mto unaitwa Mto wa Mbutu kipindi cha mvua mto huu kuna maji ambayo ukienda kuyaangalia yanayotiririka na kupotea na chini ya Igunga kuna eneo la karibu mpakani mwa Singida na Igunga eneo ambalo ni *fertile* kwa ajili ya shughuli za kilimo. Tumepiga kelele tukiwa pale kwamba utengenezwe mkakati ifunguliwe *irrigation scheme* kubwa ajili ya kuongeza tija katika uzalishaji wa kilimo cha mpunga Igunga mpaka leo imekuwa hadithi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nataka nitoe ushauri, tunapokopa fedha kutoka katika Taasisi za ndani na nje, pelekeni fedha hizi kwenye miradi ambayo itakwenda ku-stimulate ukuaji wa uchumi na kumgusa mwananchi moja kwa moja kilimo kikiwa cha kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili, tunazungumzia habari ya ku-industrialise nchi, *how do we industrialise nchi wakati vocational education hakuna mipango yoyote ya kusaidia kwenye vocational education hapa?* Nilitarajia Waziri wa Elimu kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha kuwepo na *coordination* ya kuhakikisha ya kwamba tunapojiandaa nchi kui-industrialise

lazima tuwaandae watoto wa Kitanzania kuwa na uwezo na ujuzi wa kufanya kazi kwenye viwanda tunavyotaka kuvijenga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe mfano, ninawapongeza watu wa NSSF nimeona wameifungua *National Milling*, ninaona wanaelekea kujenga Kiwanda cha Sukari ambacho wanasema kinakwenda kuajiri watu zaidi ya laki moja, nani tumeshaanza kuwaandaa watoto wa Kitanzania ndani ya miaka tatu kitakwenda kusimama, tumefanya mikakati gani kuwanda watoto wa Kitanzania kuwa na *vocational skills* ya kwenda kifanya kazi kwenye viwanda hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu niwashauri Mawaziri kwa nia njema Mawaziri wa Serikali yangu, Mawaziri wa Serikali inayotokana na chama changu, niwashauri. Ninawaomba ndugu zangu, mambo mengine hebu tuwe na *creative* sisi wenyewe tuwe na *creativity*, kwa mfano, hata suala hili la kumaliza tatizo la madawati tulisubiri mpaka Rais atoe tamko, lakini hivi leo tunaposema nchi tunataka iwe nchi ya viwanda hivi tunajua kwamba tuna walimu wetu mpaka leo hawana nyumba za kuishi? Hivi kwa nini asitokee Waziri mmoja aseme ninaweka mikakati ndani ya kipindi cha miaka mitatu hakuna mwalimu atalala nje, hakuna mwalimu atakwenda kukaa kwenye nyumba ya kupanga linashindikana hilo? Mambo haya tukiweza kuyafanya ndugu zangu tutajenga base ya kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa itakuwa ni elimu itakayoendana na zama hizi tunazozungumza, zama za viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili, kudorora kwa uchumi. Ninaishauri Serikali yangu kwa nia njema, hakuna shaka kwamba kuna viashiria na dalili kwamba uchumi wa nchi yetu to *some extent* kuna mdororo. Ninatoa ushauri kwa kaka yangu Mheshimiwa Mpango, Mheshimiwa Mpango ninakujua nimefanyakazi na wewe nikiwa Serikalini, ninakujua uzalendo wako haya mambo ya kuteleza hapa na pale tutasaidiana kwa lengo la kulijenga Taifa letu.

Ninakupa ushauri, Mheshimiwa Waziri wa fedha fanyeni kila mnaloweza punguzeni base ya kodi kwa wananchi, kodi zimekuwa nyingi sana. Tume-tax kila maeneo na unapooongeza *tax* kila eneo *definitely* lazima utapunguza *circulation* ya fedha kwenye uchumi. Na ukishapunguza *circulation* ya fedha kwenye uchumi utakwenda kuathiri masuala mazima ya huduma na uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ninaotoa kwa Serikali yangu, kuna fedha mlizichukua za mashirika na taasisi mkazipeleka kuziweka kwenye *deposit* ya Benki Kuu. Watu wa mashirika ya umma, NSSF na mashirika mengine walikuwa wakipata riba kutoka kwenye mabanki kwa hizo *deposit*. Ninawashauri Waziri wangu rudisheni fedha hizi kwenye mabanki, yaiteni mabanki myape maelekezo yapunguze riba ya mikopo kutoka asilimia 18 mpaka 13 mtakuwa



mmeongeza wigo wa Watanzania kukopa na mtakuwa mmesaidia *middle class* katika *business* hapo tutakuwa tunajenga uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *theory* inasema kwamba kiuchumi, mahali popote unapotaka ku-*stimulate* uchumi wa nchi kwa lengo la kukuza wafanyabiashara wa kati, ukifanya kitu kinaitwa kupunguza pesa kutoa pesa kwenye mzunguko katika uchumi maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba watu wanapokuwa hawana fedha kwenye uchumi inakwenda kuathiri hata shughuli za uzalishaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninatoa ushauri tusi-*ignore* suala la kusema kwamba pesa hakuna mtaani tukaishia kusema kwamba watu wanapiga dili, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuende *extra miles* na tutumie wachumi wa Taifa hili tulionao wafanye tafiti, watuambie Tanzania kwa uchumi tulionao ni fedha kiasi gani zinahitajika ziwepo kwenye *circulation* na watupe majibu ni fedha kiasi gani sasa hivi kwenye *circulation* hazipo, ziko wapi ili kusudi tuweze kuwa na *remedy* katika hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie suala zima la sera za kifedha (*monetary and fiscal policy*). Ukiamua kujenga uchumi ambao utaleta ushirikishwaji wa wananchi lazima tuhakikishe ya kwamba uwepo wa fedha nyingi kwenye mzunguko. Inawezekana labda Waziri wa Fedha waliamua kubana fedha kwenye mzunguko kwa lengo la ku-*control inflation* kwenye nchi kwa maana ya kwamba bei zinakuwa juu na fedha inakisa thamani. Lakini nataka nikwambie kitu kimoja, bado tunaweza kulifanya hili kwa kuziagiza *commercial banks* zikaweka riba kubwa kwa watu wanaweka *deposit*. Watu watapeleka fedha kwenye mabanki lakini pia tukaziambia benki zikashusha riba ya mikopo kwa wafanyabisahara wa kati na wakubwa tuta-*encourage private sector* kuchukua mikopo na ku-*invest*. Tunaposema tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda tukiacha hali iendelee namna hii kuna hatari kubwa ya Serikali kukwama na kuna hatari kubwa ya nchi kukwama kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia jambo lingine ninalotaka kushauri kwa nia njema kabisa kuna mambo tumekuwa tukiyazungumza hapa kwa muda mrefu. Ninawashauri Mawaziri wangu wanaotokana na chama changu kilichoko madarakani kwa nia njema tunaomba sana Mawaziri wasiwe wanasubiri mpaka matukio ndiyo waweze kuchukua hatua kwa mfano, mwaka jana kipindi tunafungua Bunge la mwezi wa 11, nilikuja na kilio juu ya usumbufu wa ndege wanaokula mazao ya wakulima maskini watu wasio na kipato. Tunazungumza hapa Mheshimiwa Waziri, leo ninapozungumza Singida ndiyo Mkoa tuna-*lead* katika *production* ya *sunflower* lakini leo ninavyozungumza

asilimia 70 ya *sunflower* iliyolimwa kwenye jimbo langu iliwa na ndege wanaitwa silingwa na mpaka sasa hivi tunavyozungumza nina imani hata Waziri usikute wanasubiri msimu ufike tuanze kupiga kelele tena Bungeni hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mtimize majukumu yenu kwa lengo la kumsaidia Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Sina mashaka na uzalendo wa Dkt. Magufuli, sina mashaka na uzalendo wa huyu Rais katika kutetea na kupigania maslahi ya Taifa hili lakini inawezekana kabisa kuna baadhi ya wasaidizi kwa makusudi yao wameamua kumkwamisha Rais wetu *whether* kwa kuogopa kumshauri vizuri. (Makofi/vigelele)

Kwa hiyo, ninatoa ushauri tuisubiri mpaka mambo yaharibike ndiyo tuje kwa ajili ya kuanza kupiga kelele. Wakulima wetu wanahitaji kuiona Serikali yetu iko *proactive* na kushughulikia matatizo na changamoto zao kabla athari hazijaonekana. (Makofi/vigelele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu, ni wazi kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. John pombe Magufuli alipokuja na sera ya elimu bure, niitumie fursa hii kuipongeza sana Wizara ya elimu na kumpongeza Rais japokuwa changamoto ni nyingi lakini ninauona moyo wa kizalendo wa Rais wetu katika kulitetea suala zima la sekta ya elimu. Changamoto tuliyonayo na alizungumza kaka yangu Mheshimiwa Heche, alizungumza leo asubuhi, tumeongeza idadi ya *enrolment*. Mimi kwenye jimbo langu peke yake asilimia ya wanafunzi walioongezeka kwenye udahili ni asilimia 17.8 kwenye jimbo langu lakini ndugu zangu tunauhaba wa vyumba vya madarasa, hivi ndugu zangu hili nalo tunasubiri mpaka Rais atoke atoe *declaration* kwamba muanze vyumba vya madarasa? Kwa nini tusiweke mipango mikakati tuseme ndani ya kipindi cha miaka miwili tatizo la changamoto la uhaba wa vyumba vya madarasa litakuwa limetatuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa changamoto kwa Mawaziri, ninatoa changamoto kwa Baraza langu la Mawaziri, nendeni mkakae mjifungie pelekeni *proposal* Dkt. Magufuli ni Rais msikivu suala la madawati nililizungumza mimi hapa Bunge la kwanza ndiyo nilikuwa Mbunge wa kwanza kulizungumza na alipokuja Singida sisi tulionyesha mfano na chama...(Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Omar King, jiandae Mheshimiwa Chumi.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai na akatufanya sisi leo kuwa miongoni mwa Wabunge ambao tutachangia maslahi ya nchi hii katika mipango ya kuendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Ni nafasi adhimu ya kuweza kuchangia Mpango wa Maendeleo au Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nizungumze kitu kimoja kidogo ambacho wasemaji wengi sana walikuwa wanakigusagusa ambalo linahusiana na masuala ya bandari.

Kwanza nakwenda huko moja kwa moja masuala ya bandari, ni kweli tumeona kwamba mzigo katika bandari umepungua lakini tunaposhauri tujaribu kuangalia katika maeneo ambayo mzigo maeneo gani yamepungua. Ukitizama katika hizi *transit goods* ambazo zinakwenda katika nchi jirani basi utagundua kwamba nchi ya Zambia na DRC Congo ndipo mzigo ulikopungua, lakini ukiangalia Uganda na Malawi mzigo haujapungua. Sababu zimeleezwa na wengi pengine labda VAT na pengine labda hiyo *single custom territory* ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa kufanya mizigo katika bandari ipungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili nilikuwa naomba Serikali ijaribu kuangalia hivyo vitu ambavyo vimetajwa hapo kwamba ni sababu na tujielekeze na tubaini kwamba hiyo kweli ni sababu; kwa sababu kuna baadhi ya mambo yalianza kabla ya hapo. Tukija katika hiyo *single custom territory* kwamba ilikuwa iko toka mwaka 2013 ikaanza kuwa *implemented* Disemba, 2014 sasa tutizame kitu gani kilichotuathiri. Na ukija kutazama katika mizigo mingine hususani ya mafuta mpaka katika nchi za Rwanda na Burundi kwa mujibu wa takwimu ambazo zimo katika kitabu cha bandari kwamba nayo pia ilipungua. Lakini ukiangalia katika nchi nyingine zimeongezeka sasa hili nilikuwa naomba tutafute sababu hasa ili tunapotibu basi tujue tunatibu kitu gani ambacho mahususi moja kwa moja kitakuwa kinatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninataka kulizungumzia amelizungumzia Mheshimiwa Kingu pale kwamba kuhusiana na fedha ambazo zimo katika uchumi wetu. Tunafahamu Serikali imepanga kukopa ndani, lakini moja katika changamoto ambayo Serikali yenyewe ilieleza kwamba kutoshiriki kwa sekta binafsi katika uchumi imefanya kwamba uchumi kutokukua vizuri au mambo kutokwenda sawa.

Sasa tunapoamua kukopa ndani vilevile tutasababisha hali hiyo hiyo ya kwamba fedha zitakuwa hazipatikani kwa wananchi na baadaye hawa watu binafsi hawataweza kukopa, kwa hiyo na sekta binafsi nayo itarudi katika changamoto yake ile ile ya kwamba itaanguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naishauri Serikali iharakishe suala la kupata ile dhamana ya Kimataifa kukopa kuweza kufanya *sovereign rating* kwa haraka ili tuweze kupata mikopo ya nje. Lakini pia si vibaya kwakuwa soko letu la hisa la *Dar es Salaam Stock Exchange* linakubali kualika *foreign investors* ambao labda Serikali nayo ijielekeze katika kukopa kwa *foreign investors* ingawaje changamoto zake zinajulikana kwamba ufanisi katika soko lile pamoja na vitendea kazi siyo vizuri kwa muda huu, lakini tutakapotumia njia hiyo, kwa hiyo, tutaweza kupunguza kukopa ndani na baadaye tutajielekeza katika masuala mengine ambayo ya mikopo mizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ni muhimu sana ambalo wengi walilizungumzia, Serikali ingeweka utaratibu uliowazi kufahamu shughuli zinazofanyika. Wengi wanaozungumza hapa wanalalamikia utaratibu wa Serikali kutifikisha fedha katika masuala ya dawa, katika Halmashauri na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa mujibu wa *report* ya BOT ambayo wameleeza kwamba katika mwezi wa Agost, Serikali ililipa zaidi ya shilingi bilioni 900 ili kulipia Deni la Taifa. Katika mwezi wa nyuma yake Serikali iliipa hizo *report* zimo katika mawasilisho ambayo yalifanywa na Gavana wa Benki Kuu tarehe 25 Agosti. Kwa hiyo, hii ndiyo imepelekea kwamba Serikali kutopata fedha za kutosha katika kuhudumia masuala mengine sasa hapa ikafikia kipindi ambacho watu wakaanza kuisema Serikali vibaya na hapa na mimi ninaomba kidogo niongee neno moja ingawa kwamba kwa wengine itakuwa siyo zuri lakini neno lenyewe ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ambaye yupo hai akatafuta kurehemewa na maiti. Narudia tena, mtu ambaye yupo hai hawezi kutafuta rehema kwa aliyefariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu hapa alizungumza kwamba hii Serikali imefilisika lakini akasahau Serikali hii ndiyo iliyompa yeye majengo bila kulipa akawa anafanya biashara. Sasa kama mfu ndiyo wewe unamtegemea akurehemu, sasa wewe mwenyewe ni mfu zaidi ikiwa aliyekufadhili amefilisika ina maana kwamba wewe uliyefadhiliwa umefilisika zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemu wa kiswahili ambao una lafudhi ya Kiarabu ambao unasema *wafadhilaka wasajidaka, man-fadhilaka wasajidaka*, aliyekufadhili ni bwana wako na sio pundaka; sio punda wako. Kwa hiyo, Serikali

bado atabakia bwana wake huyo ambaye amefadhiliwa na Serikali hii, kwa hiyo, Serikali haijafilisika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ni muhimu nazungumza masuala ya *retention* ambayo pia yameshazungumzwa. Nakumbuka moja ya hoja ambayo Serikali ikaamua kufuta *retention* kwa taasisi zile ambazo zimefutwa *retention* kwa sababu Serikali ilikuwa ikikopa pesa zake wenyewe. Zile taasisi zilikuwa zikiweka pesa benki baadaye Serikali inapopeleka dhamana zake kuuza katika masoko ya hisa, mabenki haya yananunua ambayo ni fedha za taasisi za hii Serikali, kwa hiyo ikaamua kuzitoa kuziweka huku. Sasa ufanyike utaratibu ambao uko mzuri na muafaka ili iweze kupatikana urahisi zaidi kwa fedha hizi kuingia katika mzunguko au Serikali yenyewe kama iliona taabu kukopeshwa na mabenki katika *retention* ambayo ziko BOT sasa je, Serikali ina mpango gani kuzitumia hizi? Labda pengine nazo zinaweza zikasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na suala moja ambalo ni muhimu sana ni lazima tuangalie *balance* ya *monetary policy* na *fiscal policy* tunajua Wizara ya Fedha inashughulikia masuala ya *fiscal policy*, lakini Benki Kuu inashughulikia *monetary policy*.

Kwa hiyo, vitu hivi viwili ni lazima viwe *balanced* ili mambo yaweze kwenda sawa na tuweze kuepukana na mambo ambayo hayaendi vizuri. Kuna watu walisifu hapa kwamba Serikali iliyopita ya Mheshimiwa Mwinyi ilikuwa nzuri, ya Mheshimiwa Mkapa ilikuwa nzuri, ya Mheshimiwa Jakaya ilikuwa nzuri na hii pia ninaamini wataisifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mshairi mmoja anasema mpende bado yuko hai, pendo lako alipokee, ukimpenda yuko kaburini umelitupa pendo lako hewani, hayo mapenzi yenu mliyoyataja hapa mmeyatupa hewani lakini tunaamini kwamba na huyu mtampenda. (Makofi)

Sasa jambo lingine ambalo ni muhimu na kama tutalifanyia kazi itakuwa vizuri. Mheshimiwa Khatib pale alizungumza jana kitu kizuri kidogo hata kile kitu nimekipenda. Anasema kwamba alikiombea dua chama chake na akasema kwamba kuna watu wanakiombea kife, hawakiombei kife, mfano wa mtu ambaye ananyeshewa na mvua, tuseme unanyeshewa na mvua baadaye akatokezea mtu akakwambia njoo ujifiche kwenye jeneza unakufa, unajjua? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niongee masuala mawili ambayo muhimu. Katika...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. (Makofi)

Mheshimiwa Chumi, ajiandae Mheshimiwa Riziki, halafu Mheshimiwa Sugu.

**MHE. DAVID C. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo. Yameshasemwa mengi sana na Wajumbe ambao wametangulia kwa hiyo nisingependa kurudia ningenda kwenye *some specific issues*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo ninapenda kuliweka wazi na kulisemea ni suala la watu kulipa kodi. Kodi katika Taifa lolote ni kama vile *nerves* za fahamu za mwanadamu. Kwa hiyo, kodi kwa kweli lazima kodi ilipwe, hilo halina mjadala, hata mataifa makubwa ambayo wakati mwingine yanatusaidia kama wahisani au kwa mikopo zile ni kodi za wale wananchi, kwa hiyo, linapokuja suala la kodi kwa kweli kusiwe na mjadala kodi lazima zilipwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuje namna gani sasa ya huo ulipaji wa kodi, nitaanza kwa kusema katika hali ya kawaida kabisa ukusanyaji wa kodi lazima uendane sambamba na elimu kwa walipa kodi. Leo hii wananchi wetu kwa kukosa ufahamu pale Mafinga mwananchi amedunduliza, ameua gobo (mahindi yale ya kuchoma ambayo yanavunwa bado mabichi), amepata kibali amevuna mbao ameua, amenunua gari lake labda kwa mtu "A", keshokutwa TRA wanamkamata kwamba wewe bwana ulinunua hili gari hukulipa kodi, hukulipa *capital gain*, sawa ni sheria lakini mtu huyu kumbe hana ufahamu wa lile jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye akinunua gari, akaandikishana mkataba na aliyemuuzia akampa kadi yeye anaona ameshamaliza, sasa kumbe hata hawa walipa kodi wadogo wadogo hebu TRA sambamba na ukusanyaji twende na elimu pia ya ulipa kodi kwa sababu hata sisi wenyewe Wabunge wengi tunapotaka kama unafanya biashara masuala ya kodi lazima utatafuta mshauri wa kukuelekeza katika suala zima la kodi.

Kwa hiyo, tupeleke elimu kwa watu hawa sasa mtu huyu kama nilivyosema amenunua gari lake, ameamua kufanyabiashara ya kusafirisha watu, kumbe hajui ukitaka iwe gari ya biashara kuna taratibu zake pia za kikodi gari inakamatwa, ameshajimaliza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, TRA the way wanakuja yaani hawaji kwa ile elimu kwamba *you are supposed to do this* ili uwe katika njia hii hapa. Yaani wanakuja kwa namna ambayo ni ya *ambush*. Kwa hiyo, kama nilivyosema

sipingani, kodi lazima ilipwe, lakini pia jitihada za kukusanya kodi ziende sambamba na elimu ya kuwaelimisha wananchi kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili hizi *machine za EFD* kwanza hazijasambazwa vya kutosha, lakini leo nilikuwa nasoma kwenye gazeti, Sheria ambayo sisi wenyewe *of course* tulipitisha kama hujadai risiti kuna *fine* utapigwa pale lakini mashine nyingi ninyi wote mashahidi unaenda, oh, mtandao uko chini mashine haifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri hebu tusaidie hii ilikuwa ni *deal* ya watu au kweli wenye biashara mashine ni mbovu? Lakini shaka yangu kwamba hizi mashine yawezekana toka mwanzo hazikuwa mashine madhubuti. Sasa hawa wanao-*supply* tumejiridhisha kweli wana-*supply* mashine za *EFD* zinazotakiwa? Kwa hiyo, tunaweza tukajikuta siku tunashurutisha watu kumbe mashine yenyewe hatujazisimamia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie, elimu ya kulipa kodi ina umuhimu wananchi toka lile tangazo la Mheshimiwa Magufuli na tangazo la kale katoto nipe na risiti, imewaingia watu mpaka watoto wangu nikinunua gazeti tu wananiambia baba mbona hujadai risiti? Lakini sasa kama elimu imeanza kuwaingia hivyo ya kudai risiti na mashine hazifanyi kazi kwa wakati, mtandao uko chini, je, tutafikia malengo ya Mpango? Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri ulitazame hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la Liganga na Mchuchuma, amesema hapa ndugu yangu asubuhi, Mheshimiwa Sixtus Mapunda. Mimi hujizuia sana kuleta mambo ya Ukanda, lakini katika hili naungana naye au kwa sababu liko Kusini?

Mimi natoka Nyanda za Juu Kusini, bahati mbaya inaweza kuwa bahati mbaya au nzuri nilifanya mazungumzo na Balozi wa China kwa ajili ya mambo ya jimbo langu. Kati ya kitu ambacho hata Ubalози wa China unasikitika mojawapo ni suala kulegalega suala la Mchuchuma, kulegalega suala la Bagamoyo na Mheshimiwa Waziri katika kitabu chako umesema hii ni miradi ya vielelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yawezekana kuna watu wengine wamesoma zaidi, wanaufahamu wa mambo haya lakini pia ni vizuri sana kutumia elimu yetu kuhakikisha kwamba tunalisaidia Taifa kusonga mbele pale ambapo tumekwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano naambiwa katika suala hili, yule mbia ambaye ana ubia pamoja na *NDC* fedha za kulipa fidia wananchi wa Ludewa kule kwa ndugu yangu zimeshapatikana na zipo. Lakini mgogoro

unaambiwa upo kwenye *power purchasing agreement*, sisi tunataka tununue kwa senti saba za dola wao kwa senti 13; lakini ukiangalia mradi ule katika ujumla wake, lengo lake zile *megawatt 600* ni katika kutusaidia sisi tupate umeme. Lakini mradi wenyewe katika ujumla wake kama alivyosema Mheshimiwa Mama Nagu unaenda kusaidia ku-*stimulate* viwanda vingine. Tunataka sisi kujenga reli hapa, hayo mavyuma tutayatoa kule. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nikuombe kwenye suala la Mchuchuma tulipokwama tuone tunatoka wapi tuweze kufanikisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kwa kushirikiana na Wizara ya Mamboya Nje, tusiwe nchi ya kusaini tu ma-MoU, alikuja hapa Rais wa China mara baada ya kuapishwa ni nchi ya kwanza duniani kuitembelea tumesaini mikataba 16, juzi tumesaini na Morocco, je, *follow up* iko wapi ya kila mkataba tuliosaini utakuwa na tija kiasi gani, tumekwama wapi, nani amekwamisha? Ili kusudi dhamiraya mpango huu iweze kutimia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie muda wangu naona unaniishia kuhusu suala la kilimo, katika Mpango huu hakuna mahali popote palipo *reflect* suala la kilimo kama ambavyo Mpango wenyewe wa Miaka Mitano unasema. Sasa niombe tujaribu kuwekeza katika kilimo hiki na tusaidie pia Shirika la Maendeleo ya Viwanda vidogovidogo *SIDO* kwa ajili ya kitu kinaitwa *knock down technology*. Juzi tumeona wakulima wa nyanya wanauza nyanya ndoo mpaka shilingi 800. Sasa wakati tuna-*deal* na mamiradi makubwa hebu pia tuone namna gani tunaweza kukinyanyua kilimo kwa namna ya kawaida, tukashirikiana na *SIDO*, tukajenga viwanda vya kawaida, tuka-*add value* katika mazao ya wakulima ili kusudi hawa wakulima kweli waonekane ni uti wa mgongo wa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni *single custom territory* watu wengi wamesema; na mimi kwa ufahamu wangu ningeshauri sana Congo DRC tuwape *special treatment* ndugu zangu. Sisi *single custom territory* tu-*deal* nayo na sisi hapa EAC. Lakini hawa watu ambao *volume* yao kibiashara ni kubwa hebu wao tuwape *special treatment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya nimalizie kwa kusema wako watu wanaosema pengine Mawaziri wanaogopa kumshauri Rais, sidhani kama kuna kitu cha namna hiyo. Hawa ni watu wenye *confidence*, wenye kujiamini katika kazi, tuwape nafasi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Riziki.



**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi aliyetujaalia sisi sote uzima na afya na akatupa upendeleo maalum kutuweka kwenye jengo hili tujadili kwa niaba ya Watanzania mamilioni kile ambacho kina mustakabali mwema kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nisome tafsiri ya maandiko matakatifu kutoka kwenye kitabu wanachofuata Waislamu cha Qurani na kiongozi wao Mtume Muhammad (SAW). Kuna hizi aya mbili, moja wapo nakumbuka nilishawahi kuisema hapa lakini nitairudia tena, ya kwanza iko katika Sura inaitwa *Sura Hajj* ni aya 46 ambayo inasema; "Hivi hawatembezi katika ardhi, wakawa nyoyo ambazo wanafahamu kwa nyoyo hizo? Au masikio wakasikia kwa masikio hayo? Kwa hakika yanayopufua si macho bali ni nyoyo zilizomo ndani ya vifua."

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna aya nyingine iko kwenye *Sura Araf* na ni aya ya 179 hii inasema; "Hakika tumeumba moto wa Jehanum kwa ajili ya watu wengi na majini pia kwa sababu..." wataalam wanasema pale kiunganishi "...kwa sababu wana nyoyo lakini hawafahamu kwa nyoyo hizo, wana macho lakini hawaoni kwa macho hayo, wana masikio lakini hawasikii kwa masikio hayo, hao ni sawasawa na wanyama bali wao ni wapotevu zaidi kuliko wanyama kwa sababu hao ni wenye kughafilika." Hadithi ya Mtume (SAW) ikasema; "mapambano yaliyo bora zaidi ni neno la haki mbele ya mtawala jeuri." (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtawala ana ngazi, tunaweza kumzungumzia Rais, mkuu wa utawala wa muhimili mmoja naweza kuwa Spika na wasaidizi wake muhimili mwingine, anaweza kuwa Jaji Mkuu na wengine wanaomsaidia. Lakini pia kwenye ngazi za Mawaziri na wote ambao kwa pamoja wanatengeneza utawala. Katika wazungumzaji mmoja jana alisema; "Aah! nina wasiwasi kama vile hatuelewi tunachotakiwa kufanya kwa sababu kila anyesimama analalamika," hatulalamiki, ndiyo tunachangia! Na ile inakuja kwa sababu ya hali halisi. Tulisema mwaka huu huu tukipitisha, tukijadili bajeti kwamba jamani mbona hapaoneshi kwamba kuna *integrated system* ya haya tunayo yajadili? Wa viwanda akisimama anaruka ruka, anachachatika, hatuoni viwanda! Akisimama wa Miundombinu na Maji utadhani maji yatatoka kesho kwenye mfereji wanasema jamaa zangu, hakuna kitu! Akisimama wa usafiri ATC imefufuliwa, *Bombardier* zimenunuliwa, ziko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Mafia siku chache kabla ya kuanza vikao vya Kamati nikawapigia simu watoto wangu nyumbani hebu harakisheni ATC mkanifanyie *booking* ndege ya Dodoma. Wakaniambia mama hazijaanza kwenda! Aaah! Mimi nilidhani ndiyo ingekuwa kituo cha mwanzo hapa! Wateja tupo wengi wa uhakika, haipo. Lakini hii Mpango unasema tena kufufua ATC

watu wanapiga makofi, watu wanashangilia, jamani hebu tuone kwa nyoyo zetu kwa sababu ni hizi nyoyo ndiyo zilisimama pale zikaapa. Kila mmoja wetu na katika kiapo kile tunaweka ahadi na huyo mwenye mamlaka zaidi na pia ndiyo tunakubali kwamba hayo mamlaka yapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kupitia kwako hebu tuzingatie ile sala tunayoomba hapa kila asubuhi, lakini pia kupitia kwako hebu jengeni mazingira ya kuwa tunamkumbuka Mwenyezi Mungu kila wakati, labda itatujengea hofu na kusema kweli tuna dhima kubwa hapa ndani ya jengo hili, isiwe ushabiki tu! Tunasema jamani haya mambo yako so *broad!* Yaani ni mapana kiasi kwamba inasikitisha hata kusoma, alisema msemaji hapa kwamba huu ni mwaka wa pili na ni mwaka mmoja, kulikuwa na mwaka kabla yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, laiti tungepata *assessment* ya mwaka ule japo miezi michache tu ile ndiyo ikawa msingi sasa wa kufanya huu mwaka huu, humu *background information* nadhani kuna majedwali mengi hapa ukurasa wa 18 mpaka 24; hivi unapozungumzia mpango wa mwaka mmoja tu mwaka wenyewe ni 2017/2018 unapotoa *data* za mwaka 2013 ambazo wala hazisaidi hata ule Mpango wenyewe wa miaka mitano ambao mkubwa ndiyo ukatolewa huu mdogo. Sasa nikasema huu ni mpango wa mwaka huu au ni nini na tatizo ni nini? Ndiyo hiyo *copy and paste* au ni kwamba taarifa tu ilimradi buku lijae iletwe? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hatutendei haki, tuletewe mpango ambao ni mahsusi na niliposema hapa kikao kilichopita kwamba mbona hamna kile wanachoitwa wataalam *measurable targets* yaani tukiangalia hapa tunasema hapa tumesema mwaka huu tutatoka *point* moja twende *point* mbili. Niliguswa zaidi wakati ule na suala la afya na nikasema mahsusi suala la vifo vya akina mama linalotokana na uzazi, wakati ule kulitokewa na *figure* pale, sijui 400, kati ya watu 100,000, nikawauliza jamani sasa kwa mwaka huo mmoja mmepanga kitu gani hapa? Mbona ni namba tu ambayo haina mwelekeo wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliposimama mjibu hoja, akasema jamani kweli hamna humo tena kwa ile sauti yake kama vile kaonewa au mtu anasema uongo, sasa mara hii ndio limekuja *broad* kabisa, katika ukurasa 54 mpaka 55 kipengele 6.4.2 afya na ustawi wa jamii wanasema kupunguza vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi basi mara hii hata namba hamna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vyenyewe peke yake viko aina chugu nzima hivyo vifo vya uzazi viko aina chungu nzima, kwa mwaka huu ni vifo gani mnavitarajia kuvifanyia kazi, na kutoka vingapi mpaka vingapi huu mwaka mmoja tu, mbona haya mambo yanakuwa hivi jamani halafu mnasema

tunapanga na kuna wanaosema maneno wanasema *if you fail to plan, you plan to fail*. Tukishindwa kupanga ina maana tunapanga kufeli au kushindwa, hivi kweli Taifa hili tunakaa watu mamia humo tumeacha mambo mengine yote kuja kujadili hili, jamani hebu tuitendee haki nchi hii, hebu tuwatendee haki wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu haukubali kwamba hali ya uchumi umeshuka jamani kwa ukweli wa dhati ya mioyo yenu hivi kweli Watanzania wangapi sasa hivi wana *purchasing power* ambayo inafanana kidogo tu na ile ya mwaka jana, yaani ule uwezo tu wa kumiliki yeye maisha yake mwenyewe kwa kile kipato anachokipata kuanzia mama ntilie mpaka maprofesa wa chuo kikuu, ni wangapi kweli *purchasing power* yao ni kweli inawawezesha hawa kuishi maisha ya kuaminika au maisha angalau kidogo yanampa mtu ahueni, akasema nina mshahara, nina kazi, nina kibarua, nina kipato cha kuaminika. Tunafanya uigizaji sekta isiyo rasmi kila mtu ajiijiri, sekta isiyo rasmi inajengwa na sekta iliyo rasmi. Viwanda vinaeleweka, wafanyakazi idadi fulani inaeleweka, mshahara wao unaeleweka kwa hiyo tunajua kiasi fulani cha pesa kitaingia kwenye mzunguko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuweki mambo tu hivi hivi, na ndio maana hata huu mpango wenyewe wote ukasimama wanasema wasemaji matofali ya barafu ambayo wala hayajengi nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mambo yanayotajwa kwamba ni msingi ambao mpango huu umesimamia ni amani, usalama, utulivu ndani ya nchi kweli. Nchi hii ina amani? Wataalam wa amani wanasema *peace is not the absence of war* yaani kukosekana vita sio kwamba mna amani, lazima kuwepo na mifumo mizuri ya kijamii ambayo ina mhakikishia kila mtu haki yake inampa utulivu, inamhakikishia maisha yake ya kila siku, nani nchi hii leo hii, Mbunge hana uhakika kama nikitoka hapa Dodoma nitafika Dar es Salaam bila kukamatwa na askari, nitadaiwa pesa isiyokuwa na mbele wala nyuma. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa George Mwakajoka, ajiandae Mheshimiwa Bura, ajiandae Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2017/2018 pamoja na Mwongozo wake.

Ningependa nianze moja kwa moja na upungufu wa mizigo kwenye bandarii yetu ya Dar es Salaam. Nilikuwa nafikiri ni vizuri zaidi Serikali hii ikajikita

kukubali kushauriwa na Waheshimiwa Wabunge wanavyotoa ushauri wao, na pia niwashauri sana Wabunge wetu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tujikite kwenye majukumu yetu ya kuishauri Serikali na kuisimamia Serikali. Kazi ambayo inafanyika sasa hivi kwenye Bunge hili ninaifananisha sana na picha za zamani za kihindi ambazo wakati boshi anatembea, alikuwa anatembea na watu walikuwa wanaitwa masuzuki, yule Suzuki alikuwa anakaa pembeni kwa boshi na boshi akigeuka tu hata akikohoa yeye anaondoa miwani kwenye macho akifikiri ameitwa au anaagizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri sana tukapunguza uoga na tukasimama kwa miguu yetu kama Wabunge ili kulisaidia Taifa hili. Taifa hili lina watu wengi ambao wamepewa majukumu, ni wasomi wazuri, lakini pia ni wataalam ambao tumewaweka kwenye Wizara mbalimbali kuhakikisha kwamba wanaisaidia Taifa. Wataalam hawa tumefika mahala sisi wanasiasa tumeanza kuwaingilia, wameshindwa kutekeleza wajibu wao kufuatana na utaalum unaowaruhusu waweze kufanya kazi hizo. Jambo hili tukubaliane kwamba Taifa hili haliwezi kwenda kwa mtindo huu kama wanasiasa tutaingilia shughuli zote za kitaalam na sisi tukawa kwenye maagizo badala ya kuangalia ni namna gani tunaweza tukaishauri Serikali na kuhakikisha kwamba Serikali inatekeleza wajibu wake ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi huwezi kuamini, nchi imebaki ni nchi ya matamko kila mmoja anatoa matamko pale anapoweza, hakuna mwongozo unaoonesha kwamba ni nani anatakiwa kufatwa hapa. Wataalam wetu sasa hivi wameshashuka thamani na utaalum wao hauieleweki tena kwa sababu ya sisi wanasiasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka sana wakati Mheshimiwa Rais ameapishwa na wakati anaanza kutembelea wadau mbalimbali kujaribu kupata mawazo alikutana na wafanyabiashara katika nchi hii. Wakati anakutana na wafanyabiashara kwenye nchi hii jambo la kwanza alilolizungumza aliwauliza ni nani mmoja wenu aliyenichangia hata shilingi moja wakati wa kampeni. Swali hili lilikuwa ni swali gumu sana kwa wafanyabiashara ambao waliitwa wakitegemea kabisa kwamba Mheshimiwa Rais angeweza kuwashukuru pia kwa kazi kubwa waliyoifanya kuhakikisha kwamba wanaendeleza viwanda vyao, wanaendeleza biashara zao na wanalipa kodi katika Taifa hili mpaka alipolikuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini aliwauliza swali tu kwamba nani ambaye amewahi kunichangia wakati niko kwenye kampeni aseme hapa, tafsiri yake ni nini? Alikuwa anaweka gape, anatengana na wafanyabiashara na sasa hivi ndio maana baada ya muda mchache alitangaza wafanyabiashara wengi ni watu ambao wanaihumu Serikali, ni wezi na ikaonesha kabisa kwamba Taifa

hili linaonesha kabisa kwamba wafanyabiashara wote katika nchi hii ni watu ambao hawaaminiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lolote duniani kama halitawathamini wafanyabiashara na kukaa na wafanyabiashara na kubadilishana na wafanyabiashara mawazo ni namna gani Taifa lao liende, Taifa hilo haliwezi kupiga hatua hata siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilichokuwa nataka kukizungumza hapa nilikuwa nataka kusema kwamba ni lazima sasa Mheshimiwa Rais, lakini pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kurudi kukaa na wafanyabiashara, hakuna Taifa lolote linaweza likaendelea kwa sababu ya kutangaza kwamba yeye anapenda maskini, hakuna maskini anayependa kuwa na njaa, si siku nyingi maskini huyo akiwa na njaa akikosa dawa atamgeuka Mheshimiwa Rais kwa sababu hawezi kukubali kuendelea na mateso wakati anajua ana haki ya kupata maisha bora katika nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni mara nyingi sana wadau mbalimbali wanajaribu kutoa ushauri. Ninakumbuka sana Bandari ya Dar es Salaam tumezungumza mimi ni mjumbe wa Kamati ya PIC, tumezungumza sana tukiwa na Katibu wa Uchukuzi tukamweleza athari ambazo zimetokea kwenye Bandari ya Dar es Salaam, wateja ambao walikuwa wakitumia Bandari ya Dar es Salaam wakubwa ilikuwa ni Kongo pamoja na Wazambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Tunduma niko pale Tunduma, kwa takwimu za mwaka 2014/2015 kwenye nchi hii asilimia 71 ya mizigo inayoshuka kwenye Bandari ya Dar es Salaam inapita kwenye mpaka wa Tunduma, lakini leo hii ukienda kuangalia tulikuwa na foleni ya malori karibuni kilometa nane ili kuvuka mpaka lakini leo huwezi kukuta gari hata moja liko barabarani limepanga foleni wanasema hali ni nzuri wakati hali bado ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wana Tunduma tumeathirika lakini pia Taifa tunaliona linaathirika kupita kiasi sasa wadau mbalimbali wanajaribu kutoa ushauri nakumbuka Mheshimiwa Sugu hapa alisema ndani ya Bunge hili akasema mtindo huu ambao Serikali imeanza kufanya kazi ya kuikusanyia Serikali ya Kongo kodi ni jambo ambalo linasababisha wateja wengi wa bandari yetu wakimbie waende Beira, waende Mombasa lakini pia wengine wameenda hadi Durban wanapitia kule japokuwa ni mbali lakini wameona afadhaili wapitie kule, hatukuweza kusikiliza tukaendelea kukomaza shingo zetu mpaka bandari inataka kukatika hapa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ndugu zangu, ninakumbuka sana wafanyabiashara pamoja na wadau wa bandari tuchukulie watu wa TATO. Watu wa TATO wamejaribu kuishauri Serikali mara nyingi, wameishauri Kamati ya Viwanda na Biashara, wakawaeleza wakasema tatizo kubwa la upungufu wa mizigo hapa ni tatizo la Serikali kutokusikiliza ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo walizungumza walijaribu kutoa mfano wa kampuni moja tu ya Impala ambayo ilikuwa ikipitisha kwa mwezi mzima tani laki tano kwenye bandari ya Dar es Salaam. Wakasema magari ambayo yalikuwa yakipakia mzigo na kwenda kupakuwa mzigo Kongo yalikuwa ni zaidi ya 30,000 kwa mwezi na magari haya yalikuwa yakitumia lita 2,500 kutoka Dar es Salaam kwenda Lubumbashi kwenda kuchukua copper na kila lita moja ya mafuta Serikali ilikuwa inachukua shilingi 600 kwa ajili ya kodi, lakini pia wakasema kwamba copper tani moja walikuwa wanalipa dola 600 kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam lakini leo hii hakuna kinachoendelea na juzi kwenye takwimu za Durban imeonesha Kampuni ya Impala imesafirisha tani laki saba kutoka Kongo na Zambia wamekwenda kupita kule kwa sababu ya ukiritimba tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana mambo ya uchumi hayana utani, nchi za wenzetu zilizoendelea tunazoziona zina maendeleo mazuri si kwamba zinacheza na uchumi, uchumi sio jambo la kucheza nalo, leo watu wanasimama, Mheshimiwa Rais anasimama, Waheshimiwa Mawaziri wanasimama wanasema hata ikija meli moja, kauli hizi kwa kweli zinafika mahala zinawakatisha tamaa Watanzania na wanafikiria hawa ni viongozi kweli ambao tumewatanguliza kwa ajili ya kuleta ustawi wa Taifa hili. Ndugu zangu haitawezekana ukipata meli mbili au tano badala ya kupata meli 20 mpaka 30 huwezi kufananisha hata ungepandisha ushuru kiasi gani ni lazima tutakuwa na hasara katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndio maana leo tunazungumzia uchumi kushuka kwenye Taifa hili watu wanakomaa hapa wanasema uchumi haujashuka wakati huduma za jamii, fedha katika Halmashauri zetu hazijafika leo watu wanasema uchumi haujashuka katika Taifa hili. Tunataka tuseme ni lazima Serikali ifike ikubaliane na ushauri mbalimbali unaotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni kuhusiana na wafanyabiashara katika nchi hii. Wafanyabiashara wengi sasa wamekuwa na wasiwasi wameanza kuhamisha biashara zao wanakwenda Kongo, Zambia, Malawi na maeneo mengine wanahamisha biashara kwa sababu hawana uhakika wa biashara zao katika nchi hii. Kuna wafanyabiashara ambao wamekamatiwa mizigo yao, kuna wafanyabiashara ambao tayari wamefungiwa akaunti zao bila sababu za msingi na bila taarifa za msingi na wanafunguliwa akaunti bila kuambiwa nini kilichoendelea, jambo hili

wafanyabiashara wamekuwa na wasiwasi wameona kabisa Serikali hii inaonesha kabisa haiwezi kuwatendea tena haki na wanaamua kuhamisha biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nikwambie tu takwimu zilizopo ukienda nchini Zambia kuna Watanzania zaidi ya milioni tatu wameamua kwenda kufanya biashara Zambia, lakini Malawi kuna Watanzania zaidi ya milioni moja na laki tano wanafanya biashara kule Malawi. Serikali imekaa kimya wanalipa kodi kule wananemesha nchi ya Malawi na Zambia kule Serikali imekaa kimya kwa sababu ya masharti magumu ambayo Serikali imeweka. Nataka nitoe mfano mmoja wa masharti ambayo Serikali inatakiwa iyatazame. Mimi niko mpakani mwa Zambia na Tanzania ukilipia mzigo wako eneo la *custom* pale ZRA - Zambia ukiondoka kwenda kufika Lusaka mzigo ule watu wa ZRA wanakuja kuchunguza risiti zako kama umelipia vizuri na mzigo ndio ule uliolipia, wakikuta mzigo ndio uliolipia wanachokifanya wao ni kukuruhusu ushushe mzigo na uendelee kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tanzania mtu anatoa mzigo nje akishafikisha kwenye Bandari ya Dar es Salaam analipa ushuru, akishauchukua ule mzigo anafika Kariakoo watu wa *TRA* walewale wanakwenda kuchukua kodi, anatoka pale anakuja mtu wa Mbeya ananunua mzigo watu wa *TRA* walewale wanakwenda wanachukua mzigo ule kodi, anatoka pale anapeleka; mtu ananunua Mbeya pale anapeleka Sumbawanga watu wa *TRA* walewale wanakwenda kuchukua kodi, mzigo unatoka Sumbawanga mtu wa Nkasi anakwenda kununua mzigo mtu wa *TRA* yule yule anakwenda kufata mzigo Nkasi, ni sheria za wapi za kukusanya kodi katika dunia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ndiyo vikwazo vikubwa vya wafanyabiashara katika nchi hii, ni lazima tufike mahali nchi yetu tunaipenda na hatuna nchi nyingine ya kukimbilia zaidi ya nchi hii; na sio nchi ya mtu mmoja ni nchi ya Watanzania wote tunahitaji kuipigania na lazima Wabunge tushikamane kwa jambo hili tuzungumze kwa nguvu zetu zote ili kuboresha uchumi wa nchi hii wananchi wetu waweze kupata madawa watoto wetu waweze kusoma na shughuli zingine ziweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilikuwa najaribu kujiuliza elimu bure Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaonesha ni jinsi gani ilivyofeli kwenye elimu bure. Wakati tunafanya mahesabu imeonesha kabisa kwamba karibuni shilingi bilioni 15.7 zinakwenda kila mwezi kwa ajili ya kulipia gharama za elimu bure kwa watoto 8,340,000; tafsiri yake ni kwamba kila mtoto anapewa shilingi 1,884.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inasema kwamba kila mtoto wa shule ya msingi anatakiwa kulipiwa shilingi 10,000 tunataka kujua shilingi 8,116 zinakwenda wapi na zitapatikana namna gani *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama kweli bajeti ni shilingi bilioni 15.7 tafsiri yake ni kwamba ukifanya mahesabu ya haraka haraka kwa watoto 8,342,000 utakuta ilihitajika fedha bilioni 83 kwa mwezi lakini inapelekwa bilioni 15 leo mnatuambia kwamba huduma za watoto mashuleni zinakubalika, kazi hiyo haipo, Serikali imeshindwa na iwaambie wananchi kwamba imeshindwa na mzigo huu wananchi waendeleo kuubeba mzigo huu. Ndio maana madarasa sasa hivi hayajengwi, ndio maana ukienda ukiona msongamano wa watoto unazidi kuongezeka kwa sababu Serikali imewadanganya wananchi na kazi haifanyiki hata kidogo katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tulikuwa Bungeni humu, tukaishauri Serikali tukasema kitendo cha kuwaambia watumishi wakusanye ushuru kwenye Halmashauri zetu *manpower* ya watumishi wetu ni wachache katika Halmashauri zetu, tukasema hili jambo litakuwa ni gumu, leo katika Mji wa Tunduma ambapo kwa kipindi hiki cha mavuno tulikuwa tunakuwa na asilimia 40 mpaka 45 ya makusanyo leo tuna asilimia 18 tu, leo hii tumekaa hapa vyanzo 42 havijakusanywa hata shilingi moja ukimuuliza Mkurugenzi anasema watumishi ni wachache siwezi kuwagawa watumishi katika Halmashauri yangu. Serikali ikafidia fedha hizi ili tuweze kufanya maendeleo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusiana na kilimo, nilikuwa najaribu kuangalia kwenye Mpango huu naona kabisa kwamba kilimo kinaendelea kushuka... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ya leo na ninakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kabla sijasema lolote basi, niunge mkono hoja hii kabla sijasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1973 Wabunge wenye akili timamu, wenye uwezo walikaa pale Karimjee wakaamua kwamba Makao Makuu ya nchi hii yaje Dodoma na tangu kipindi hicho Marais waliopita wamefanya kazi kubwa, Rais wa Awamu ya Kwanza amefanya kazi kubwa, Rais wa Awamu ya Pili amefanya kazi kubwa, Rais wa Awamu ya tatu amefanya kazi kubwa, Rais wa Awamu ya Nne amefanya kazi kubwa na Rais wa Awamu ya Tano ameamua kutekeleza yale ambayo yaliamuliwa mwaka 1973. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania kwa ujumla pamoja na sisi wananchi wa Dodoma tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa maamuzi haya. Wametokeleza dhamira ya wananchi kwa sababu ukitoka hapa Dodoma mpaka Kagera unafika siku hiyo, ukitoka hapa mpaka Songea unafika siku hiyo, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa dhamira hii ambayo wameamua kuhamia Dodoma kwa awamu na sisi tunawaunga mkono na mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge ambao wana uwezo wa kujenga mahoteli, wana uwezo wa kujenga viwanda, wana uwezo wa kufanya miradi mbalimbali tunawakaribisha Dodoma. Kuna ardhi ya kutosha, barabara zinapitika, ukitaka kwenda Singida utakwenda kwa lami, Iringa utakwenda kwa lami, Arusha utakwenda kwa lami na Dar es Salaam utakwenda kwa lami. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nianzie hilo kwamba tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano, lakini niombe kwa Serikali hii kwamba CDA waliopewa mamlaka ya kustawisha mji huu hawana fedha, wanatakiwa kujenga barabara, wanatakiwa kupima viwanja, wanatakiwa kuhakikisha kwamba *squatter* hakuna hapa, wanatakiwa kuhakikisha kwamba hakuna foleni kama Dar es Salaam lakini hawana fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu ambao umeletwa sikuona kama CDA wametengewa fedha yoyote kwa ajili ya kupanga Mji wa Dodoma. Nimeangalia katika kitabu chako ukurasa wa 51 kanda maalum ya kiuchumi sikuona kama Dodoma imewekwa katika kanda maalum kiuchumi. Kwa sababu watakojenga viwanda katika Mkoa wa Dodoma watataka ardhi, lakini ardhi hii wanaipataje kama wenye ardhi hawatalipwa fidia, watapataje ardhi kama nyumba za wanakijiji hazitalipiwa fidia. Kwa hiyo, kuna haja ya kuweka Dodoma katika kanda maalum ya kiuchumi ili Serikali itakapoamua sasa kuhamia na wafanyabiashara mbalimbali watakapoamu kujenga Dodoma basi iwepo fedha kwa ajili ya kutenga maeneo, iwepo fedha kwa ajili ya huduma mbalimbali, huduma ya maji taka, huduma ya maji, barabara, upimaji wa ardhi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie sasa Mpango ambao uko mbele yetu. Nimeona kwenye Mpango maeneo mbalimbali yameainishwa na nimeona mazao ambayo yameainishwa ambayo yamepewa kipaumbele, lakini naona haitoshi. Hata mipango iliyowekwa kwa ajili ya miwa, tumbaku, mpunga, lakini bado mazao kama mbaazi, chai, korosho, bado mazao mengi ambayo nilitegemea kwamba Serikali itaonesha mkazo maana asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima. Lakini kama asilimia kubwa hii ya Watanzania hawatawekewa mkakati maalum hakika hatutafaulu kwa haya ambayo tunayategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahamasisha kujenga viwanda, lakini viwanda hivi ambavyo tunahamasisha kujenga tunategemea malighafi itoke ndani ya nchi yetu, lakini viwanda vingi ninavyoona vitakuwa vya mazao sio vya mazao ya mpunga tu au mazao ya chai au mazao ya korosho tu, lakini mazao yako mengi, lakini Tanzania wananchi walio wengi wanategemea mvua. Sasa katika karne hii ya tabia nchi inayobadilika kila siku ifike wakati kwamba tusitegemee mvua, lazima tuhakikishe kwamba kilimo cha umwagiliaji kinapewa kipaumbele katika mikoa yetu bila kujali mkoa huu una mvua au mkoa huu hauna mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea maeneo kama yale ya Rubada, maeneo ambayo Serikali ilitoa kwa ajili ya kilimo ili kuiwezesha nchi kuwa na mazao ya kutosha. Kule Kasulu kuna shamba kubwa karibu ya eka 10,000 au 5,000 wale wanaotoka Kasulu wanajua tungeweza kuendeleza yale mashamba na tukayagawa kwa wananchi au Serikali ikaona namna ya kuendeleza yale mashamba, ili tunaposema kwamba nchi iwe ya viwanda basi malighafi ipatikane nchini na Watanzania wafaidi kuwa na viwanda katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo haina mtaji wa kutosha kutoa pembejeo au kuwapa wananchi pembejeo, lakini wako wananchi wengi ambao wangependa kulima, wangependa kukopa pembejeo, wangependa kukopa matrekta, lakini benki haina fedha. Na benki ina kituo kimoja tu, kituo kiko Dar es Salaam, ukimwambia mkulima wa Kagera, atoke Kagera, Mara, Kigoma kwa ajili ya kwenda kutafuta mkopo Benki ya Kilimo Dar es Salaam, hakika ni kazi kubwa na anapokwenda Dar es Salaam hana hakika kama atapata huo mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali yangu sikivu iangalie namna ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, lakini ione namna ya kuwawezesha wakulima kusogeza huduma ya benki karibu nao. Nishauri pia kwamba miradi ile ambayo ilikwishanza sasa ndio ikamilishwe kabla hatujaanza miradi mipya, kwa sababu tunapojirundikia miradi mingi wakati fedha hatuna za kutosha tunajikuta miradi mingi imekwama. Kwa hiyo, kuna haja ya kumaliza miradi ile ambayo tulishaanza, lakini tukatoa vipaumbele kwa miradi ambayo tunaona inaweza ikaisaidia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kwamba lazima tujue tunapotaka kuwa na viwanda umeme tunatoa wapi? Je, umeme upo wa kutosha nchini? Ifike sasa habari ya Mchuchuma na Liganga utoe megawatt 600 zile ambazo zimepangwa, lakini tunaweza tukapata wawekezaji wengi tusiwe na maji, tusiwe na umeme wa kutosha kwa hiyo, hata kuhamasisha kwamba, wajenge viwanda itakuwa ni kazi. Watajenga viwanda, lakini watakosa maji, watakosa umeme; kwa hiyo, mambo muhimu katika kuwawezesha hawa wawekezaji ni jambo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini reli ya kati, ili kuhifadhi barabara zetu lazima tuwe na reli ya kati inayofanya kazi vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema nimeshangazwa na maneno ambayo nimeyasikia kwa baadhi ya Wabunge. Kazi yetu Wabunge ni kuishauri Serikali, lakini Mbunge unaposimama na kusema matusi sidhani kama Waziri wa Fedha anaweza akaandika matusi hayo yanayosemwa. Unaposema maneno ya kejeli sidhani kama Waziri anaweza akaandika maneno ya kejeli katika kitabu chake cha Mpango. Kwa hiyo, kwa sababu kazi yetu ni kuishauri Serikali tusimame tuishauri Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka kuanzia mwezi wa nne mpaka mwezi wa sita Bunge lilikaa hapa kujadili Bajeti ya Serikali, lakini wapo wengine ambao waliweka *plaster* kwenye midomo yao, waliishauri Serikali wakati gani? Leo watu wanasimama wanasema tulishauri Serikali kipindi cha bajeti! Tulishauri Serikali hawakusikia! Mimi sikuwaona walioishauri Serikali zaidi ya Wabunge wa CCM. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba tukubaliane na haya ambayo yapo kwa sababu bajeti hii ilijadiliwa na upande mmoja na tukakubaliana kwamba, haya ni sawa. Na leo watu wanachangia baada ya kuona bajeti iliyopitishwa na Wabunge wa CCM ni sawa. Ninaomba kazi yetu Wabunge ni kuishauri Serikali, tuishauri Serikali, tuache lawama, tuishauri Serikali tuache matusi, tuache kubeza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwamba watu wanajua na tumeona katika Majimbo yetu baada ya kusema kwamba elimu ni bure, maeneo mengine darasa la kwanza waliandikishwa watoto 100, maeneo mengine watoto 200. Kwa hiyo, huwezi kusimama ukadharau hili kwa sababu wako wananchi ambao hawakuweza kuandikisha watoto kwa sababu ya michango ya shule. Tunakotoka wananchi wanashukuru kwamba sasa watoto wanasoma kwa sababu wanalipiwa michango na Serikali. Na ninashangaa kwamba wengine walisema vyama vyao vilisema kwamba wangelipa ada mpaka *university*, sasa tunalipa mpaka *form four* wanabeza, akutukanaye hakuchagulii tusi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wako ambao hawaangalii mbele, wanaangalia nyuma siku zote. Zamani watu walibeza wakasema Mheshimiwa Kikwete anachekacheka, Mheshimiwa Kikwete hawezi, leo wanasimama wanamsifu Mheshimiwa Kikwete. Hakika nadhani tuyatafakari na kuchambua yale ambayo tunaona yatalisaidia Taifa letu, tuyaweke yatusaidie katika kuendeleza nchi hii. Tunajua hali ya kodi katika nchi yetu, tunajua Wabunge wamesema, Serikali imesikia, Mawaziri wamesikia, Waziri Mkuu tunaye kwenye Bunge letu amesikia.

Mheshimiwa Waziri...(Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mpango kwa kuleta mwelekeo wa Mpango huu, ili ujadiliwe na Bunge lako na mimi kupata nafasi ya kutoa mawazo yangu, lakini nasikitika itabidi nitumie sehemu ya muda wangu mzuri kuweza kueleza maeneo ambayo pengine yalikuwa *very obvious*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya michango yetu inaonesha kwamba baadhi ya Wabunge tume-panic na Wabunge wengi tulio-panic tunaufanya umma wa Watanzania u-panic. Na ukifuatilia vitu vinavyotufanya tu-panic vinakosa mantiki na leo mbele ya Bunge lako Tukufu nalazimika kuongea kwa kutumia analogia kwa sababu ndio namna pekee ambayo nadhani nitaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka kadhaa iliyopita hapa Dodoma watu wote wakiwemo Wabunge walikuwa wanakutana pale Chako ni Chako wanakula kuku. Miaka mitatu/minne baadaye sehemu mbalimbali zinazotoa huduma kama za Chako ni Chako zimefunguliwa na wateja wanachagua sehemu za kwenda, *it is very natural*. Miaka kadhaa iliyopita, labda kabla sijafika huko, kama unaishi mtaani, nasema ninatumia analogia, lugha rahisi kabisa na mifano rahisi, kama unakaa mtaani na katika mtaa wako unapakana na mitaa mingine minne/mitano katika mitaa hiyo mitano hakuna baa, kuna baa moja tu katika mtaa wako watu wote wanaokunywa katika maeneo hayo watakunywa katika baa yako, lakini siku mtaa wa tatu wamefungua baa tabia ya walevi ni kwenda kujaribu katika baa nyingine pia. Lakini wakiwa kule wataweza kulinganisha na ubora wa huduma ya baa yako; hiyo ndio lugha ya analogia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaendesha Bandari yetu ya Dar es Salaam bandari nyingine zimefuata baadae na kwa kawaida kwa tabia ya watu hupenda kujaribu. Leo bandari nyingine zipo kwa vyovyote vile huwezi kubaki na wateja wale wale ambao ulikuwanao kwa kipindi chote. Hiyo ni lugha rahisi, Watanzania tusiyumbishwe na kauli za baadhi ya Wabunge kuonyesha kwamba sababu za kupungua mizigo bandarini zinahusiana moja kwa moja na mambo ya kodi, si kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, hilo haliondoi jukumu la Waziri wa Fedha kuendelea kuchunguza sababu mbalimbali za kupungua wateja, lakini sababu nyingine ndio hizo. Lazima kazi ya ziada ifanyike ili kuweza kuvuta wateja zaidi na kuweza kuimarisha bandari yetu ili iweze kuchangia mapato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kuona baadhi ya Wabunge tunawalilia wafanyabiashara makanjanja. Ni ajabu kuona kwamba katika bandari ile ile ambayo tunasema kwamba mizigo imepungua, mapato yameongezeka, mantiki yake ni nini? Mantiki yake ni rahisi tu, wale ambao walizoea ubabaishaji wameenda kubahatisha maeneo mengine labda wakabahatisha kubabaisha. Lakini wafanyabiashara makini wanaendela kutumia bandari yetu na hao ndio wanaotupa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi kwenye eneo hilo ni upotoshwaji wa mantiki nzima ya kusimamia matumizi na kukusanya kodi. Humu ndani baadhi yetu wametafsiri kama kubana matumizi; sijaona mantiki, bajeti ya mwaka jana tunayoimaliza mwaka huu ni shilingi trilioni 29 na mpango huu unatupeleka kwenye shilingi trilioni 32. Hiyo sio kubana matumizi, Serikali ya Awamu ya Tano inachokifanya ni kusimamia matumizi, kuna utofauti kati ya kubana matumizi na kusimamia matumizi. Serikali inachokifanya ni kuhakikisha inaongeza *efficiency* katika matumizi ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale maeneo ambayo hayana tija Serikali imepunguza kupeleka pesa na badala yake imepeleka maeneo yenye tija zaidi. Kwa hiyo, Watanzania tuelewe kwamba hatujabana matumizi isipokuwa tunapeleka fedha maeneo yenye tija zaidi, maeneo ambayo yatakuza uchumi zaidi na ndio maana bajeti imetoka toka shilingi trilioni 29 kwenda shilingi trilioni 32, hiyo ndio mantiki, ni kusimamia matumizi. Sasa wale waliozoea fedha rahisi, wale waliozoea ubabaishaji hilo nalo linawaumiza. Niwaombe Watanzania makini, wanaolipenda Taifa hili wamuunge mkono Mheshimiwa Rais katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuhakikishia katikati ya giza nene ndipo inakaribia asubuhi, hapa tulipo ndipo wakati sahihi kunakaribia kucha. Mheshimiwa Zitto Kabwe alisema lazima kuwe na maumivu tunapotaka kufanya mabadiliko makubwa kama haya. Tukumbuke miongoni mwetu baadhi ya Watanzania walizoea fedha rahisi, walizoweza leo anaanzisha biashara ya shilingi milioni 10 na kila mwezi anapata faida ya shilingi milioni tano kwa sababu, alikuwa anakwepa kodi. Tumueleze mantiki ya kodi na tumueleze kwamba biashara zinakuwa *steadily*, hatua kwa hatua. Watanzania makini hawana tatizo na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Mpango atoe ushirikiano na Mawaziri wengine waendeleo kuasimamia matumizi ya Serikali na kuelekeza pesa katika maeneo yenye tija zaidi kwa Watanzania. Hilo lilikuwa kuweka tu mazingira sawa kwa sababu niliona linapotoshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa ambalo leo nilitaka nichangie ni dhana nzima ya kukuza viwanda. Katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tumeweka bayana aina gani ya viwanda vitatutoa Tanzania kwa haraka zaidi. Tulisema tuwekeze kwenye viwanda vinavyosindika zaidi mazao ya kilimo kwa lengo kwanza la kumuwezesha mkulima mdogo apate soko la mazao yake, lakini pia kutoa ajira kubwa zaidi kwa Watanzania. Katika mpango tulioupata hilo halijawekwa bayana, tumeongelea viwanda vya *General Tyre*, tumeongelea viwanda vingine ambavyo kimsingi havigusi asilimia 80 ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosikitika kwenye mpango huu ni kwamba hatujaoanisha vizuri ile Ilani ya Chama cha Mapinduzi na huu mpango. Tunapowekeza nguvu nyingi kwenye kushughulikia viwanda tumesema ni jambo zuri, Magadi ya Soda - Bonde la Engaruka, tumeongea viwanda chini ya *TEMCO* na nini, lakini viwanda hivi katika ujumla wake haviendi kutatua tatizo la ajira kwa vijana wetu walio asilimia kubwa na wala haliendi kutatua tatizo la soko la mazao yetu ya kilimo. Kwa hiyo, niishauri sana Serikali kwenye hili lazima turudi tukafanye kazi upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine kwa haraka haraka, tunahangaika sana na soko la mahindi ni vema katika mpango huu sasa ikawekwa bayana. Kinachomfanya mkulima akalime ni bei ya mazao. Tunatoa ruzuku, lakini bado wakulima hawazalishi kwa tija kwa sababu hawapatii faida katika uzalishaji wao. Ipo haja sana ya kuja na sera madhubuti itakayomfanya mkulima mdogo wa Tanzania awe huru kuuza mazao yake kokote na wakati wowote. Leo ukienda kila mahali pikipiki zimejaa, Serikali imetoa ruzuku sana kwenye *power tiller*, lakini huzioni kokote kwa sababu hazina manufaa

kwenye kilimo chao, lakini watu wangapi wananunua yebo yebo kwa sababu hizo bodaboda kwa sababu wanajua zinawalipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutajenga mazingira mazuri kwenye sekta ya kilimo hatutahitaji kugharamia mbolea za ruzuku tena. Tujenge mazingira yenye ushindani kwenye sekta ya kilimo, tuwaache wakulima wadogo wauze mazao yao wanakotaka, anayetaka kupeleka Malawi, anayetaka kwenda Zambia na kama Serikali inataka kununua iingie kwenye ushindani. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumemuwezesha sana mkulima mdogo na wala hatutahangaika habari za kutafuta pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia muda ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante. Huyu ndio mchangiaji wetu wa mwisho wa leo. Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 3 Novemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*